# MUUNDO WA SIMULIZI WA RIWAYA YA KISWAHILI : UCHANGANUZI WA *VUTA N'KUVUTE*

**PETRONILLAH MUIYA KITHEKA**

**C50/11438/2018**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI, CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2022**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

17/2/2022

Petronillah Muiya Kitheka

Tarehe

C50/11438/2018

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii tulioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

23/2/2022

Prof. Kyallo Wadi Wamitila

Tarehe

23/2/2022

Dkt. Amiri Swaleh

Tarehe

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa, Bw. Justus Mitau na mamangu Bi. Patricia Annah.

# SHUKURANI

Namshukuru mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na uzima wa kimwili na kiakili kwenye kipindi nilichokuwa nafanya kazi hii na kwa kuniwezesha kuikamilisha.

Shukurani za dhati ziwafikie wasimamizi wangu Prof. Kyallo Wadi Wamitila na Dkt. Amiri Swaleh kwa ushauri, mawaidha, mwongozo na uvumilivu wao. Asanteni kwa kujitolea kusoma kila neno kwenye kazi hii. Mwenyezi Mungu awabariki.

Ninawashukuru wahadhiri wangu waliojitolea kutufunza kozi mbalimbali zilizotuekea msingi wa kazi hii. Wahadhiri hawa ni: Dkt. Mwaliwa, Prof. Mbuthia, Dkt. Zaja, Dkt. Jefwa Mweri, Prof. Mbatia, Prof. John Habwe, Prof. Wamitila, Prof. Olali, Prof. Rayya Timmamy, Prof. Kineene wa Mutiso, Dkt. Mukhwana na Dkt. Muungania. Mungu awazidishie mema maishani mwenu.

Kwa moyo wa upendo ninawashukuru wazazi wangu Bw. Justus Mitau na Bi. Patricia Annah kwa mapenzi, malezi na usaidizi mlionipa kila nilipowahitaji. Mungu awabariki na kuwazidishia maishani msije mkapungukiwa na chochote.

Vilevile ninatoa shukurani za dhati kwa ndungu zangu Peter Mitau, Reuben Mutia, Priscillah Kamene na Stephen Manzi. Mlinipa motisha na msukumo wa kumalizia kazi hii. Asanteni sana na Mungu awabariki. Sitomsahau Eric Munene aliyenifaa kwa mengi. Mungu akubariki sana.

Mwisho ningependa kuwashukuru wanafunzi wenzangu tulioshirikiana nao kwenye kozi hii ambao ni pamoja na: Esther Wanami, Anne Oruko, Emmah Opiyo, Paul Amadi na Patrick Mbae.

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza muundo wa simulizi kwenye riwaya ya *Vuta N'kuvute* yake Adam Shafi. Utafiti wetu ulikuwa na malengo ambayo ni kuchunguza muundo wa simulizi katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*, kuonyesha jinsi vipengele vya hadithi, matini na usimulizi vinavyodhihirika katika riwaya hiyo na kubainisha uamilifu wa vipengele vya simulizi katika kujenga ukamilifu wa riwaya ya *Vuta N'kuvute.* Utafiti uliongozwa na nadharia ya Naratolojia mtazamo wa Rimmon-Kenan (2002). Mihimili ya nadharia hii ndiyo iliongoza kwenye utafiti kwani ilisaidia kwenye uchunguzi wa usawiri wa wahusika na uwasilishaji wa usemi na mawazo yao. Vilevile, ilisaidia kuelewa jinsi kipengele cha wakati kinavyojitokeza kwenye riwaya ya *Vuta N'kuvute* na kubaini jinsi usimulizi na mtazamo unavyojitokeza. Utafiti ulikuwa wa maktabani na uchanganuzi na uwasilishwaji wa data ulikuwa kwa mbinu ya maelezo. Mapendekezo yaliyotolewa kwenye utafiti wetu ni kuwa, tafiti za baadaye zifanywe kuhusu riwaya zingine za Adam Shafi na pia tafiti za kiulinganishi kama vile kwenye riwaya na hadithi fupi kuhusu muundo wa simulizi.

YALIYOMO

**UNGAMO** .... ii

**TABARUKU** .... iii

**SHUKURANI** .... iv

**IKISIRI** .... v

**SURA YA KWANZA** .... 1

1.0 Utangulizi .... 1

1.1 Usuli wa Mada .... 1

1.2 Tatizo la Utafiti .... 3

1.3 Malengo ya Utafiti .... 4

1.4 Maswali ya Utafiti .... 4

1.5 Sababu za Kuchagua Mada .... 4

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti .... 5

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .... 5

1.8 Msingi wa Kinadharia .... 8

1.9 Mbinu za Utafiti .... 10

1.9.1 Aina ya Utafiti na Ukusanyaji wa Data .... 10

1.9.2 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data .... 10

2.0 Hitimisho .... 11

**SURA YA PILI** .... 12

**UHUSIKA NA UWASILISHAJI WA USEMI NA MAWAZO KATIKA RIWAYA YA *VUTA N'KUVUTE*** .... 12

2.0 Utangulizi .... 12

2.1 Mbinu za Usawiri wa Wahusika .... 12

2.1.1 Usawiri wa moja kwa moja .... 12

2.1.2 Usawiri usio wa moja Kwa moja .... 16

2.2 UWASILISHAJI WA USEMI NA MAWAZO YA WAHUSIKA .... 30

2.3 Utangulizi .... 30

2.4 Uwasilishaji wa Usemi wa Wahusika .... 30

2.4.1 Usemi Halisi ........ 30
2.4.2 Usemi Taarifa ........ 32
2.4.3 Usemi Taarifa Huru ........ 33
2.4.4 Muhtasari wa Daigesia ........ 34
2.4.5 Muhtasari wa Daigesia usio kamili ........ 34
2.5 UWASILISHAJI WA MAWAZO YA WAHUSIKA ........ 35
2.5.1 Mawazo Halisi ........ 36
2.5.2 Mawazo Taarifa ........ 39
2.5.3 Mawazo Taarifa Huru ........ 40
2.6 Hitimisho ........ 42
**SURA YA TATU ........ 43**
**WAKATI NA MUUNDO WA SIMULIZI ........ 43**
3.0 Utangulizi ........ 43
3.1 Mpangilio wa matukio ........ 43
3.1.2 Analepsia ........ 44
3.1.3 Prolepsia ........ 46
3.2 Muda wa Matukio ........ 46
3.2.1 Udondoshi ........ 47
3.2.2 Muhtasari ........ 50
3.2.3 Onyesho/ Maonyesho ........ 51
3.2.4 Mtuo ........ 54
3.3 Idadi Marudio ........ 56
3.3.1 Usimulizi Mosi ........ 56
3.3.2 Usimulizi Rudufu ........ 57
3.3.3 Usimulizi Banifu ........ 61
3.4 Hitimisho ........ 62
**SURA YA NNE ........ 64**
**USIMULIZI NA MTAZAMO KATIKA *VUTA N'KUVUTE* ........ 64**
4.0 Utangulizi ........ 64

4.1 Aina za Usimulizi ........ 64
4.1.1 Usimulizi baadaye ........ 64
4.1.2 Usimulizi wa kitabiri ........ 65
4.1.3 Usimulizi sawia ........ 66
4.2 Aina za usimulizi kwa kuzingatia kigezo cha Nafsi ........ 67
4.2.1 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu ........ 67
4.3 Utambuzi wa msimulizi ........ 69
4.3.1 Ufafanuzi wa mandhari ........ 69
4.3.2 Muhtasari wa muda ........ 70
4.3.3 Uelezaji wa wahusika ........ 71
4.4 Mtazamo ........ 72
4.4.1 Aina kuu za mtazamo ........ 72
4.5 Sawia za uchunguzi wa mtazamo ........ 73
4.5.1 Sawia ya mwanda-wakati ........ 73
4.5.2 Sawia ya kisaikolojia ........ 75
4.5.3 Sawia ya kitathmini ........ 76
4.5.4 Sawia ya kilugha au kiisimu ........ 78
4.6 Hitimisho ........ 81
**SURA YA TANO ........ 82**
**HITIMISHO ........ 82**
5.0 Utangulizi ........ 82
5.1 Muhtasari wa utafiti ........ 82
5.2 Matokeo ya Utafiti ........ 83
5.3 Mapendekezo kuhusu utafiti wa baadaye ........ 84
5.4 Kiishio ........ 84
**MAREJELEO ........ 85**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Utafiti huu ulishughulikia muundo wa simulizi katika riwaya ya Kiswahili kwa kujikita kwenye riwaya ya Adam Shafi, *Vuta N'kuvute* (1999). Uchanganuzi uliongozwa na nadharia ya Naratolojia mtazamo wa Rimmon-Kenan (2002). Kulingana na Rimmon-Kenan, muundo wa simulizi hujikita katika hadithi, matini yenyewe na usimulizi katika kuwasilisha ujumbe kwa msomaji. Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni kuchunguza muundo wa simulizi katika riwaya ya *Vuta N'kuvute,* kuonyesha jinsi vipengele vya hadithi, matini na usimulizi vinadhihirika katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* na kubainisha uamilifu wa vipengele vya simulizi katika kujenga ukamilifu wa riwaya ya *Vuta N'kuvute*.

## 1.1 Usuli wa Mada

Prince (1987) anasema kuwa, simulizi ni uwasilishaji wa tukio moja au matukio mengi ambayo ni ya uhalisia au ya kubuni ambayo yanawasilishwa na msimulizi mmoja, wawili au zaidi. Kutokana na maelezo haya, ni dhahiri kuwa lazima kuwepo na tukio au matukio ambayo yanaweza kuthibitishwa kwenye hali halisi ya maisha au matukio ambayo ni ya kubuniwa na lazima yamhusishe mtu ambaye anasimulia na anaweza kuwa mmoja au wengi.

Simulizi ni diskosi ambayo inaweza kuzungumziwa au iliyoandikwa ambayo hunuia kuelezea tukio au mfuatano wa matukio na pia inaweza kutazamwa kama tukio ambalo linahusisha mtu anayesimulia kilichotendeka (Genette: 1980).

Uchanganuzi wa muundo na namna matukio yanavyowasilishwa huhusisha uhusiano kati ya simulizi na hadithi, simulizi na usimulizi na hadithi na usimulizi na huu ndio muundo unaopatikana kwenye simulizi. Hivyo basi, ndiposa simulizi iwe na muundo maalum, lazima uhusiano baina ya vipengele mbalimbali uwepo ili mawazo na ujumbe uweze kuwasilishwa kwa namna inayofaa.

Rimmon-Kenan (2002) anaieleza simulizi ya kibunilizi kama usimulizi wa mfuatano wa matukio ya kibunilizi. Anafafanua usimulizi kama mchakato ambapo ujumbe wa simulizi hupitia kwa anayesimulia hadi anayesimuliwa na mbinu ya kusimulia inayotumika kupitisha ujumbe huo na hili ndilo hutofautisha simulizi za kibunilizi na simulizi zingine kama vile za

filamu na za densi. Vilevile, anaendeleza mawazo yake kwa kusema kuwa simulizi huhusisha zaidi ya tukio moja.

Isitoshe, Rimmon-Kenan anasema kuwa muundo wa simulizi umejengwa kwa vipengele vitatu vikuu ambavyo ni matini, hadithi na usimulizi. Vipengele hivi vitatu, kwa mujibu wa Rimmon- Kenan, lazima vikamilishane ili simulizi iweze kufanikisha malengo yake.

Kimsingi, uchambuzi wa diskosi ya simulizi ni stadi ya uhusiano kati ya simulizi, hadithi na usimulizi. Hivyo basi, ndiposa simulizi iwe na muundo maalum lazima kuwepo na muumano baina ya vipengele hivi mbalimbali ili mawazo ya mwandishi wa riwaya yaweze kuoana. Isitoshe, muumano wa vipengele hivi muhimu vya simulizi husababisha uwasilishaji unaofaa wa ujumbe katika riwaya.

Anaieleza hadithi kama inayowasilisha matendo yaliyosimuliwa katika matini iliyoundwa kwa mfuatano wa utokeaji wa matukio kiwakati, pamoja na wahusika kwenye matukio hayo. Mathalan:

A → B → C → D → E

Mwanzo Mwisho

Matini ni diskosi ya mazungumzo au iliyoandikwa ambayo huhusisha usimuliaji wa matukio, kwa maana ya kile ambacho husomwa. Kipengele cha matini katika simulizi huwasilisha ujumbe kwa msomaji wa hadithi kwa njia maalum, kama vile kutumia lugha, matumizi ya picha na sauti au muungano wa lugha, matumizi ya picha na sauti. Kwa upande mwingine, usimulizi ni tendo au mchakato wa uzalishaji wa simulizi. Usimulizi hujikita katika uorodheshaji wa matukio katika hadithi.

*Vuta N'kuvute* ni riwaya inayozungumzia maisha ya msichana aitwaye Yasmin pamoja na Denge na kundi lake la vijana wakiwemo Mambo, Chande, Sukutua, Huseni na wengineo wanaopigania ukombozi dhidi ya utawala wa kikoloni Zanzibar. Yasmin anazungukwa na maisha yenye matatizo mengi yakiwemo kuozwa akiwa na umri mdogo na kulazimishwa kuwa mke wa jizee la miaka hamsini na mbili na maisha ya uchochole. Vilevile, Yasmin anajipata kwenye mahusiano na watu mbalimbali wakiwemo Denge, Shihab na Bukheti

baada ya kumkimbia mumewe Bwana Raza. Vijana wanaojaribu kutetea haki za wananchi wananyanyaswa, kupewa vitisho vya mara kwa mara na kukamatwa na kupitia mateso gerezani huku wakiitwa Makomunisti kwa kuwa wanaonekana kujaribu kubadili mienendo ya wanyanyasaji wanaowatawala kimambavu. Upande wa wanyanyasaji, unatumia nguvu za dola huku ukiongozwa na Inspekta Wright, askari kanzu, maafisa wa kikoloni na kamishna wa polisi ambaye ni mzungu. Matukio yaliyomo katika riwaya hii yanapatikana katika mandhari mbalimbali yakiwemo ya Mombasa lakini kwa kiasi kikubwa yanatukia Zanzibar ambako harakati za kimapinduzi zinaendelezwa na Denge na kundi lake.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Muundo wa simulizi huhusisha vipengele vitatu vikuu vinavyopatikana katika kazi za kifasihi kuletwa pamoja na mtunzi wa kazi ya fasihi ili kukamilisha kazi yake. Vipengele hivyo hutokana na msisitizo na ubainikaji wake na pia hutegemea mtunzi na mkondo wa mwandishi. Vipengele hivyo ni kama vile hadithi, matini na usimulizi.

Muundo wa simulizi humsaidia msomaji kuelewa zaidi kazi ya fasihi kwa kumpa maarifa zaidi ya jinsi mtunzi amewasilisha hadithi yake, matini yake na kutambua usimulizi unavyojitokeza huku ukimpa uelewa ni nani anayezungumza na ni kwa kiwango kipi na kama yupo kwenye kisa chenyewe au la. Vilevile humsaidia msomaji kuwa na mtazamo tofauti na aliouzoea anaposoma kazi za kifasihi kwani uweza kuelewa zaidi kinachotendeka katika matini husika.

Kimsingi, utafiti huu ulishughulikia vipengele mahsusi vinavyotajwa na kuchunguzwa na Rimmon-Kenan (2002) ambavyo ni hadithi, matini na usimulizi na kila kipengele kina visehemu vingine vidogo vidogo. Usimulizi uliangaziwa kwa kuchunguza aina za usimulizi, utambuzi wa msimulizi pamoja na mtazamo kwa kuangazia aina kuu za mtazamo na sawia mbalimbali zitumiwazo kuuchunguza. Katika kipengele cha wakati, tuliangazia jinsi matukio yalivyopangwa, muda ambao matukio yanachukua katika hadithi na idadi ya utokeaji wa tukio kwa kuthibitisha ni mara ngapi tukio fulani limetukia na limesimuliwa mara ngapi. Kipengele cha uhusika na wahusika kilichunguzwa kwa kuangazia mbinu mbalimbali zilizotumika kuwasawiri wahusika na jinsi usemi na mawazo ya wahusika yalivyowasilishwa na athari zake kwa riwaya nzima. Utafiti huu ulishughulikia muundo wa simulizi katika riwaya ya Kiswahili tukijikita katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* yake Adam Shafi.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yalikuwa yafuatayo;

i)Kuchunguza muundo wa simulizi katika riwaya ya *Vuta N'kuvute.*

ii)Kuonyesha jinsi vipengele vya hadithi, matini na usimulizi vinavyodhihirika katika riwaya ya *Vuta N'kuvute.*

iii)Kubainisha uamilifu wa vipengele vya simulizi katika kujenga ukamilifu wa riwaya ya *Vuta N'kuvute.*

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo;

i) Je, ni kwa jinsi gani muundo wa simulizi umewasilishwa katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*?

ii) Vipengele vya hadithi, matini na usimulizi vinadhihirikaje katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*?

iii) Ni uamilifu upi unaotekelezwa na vipengele vya simulizi katika kujenga ukamilifu wa riwaya ya *Vuta N'kuvute*?

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Riwaya ya *Vuta N'kuvute* haijachunguzwa kwa mkabala na maoni ya Rimmon-Kenan kadri tunavyojua. Mkabala wa Rimmon-Kenan ni mwendelezo na uboreshaji wa mawazo ya Genette (1980). Uendelezaji na uboreshaji wa mawazo ya Genette unabainika kupitia kwa mpangilio alioibuka nao Rimmon-Kenan kwa kuvipanga vipengele vya simulizi upya na kwa njia tofauti na alivyofanya Genette. Vipengele vya simulizi kulingana na Genette vilikuwa sauti, wakati na hali. Rimmon-Kenan (2002) aliviendeleza vipengele vya Genette kwa kuibuka na hadithi, matini na usimulizi huku kipengele cha matini kikihusisha wakati na hali na kipengele cha usimulizi kikihusisha sauti. Vilevile Rimmon-Kenan aliibua vipengele vingine tofauti katika mtazamo wake vikiwemo uhusika, wahusika na matukio. Vipengele hivi vilitupa msukumo wa kuteua mada hii kwani simulizi huhusisha uhusika na wahusika na ni vyema kuchunguza vipengele hivyo na pia tulitaka kuelewa matukio yanavyotokea katika riwaya ya *Vuta N'kuvute.*

Isitoshe, utafiti huu utakuwa na faida nyingi kwa wasomi na watafiti wa sasa na wa baadaye, kwani utawapa msingi wa uelewa wa muundo wa simulizi katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* na fasihi ya Kiswahili ambao haujafanyiwa utafiti katika riwaya hii na nyingine za Kiswahili.

## 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijihusisha tu na muundo wa simulizi katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* (1999) kwa kujikita kwenye vipengele vitatu vikuu ambavyo ni hadithi, matini na usimulizi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Naratolojia kwa mtazamo wa Rimmon-Kenan (2002). Mtazamo huu ndio ulitumika kuchanganua vipengele vilivyochambuliwa katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* kuhusu muundo wa simulizi.

Utafiti huu hasa ulishughulikia wahusika na uhusika pamoja na uwasilishaji wa usemi na mawazo ya wahusika, wakati na usimulizi pamoja na mtazamo kwa kuwa vipengele hivi vipo tele kwenye matini husika.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Ong'ondi (2005) alitafiti usimulizi katika riwaya ya *Walenisi* (1995) ya Katama Mkangi akingozwa na nadharia ya Naratolojia mkabala wa Genette. Matokeo ya utafiti wa Ong'ondi yalidhihirisha kuwa mitazamo mbalimbali ilitumika kwenye usimulizi wa matukio hadithini na nafsi ya tatu ndiyo ilitamalaki kwenye usimulizi ikilinganishwa na ya nafsi ya kwanza iliyopatikana kwenye sehemu chache tu. Usimulizi horomo vilevile ulijitokeza kwa kuhusishwa na mazungumzo ya wahusika. Kipengele cha wakati vilevile kilishughulikiwa na kuonekana kuwa kinadhihirika katika riwaya ya *Walenisi*. Umuhimu wa utafiti wake kwa kazi yetu ni kuwa ulitumia nadharia ya Naratolojia ambayo tumeitumia kwenye utafiti wetu japokuwa kwa mtazamo tofauti japo utafiti wake ni wa riwaya kama ulivyo wetu.

Shitemi (2011) alishughulikia usimulizi katika *Utenzi wa Siri Li Asirali* katika tasnifu yake ya uzamifu. Alichunguza iwapo utenzi huu unapowasilishwa unatumia mbinu za usimulizi pamoja na kuonyesha arki za kisimulizi zilizoko kwenye utenzi huo. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya Naratolojia mkabala wa Rimmon-Kenan (2002). Utafiti wake ulibaini kuwa, msimulizi alidhihirisha hisia zake kwa msomaji na matukio yaliyosimuliwa baada ya kutokea kwake ndiyo yalitamalaki kwenye utenzi huo. Mbinu za uwasilishaji mawazo zilijitokeza kwenye utenzi japokuwa kwa uchache zikilinganishwa na za

uwasilishaji wa usemi. Umuhimu wa utafiti huu kwa utafiti wetu ni kuwa ulitumia nadharia ya Naratolojia tuliyoitumia kwenye utafiti wetu japokuwa alijishughulisha na utenzi tofauti na utafiti wetu ulioshughulikia riwaya.

Kimani (2012) alishughulikia arki za simulizi bunilizi kwenye U*tendi wa Mikidadi na Mayasa* kwa kuongozwa na nadharia ya Naratolojia mwegemeo wa Rimmon-Kenan (2002). Vipengele alivyovichunguza ni wakati, wahusika, mtazamo katika usimulizi na uwasilishaji wa usemi na mawazo. Utafiti wake ulibaini kuwa, msimulizi mseto yupo na kiwango kinachowasilisha hadithi kuu kilijidhihirisha kwani hakuna vijihadithi vilivyojitegemeza. Wahusika vilevile walisawiriwa kwa viashiria mbalimbali na usimulizi kabla ulibainika kuwa wa kiwango kidogo ukilinganishwa na wa baadaye. *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* vilevile ulidhihirisha kuwa, mbinu za uwasilishaji wa usemi ndizo zilithibitishwa bila uwepo wa uwasilishaji wa mawazo. Utafiti huu ni muhimu kwa kuwa ulitumia nadharia ya Naratolojia mtazamo wa Rimmon-Kenan ambao tumeutumia kwenye utafiti wetu japokuwa ni tofauti na kazi yetu kwa kujikita kwenye utendi tofauti na riwaya tuliyoishughulikia.

Arege (2012) katika tasnifu yake ya uzamifu, alishughulikia usimulizi katika *Utenzi wa Rasi'l Ghuli* kwa kuongozwa na nadharia ya Naratolojia mkabala wa Genette(1980). Malengo ya utafiti wake yalikuwa ni kutambua mikakati mbalimbali ya usimulizi iliyotumika katika *Utenzi wa Rasi'l Ghuli*, kuonyesha utendakazi wa mikakati mbalimbali ya usimulizi iliyotumika katika kujenga muundo wa usimulizi katika *Utenzi wa Rasi'l Ghuli* na kujadili athari za muundo wa *Utenzi wa Rasi'l Ghuli* katika usimulizi. Alishughulikia kipengele cha wakati, daraja za usimulizi, sauti za usimulizi, uhusika na wahusika. Utafiti wake ulibaini kuwa, prolepsia na analepsia zimetumika katika utenzi huu japokuwa analepsia ilijitokeza kwa kiasi kikubwa zaidi. Nafsi zote zilidhihirika kwenye utafiti wake. Utambulisho wa wahusika wa moja kwa moja na usio wa moja kwa moja vilevile ulijitokeza. Utafiti huu ni muhimu kwa kazi yetu kwa kuwa ulitumia nadharia ya Naratolojia tuliyoitumia katika utafiti wetu na hivyo, kutupa mwelekeo muhimu.

Khamis (2015) alishughulikia uhakiki wa usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba Cha Moyo* (2009) *na Mstahiki Meya* (2009). Vipengele alivyovichunguza ni wakati, daraja na sauti za usimulizi, wahusika na uhusika kwa kuongozwa na nadharia ya Naratolojia mtazamo wa

Genette (1980). Analepsia ikilinganishwa na prolepsia ilijitokeza zaidi kwenye tamthilia husika. Kipengele cha idadi marudio na muda vilibainika pia. Zaidi ya hayo, daraja na sauti za usimulizi pamwe na aina za wasimulizi pia zilijidhihirisha. Kazi yake ina umuhimu kwa utafiti wetu kwa kuwa ilitufaa kwa uchanganuzi wa vipengele vya wakati, uhusika, daraja na sauti za usimulizi. Tofauti na utafiti wa Khamis, utafiti wetu ulijikita kwenye riwaya.

Burundi na wenzake (2017) walitafiti kuhusu usimulizi katika *Utenzi wa Swifa Ya Nguvumali*. Utafiti wao ulitaka kubaini anayesimulia ni nani, ni usimulizi wa aina gani uliotumiwa na maajenti waliotumika kukamilisha usimulizi huo wakiongozwa na nadharia ya usimulizi. Walibaini kuwa, nafsi ya kwanza na ya tatu ndizo zimetumika kusimulia matukio. Msimulizi wa nafsi ya kwanza amedhihirika kutokana na jinsi alivyoyaeleza matukio jambo linalomfanya kuwa mtazamaji au shahidi wa matukio hayo. Msimulizi anayeaminika kujua kila kitu kinachotendeka hadithini vilevile alijidhihirisha kwenye utenzi huu na pia msimulizi horomo ambaye huwa hausiki na lolote kama vile kutenda hadithini. Umuhimu wa utafiti huu kwa kazi yetu ni kuwa, ulishughulikia kipengele cha usimulizi ambacho tulikishughulikia katika kazi yetu japokuwa ulijikita kwenye utenzi bali na utafiti wetu unaohusu riwaya.

Wambui (2018) alichunguza usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini* (2007). Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya Naratolojia mtazamo wa Genette (1980). Ilibainika kuwa, msimulizi ni wa ndani pamwe na uwepo wa usimulizi wa nafsi zote. Vilevile hadithi za viwango tofauti tofauti na wasimulizi wake vilijitokeza. Aidha, analepsia ilijitokeza zaidi ikilinganishwa na prolepsia. Umuhimu wa utafiti huu ni kuwa, ulitumia nadharia sawia na ya utafiti tulioufanya ambayo ni ya Naratolojia na pia ulishughulikia baadhi ya vipengele ambavyo tulivishughulikia. Utafiti wake ni wa riwaya japokuwa riwaya tuliyoishughulikia ni tofauti na aliyoihakiki yeye.

Kwaka (2018) alifanya utafiti wa wakati na uwasilishaji usemi kama vipengele vya usimulizi katika *Utenzi wa Nabii Isa* akitumia nadharia ya Naratolojia mkabala wa Genette (1980). Vipengele alivyovishughulikia ni wakati na uwasilishaji usemi. Kwake, analepsia imetumika zaidi kuliko prolepsia. Vipengele vya muda na vya idadi marudio vilevile vilipatikana kwa wingi kwenye utafiti wake. Uwasilishaji usemi pia ulitumika katika *Utenzi wa Nabii Isa* na

kuonyesha namna lugha na mawazo hutumiwa na wahusika kufanikisha mawasiliano. Utafiti huu kama ulivyo utafiti wetu, ulitumia nadharia ya Naratolojia na ulitufaa sana katika uelewa wa nadharia hiyo. Tofauti na utafiti wetu, utafiti huu ulijikita katika utenzi ilhali wetu ulikuwa wa riwaya.

## 1.8 Msingi wa Kinadharia

Nadharia iliyouongoza utafiti huu ni ya Naratolojia. Naratolojia kama asemavyo Bal (2009), hujihusisha na simulizi pamwe na matini zake, ambayo hutumia picha na kuhusisha matendo na vifaa vilivyoko kiutamaduni kuelezea hadithi. Naratolojia husaidia kuamili, kuhakiki na kuchunguza simulizi kwa undani. Kimsingi, nadharia ya Naratolojia huchagua sifa zinazoambatanishwa na simulizi na kuweka kando zisizohusiana. Chukulizi iliyoko kwenye nadharia hii ni kuwa, matini hufuata kanuni maalum.

Historia ya nadharia hii inafahamika kutokana na kuwa ilitokana na nadharia ya umuundo ambayo hutilia mkazo uchunguzaji wa muundo na jinsi simulizi hufanya kazi kwa kuangazia sifa zake. Plato ndiye aliuweka msingi wa nadharia hii kwenye andiko la *The Republic* katika kitabu cha tatu cha andiko hilo. Plato aliibua dhana mbili katika kazi yake ambazo ni mimesia na daigesia. Plato alieleza *mimesia* kama uigaji na *daigesia* kama usimuliaji. Baadaye, Aristotle ambaye alikuwa mwanafunzi wa Plato, aliyaendeleza maelezo ya mimesia na daigesia kwenye *Poetics* ambayo ilikuwa kazi yake.

Miaka ya 1920 ni muhimu kwenye nadharia hii kwani inahusishwa na kazi za Kirusi zinazoaminika kuleta mwanga zaidi wa ufahamu wa nadharia hii. Lord Raglan (1936) ni kati ya wataalamu walioendeleza ukuaji wa Naratolojia kwenye kazi yake *The Hero* kwa kuchunguza visaasili mbalimbali vya maisha ya mashujaa wa kitamaduni kwenye jamii mbalimbali kwa kuangazia tungo zao.

Vilevile Vladmir Propp, kwenye *The Morphology of The Folktale* alitafiti zaidi ya hurafa 100. Baadaye, mwaka wa 1966 ndio Naratolojia ilifahamika kama kungwi kutokana na makala ya "*Communications"* kuchapishwa yaliyonuia kuhakiki hadithi kimuundo. Wataalamu ambao walihusika na makala haya ni Greimas, Genette, Barthes, Bremond na Todorov na ndio wanachukuliwa kuwa waanzilishi wa nadharia hii.

Isitoshe, utafiti wetu ulitumia mtazamo wa Rimmon-Kenan (2002) kwa kuwa alipanga na kuwasilisha vipengele vya simulizi kwa kuviweka pamoja jinsi vinavyohusiana moja kwa

moja na pia vinavyotegemeana. Utafiti wetu ulijikita kwenye mihimili ya nadharia ya Naratolojia kama ifuatavyo: Uhusika na uwasilishaji usemi na mawazo ya wahusika, wakati, usimulizi na mtazamo.

Usimulizi ni kipengele muhimu sana kwa kuwa huweza kueleza aina mbalimbali za usimulizi. Usimulizi unaweza kuwa wa baadaye, wa kiutabiri, usimulizi changamano na usimulizi sawia. Pamoja na hayo, usimulizi huhusisha aina za wasimulizi na ishara mbalimbali zitumiwazo kwenye utambuzi wa msimulizi. Mtazamo kwa upande wake ni muhimu kwa kuwa humsaidia msomaji kuelewa msimulizi ana msimamo upi kuhusu masuala fulani, maoni yake kuhusu hali fulani na anajitambulisha na nani. Vilevile, mtazamo kwa kuangazia aina zake husaidia kutambua kama msimulizi wa hadithi yupo kwenye ulimwengu wa hadithi au yupo nje yake.

Wakati ni kipengele muhimu sana katika kazi za kisimulizi. Kipengele hiki huelezea jinsi wakati umeshughulikiwa kwenye hadithi fulani. Wakati katika simulizi za kibunilizi unaweza kuelezwa kama mfuatano wa kikronolojia kati ya hadithi na matini. Kipengele hiki hutazamwa kwa kuangalia dhana ya wakati hadithi na wakati matini. Wakati hadithi ni wakati ambao hadithi fulani huchukua kuanzia mwanzo hadi mwisho. Wakati hadithi unaweza kuwa wa siku moja, wiki moja, wiki tano, kumi, mwaka mmoja au miaka mingi. Wakati matini ni wakati ambao msomaji hutumia kusoma matini fulani. Mpangilio huchunguzwa kama kigezo chini ya wakati ambapo matukio yanaweza kusimuliwa kwa kuangalia jinsi yanavyofuatana kiwakati au kwa kutofuatana kiwakati pale ambapo matukio mengine yanaweza kuwasilishwa kwa mtindo wa kianalepsia au kiprolepsia. Muda pia huchunguzwa kwa kuangalia kipindi ambacho tukio fulani limechukua liwe limechukua muda mfupi au muda mrefu. Idadi marudio hutumika kuelezea ni mara ngapi tukio fulani limetokea na limesimuliwa mara ngapi.

Usawiri wa wahusika husaidia kuwaelewa wahusika waliomo kwenye simulizi. Wahusika wanaweza kusawiriwa kwa njia ambayo ni ya moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Kwenye usawiri wa njia ya moja kwa moja, mhusika huelezwa kwa njia ya moja kwa moja kwa kutumia vivumishi, nomino dhahania na aina nyingine za maneno. Vilevile, msimulizi au mhusika katika kazi husika anaweza kuzitaja sifa za mhusika mwingine. Kwa upande wa usawiri usio wa moja kwa moja, sifa za mhusika huwa hazitajwi bali msomaji

hupewa nafasi ya kutambua sifa mbalimbali za wahusika. Sifa za mhusika zinaweza zikajitokeza au zisijitokeze moja kwa moja hivyo basi, huwa ni jukumu la msomaji kuchunguza viashiria mbalimbali vinavyojenga sifa za mhusika fulani. Baadhi ya viashiria ni kama, matendo ya mhusika, mazungumzo ya mhusika, mwonekano wa nje, mavazi, mazingira aliyomo, majazi na analojia.

Kipengele cha uwasilishaji usemi na mawazo ya wahusika, hutumiwa kwa kuangazia lugha inavyotumika kutoa maana. Uwasilishaji wa usemi huhusisha uwasilishaji wa semi za wahusika ambazo ni za moja kwa moja wanapozungumza na wahusika wenzao. Kwa upande wa uwasilishaji wa mawazo ya wahusika huhusisha uwasilishaji wa mawazo ya wahusika ambayo hutokana na mambo yanayotokea akilini mwao wala si mazungumzo ya moja kwa moja. Baadhi ya mbinu ambazo hutumiwa kuwasilisha usemi na mawazo ya wahusika katika kazi ya fasihi ni usemi halisi, usemi halisi huru, usemi wa taarifa, usemi taarifa huru, mawazo halisi, mawazo halisi huru, mawazo ya taarifa na mawazo ya taarifa huru.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii ilihusisha aina ya utafiti, ukusanyaji data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

### 1.9.1 Aina ya Utafiti na Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani ambapo tulisoma riwaya ya *Vuta N'kuvute* (1999) kwa kuzingatia nadharia yetu tuliyoiteua. Tuliainisha na kuchunguza vipengele vya simulizi vilivyomo kwa kuongozwa na nadharia ya Naratolojia mkabala wa Rimmon-Kenan (2002). Aidha, tulisoma tasnifu, majarida na vitabu vinavyozungumzia mada yetu ya utafiti. Pamoja na hayo, tulisoma mtandaoni makala yaliyohusiana na utafiti huu bila kuwaacha nyuma wataalamu na wasomi wa fasihi kwa kuwa walitufaa sana kwa ushauri wao.

### 1.9.2 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Baada ya kukusanya data yetu, tuliichanganua kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya Naratolojia mtazamo wa Rimmon-Kenan (2002) ili kuweza kuchunguza muundo wa simulizi wa riwaya ya *Vuta N’kuvute*. Vipengele vilivyochunguzwa ni hadithi, matini na usimulizi. Pindi tu tulipokamilisha kuchanganua data, tuliiwasilisha kwa mbinu ya maelezo, tukitolea mifano vipengele vya simulizi vilivyodhihirika kwenye *Vuta N’kuvute*.

## 2.0 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia utangulizi wa utafiti, usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi wa Kinadharia na mbinu za utafiti. Kwenye sehemu ya mbinu za utafiti, tumeangazia aina ya utafiti ambao umebainika kuwa wa maktabani na uchanganuzi wa data ambao umefanywa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya Naratolojia na uwasilishaji wa data ambao utakuwa wa njia ya maelezo.

# SURA YA PILI

# UHUSIKA NA UWASILISHAJI WA USEMI NA MAWAZO KATIKA RIWAYA YA *VUTA N'KUVUTE*

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia masuala mawili makuu ambayo ni uhusika na uwasilishaji wa usemi na mawazo katika riwaya ya *Vuta N'kuvute.* Katika sehemu ya kwanza ya uhusika na wahusika, sura hii ilinuia kuonyesha mbinu mbalimbali zilizotumika kuwasawiri wahusika ili kutusaidia kuwaelewa. Sura hii ilinuia kuthibitisha kuwa kuna usawiri wa wahusika ambao ni wa moja kwa moja na ule usio wa moja kwa moja. Kwenye usawiri usio wa moja kwa moja, utafiti ulitaka kubaini kama mbinu mbalimbali ambazo hutumika kuwasawiri wahusika zimetumika katika riwaya teule. Mbinu hizo ni: mazingira wanamopatikana wahusika, mavazi wanayovaa, mwonekano wao wa nje, usemi, matendo yao, analojia na hali zao za saikolojia.

Kwa mujibu wa sura hii, wahusika wanadhihirika kama viumbe wa wanasanaa ambao hubuniwa na msanii kutoka mazingira mahsusi. Aidha, ni kipengele muhimu cha fani. Msanii huwaweka wahusika wake katika mandhari yatakayomsaidia kuwasilisha hoja zake kutokana na vitendo, maingiliano na fikira zao. Wahusika ambao wanaweza kuwa binadamu, wanyama, mizimu au vitu vinginevyo hadithini wanaotokana na mawazo ya mwandishi na wanaumbwa ili kuwasilisha ujumbe wake.

## 2.1 Mbinu za Usawiri wa Wahusika

Wahusika wa kifasihi wanaweza kusawiriwa kwa namna mbili kuu ambazo ni kwa njia ya moja kwa moja na kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja.

### 2.1.1 Usawiri wa moja kwa moja

Vivumishi, nomino dhahania au aina nyingine za maneno, ndizo hutumika kubainisha usawiri wa moja kwa moja wa wahusika (Rimmon-Kenan, 2002). Sifa za mhusika zinapotajwa moja kwa moja, huwa zinaweza kuaminika ikiwa sauti inayozungumza ina nguvu zaidi kwenye matini husika yaani ikiwa msimulizi atataja sifa za mhusika, zitachukuliwa kwa uzito mwingi kuliko sifa hizo zikitajwa na mhusika mwenzake.

Riwaya ya *Vuta N'kuvute* ina baadhi ya mifano ya usawiri wa wahusika kwa njia ya moja kwa moja. Kwa mfano, msimulizi anavyoeleza sifa za Bwana Raza anasema:

> Alikuwa ni mume asiyelingana naye hata kidogo. Si kwa umri wala tabia kwani wakati Yasmin ni kigoli wa miaka kumi na tano tu, mumewe Bwana Raza alikuwa zee la miaka hamsini na mbili (uk.1)

Maelezo ya msimulizi kumhusu Bwana Raza ni ya moja kwa moja kwani msimulizi anamwelezea msomaji kuwa, Bwana Raza hakulingana na Yasmin kwa lolote kwani alikuwa na miaka kumi na tano na Bwana Raza alikuwa na miaka hamsini na mbili. Kivumishi "zee" kimetumika kuonyesha alivyokuwa Bwana Raza na kwa kuwa sauti inayozungumza ni ya msimulizi, sifa za Bwana Raza zinaaminika zaidi kuliko jinsi zingeaminika lau zingetajwa na mhusika mwenzake. Vilevile, msimulizi anatoa sifa za moja kwa moja kumhusu Yasmin katika ukurasa huo huo kama ifuatavyo:

> Yasmin alikuwa na kijuso kidogo cha mdawari mfano wa tungule na macho makubwa ambayo kila wakati yalionekana kama yanalengwalengwa na machozi. Alikuwa na pua ndogo, nyembamba na chini ya pua hiyo ilipangana midomo miwili mizuri iliyokuwa haitulii kwa tabia yake ya kuchekacheka, huku akionyesha safu mbili za meno yake mazuri. Alikuwa na kichaka cha nywele nyeusi zilizokoza ambazo zilianguka kwa utulivu juu ya mabega yake. Alikuwa si mrefu lakini hakuwa mfupi wa kuchusha na matege aliyokuwa nayo yalizidi kuutia haiba mwendo wake wakati anapotembea (uk.1)

Kutokana na dondoo hili, tunafahamu Yasmin alivyokuwa mzuri kutokana na maelezo ya msimulizi. Yasmin anaonekana kuwa na macho makubwa ambayo wakati wote yalikuwa kama yanalengwalengwa na machozi na midomo miwili mizuri iliyokuwa haitulii kutokana na tabia yake ya kuchekacheka. Ni wazi kwamba msimulizi alitaka kumsawiri Yasmin kama msichana mzuri mwenye kupendeza kutokana na vivumishi alivyovitumia kama anavyosema, "alikuwa na kijuso kidogo cha mdawari na alikuwa na pua ndogo nyembamba".

Usawiri wa moja kwa moja vilevile unabainika pale ambapo msimulizi anatueleza kumhusu Mwajuma aliyekuwa rafiki wa Yasmin. Maelezo anayoyatoa msimulizi kumhusu Mwajuma, yanaonyesha kuwa ndiyo yalimvutisha Mwajuma kwa watu wengine mtaani kwani alikuwa kivutio kwa wazee, vijana na vizee. Msimulizi anasema kuwa:

> Alikuwa ni mwanamke wa makamo tu, hazidi miaka ishirini na tano lakini umbile lake la wembamba lilimfanya aonekane yuko chini ya umri huo. Alikuwa na kisauti kikali azungumzapo kila jirani hujua kwamba Mwajuma yupo. Alikuwa na uso mwembamba uliochongoka sawasawa na macho remburembu yaliyowafanya wenzake wampe jina la utani "macho ya urojo" kwa kuwa yalirembuka kiasi ambacho asingeweza kutofautisha wakati amelewa na pale asipolewa (uk.4)

Kutokana na maelezo ya moja kwa moja ya msimulizi kumhusu Mwajuma, tunapata kuelewa kuwa, Mwajuma alikuwa mwanamke wa makamo wala hakuwa mzee, alikuwa mwembamba jambo ambalo lilimfanya aonekane kuwa chini ya miaka ishirini na tano. Vilevile, tunafahamu kwamba, alikuwa na kisauti kikali kilichomfanya kila wakati akizungumza watu wanajua kwamba yupo. Msimulizi anaendelea kueleza kuwa, Mwajuma alikuwa na macho remburembu ambayo mtu asingetofautisha wakati amelewa na wakati hajalewa. Kutokana na hili, tunapata kuelewa sifa nyingine ya Mwajuma ambayo ni ya ulevi. Vivumishi vilivyotumika hapa ni kama vile, kisauti kikali, uso mwembamba na macho remburembu. Vivumishi hivi vinaonyesha kuwa kuna jinsi ambayo msimulizi alitaka kumsawiri Mwajuma kama mwanamke wa makamo mwenye umbile la wembamba na kisauti kikali kutokana na jinsi alivyompenda au kumchukia.

Tunapompata kijana aliyekuwa anamtazama Yasmin akicheza nachi kule Mombasa, tunapata kufahamu sifa zake kutokana na jinsi msimulizi anavyoieleza taswira yake kwani alikuwa kijana barobaro wala sio mzee kama Bwana Raza na alimvutia sana Yasmin. Msimulizi anaeleza kuwa:

> Alikuwa kijana barobaro mwenye umbo la wastani. Alikuwa na macho makali ya rangi ya hudhurungi na nywele ndefu za mseto wa kipilipili na singa. Chini ya pua yake, yalitambaa masharubu machanga yaliyodhihirisha kwamba nd'o kwanza anaingia katika baleghi. Nyusi zake zilizokoza weusi zilianza kutoka katika pembe zote mbili za uso zikaja zikakutana chini ya kipaji (uk.12)

Maelezo ya msimulizi ya moja kwa moja kuhusu kijana aliyemtazama Yasmin alipokuwa anacheza nachi, yanatufahamisha kuwa, alikuwa barobaro, mwenye macho makali na nywele ndefu za mseto wa kipilipili na singa. Pamoja na hayo, tunafahamu kwamba, ndio alikuwa anabaleghe. Kikweli, msimulizi amemsawiri kama kijana mtanashati na wa umri mdogo. Baadhi ya vivumishi vilivyotumika kumuelezea kijana yule ni kama vile, masharubu machanga na nywele ndefu za mseto.

Pale Karimjee Club, wakati muziki ulianza kupigwa na dansa za maonyesho kuanza, kuna mtoto mzuri wa kike aliyetoka katikati ya ukumbi huku watu wakimshangilia kwa kumpigia makofi na wengine kumpigia mbinja. Msimulizi anasema kuwa:

> Alikuwa mtoto mrefu mwembamba (uk.120)

Kutokana na maelezo ya msimulizi, tunaona huu ni usawiri wa moja kwa moja kutokana na vivumishi vya sifa vilivyotumika ambavyo ni mrefu na mwembamba. Msichana huyu amesawiriwa kama mzuri au mwenye sifa za kupendeza na pia anaonekana ni gwiji wa kucheza densi. Mfano mwingine ni wa Shihab.

> Alikuwa kijana mzuri wa kupendeza ambaye mwanamke yeyote angeliona fahari kuwa naye. Alikaa kwa maringo na majivuno akiwasikiliza Cheusi Dawa wakiimba kwa furaha na bashasha (uk.144)

Maelezo ya msimulizi kumhusu Shihab, yanatuwezesha kujua kuwa amesawiriwa kama kijana mtanashati ambaye kila mwanamke angependa kuwa naye na pia tunafahamu sifa nyingine yake kuwa alikuwa mwenye maringo na majivuno kutokana na alivyokuwa kimaumbile. Vilevile kuna matumizi ya vivumishi vya sifa ambavyo ni "kijana mzuri wa kupendeza" na vivumishi hivi vinatudhihirishia kuwa huu ni usawiri wa moja kwa moja. Tunapoona taswira ya Mambo anapomtembelea Denge, tunapata kutambua sifa zake kutokana na maelezo ya msimulizi.

> Yeye alikuwa na sura ya machachari na hasa wanapokuwepo wanawake. Alikuwa akijiamini sana katika matongozaji na kila wakati alikuwa na hakika ya kumpata mwanamke amtakaye. Alikuwa maridadi na kila wakati ananukia marashi. Hupenda kuvaa nguo za rangi moja. Wanawake humwita Bwana Mapozi kwa ile tabia yake ya kuongea huku amejishika nyonga na kuranda huku na huku (uk 102-3)

Dondoo hili limemsawiri Mambo kama mtu aliyependa wanawake kutokana na sura yake ya kupendeza. Vilevile, amesawiriwa kama kijana aliyependa usafi kutokana na kuvaa nguo za rangi moja na kunukia marashi wakati wote. Kutokana na maelezo ya msimulizi, tunapata kubaini sifa za Mambo na kumfahamu zaidi.

Usawiri wa moja kwa moja vilevile unaweza kubainika wahusika wanapokuwa kwenye mazungumzo. Mhusika mmoja anaweza kutoa maoni ya mhusika mwenzake kulingana na

anavyomfahamu. Kwa mfano, Mwajuma anapoeleza kuwa Denge hana chochote, hii haina maana kwamba Denge ni maskini hohehahe kwani hayo ni maoni yake kulingana na anavyomfahamu Denge.

Mwandishi anapotumia mbinu hii, anaweza kuonyesha kuwa anampenda au anamchukia mhusika fulani kutokana na maelezo anayoyatoa. Kutokana na hisia za mwandishi, anaweza kueleza mhusika kwa kifupi kutokana na kutopendezwa naye na kutoa maelezo marefu mazuri ya mhusika anayemvutia na kumfurahisha. Mbali na hayo, usawiri wa moja kwa moja humsaidia msomaji kufahamu sifa za mhusika ambazo hazisahauliki anapoisoma kazi hata akikutana na mhusika huyo kwenye sehemu ya mwisho ya matini husika, humtambua. Vilevile, mbinu hii ina udhaifu ambao ni, msomaji kuwa hana nafasi ya kutathmini tabia alizonazo mhusika mwingine kwani hili huwa ni jukumu la msimulizi.

### 2.1.2 Usawiri usio wa moja Kwa moja

Usawiri huwa sio wa moja kwa moja na badala yake sifa za mhusika huwasilishwa kupitia kwa njia tofauti tofauti. Mbinu ambazo hutumiwa katika usawiri usio wa moja kwa moja ni: mazingira anamopatikana mhusika, mavazi anayovaa, mwonekano wake wa nje, usemi wake, matendo yake, matumizi ya majina ya kimajazi, matumizi ya ishara na analojia.

#### 2.1.2.1 Mazingira

Mhusika anaweza kusawiriwa kwa kuangazia maeneo anamopatikana kama vile chumbani, nyumbani, mtaani au mjini, pamoja na mazingira ya familia au tabaka lake (Rimmon-Kenan, 2002). Kwa mfano: Mazingira anamopatikana Bukheti, yanatusaidia kumfahamu zaidi.

> Bukheti amekaa ukumbini peke yake, nyumba yake imejaa upweke. Ukumbi wenyewe ulikuwa wa nyumba ya mjane na kila kilichokuwepo pale kilikuwa kimekaa ovyo ovyo. Viti viwili vya henzirani, kimoja pembe ya kulia kingine pembe ya kushoto mito yake ya kukalia imevishwa foronya chafu. Meza moja ndogo iko chini ya dirisha, imejaa magazeti. Busati kuukuu limetandikwa chini. Kochi la henzirani lipo katikati na hapo ndipo alipokaa mwenyewe amezama katika mawazo (uk.36)

Chumba anamoishi Bukheti ni chumba kinachosawiri upweke kwani aliishi hapo peke yake. Tunapata kujua kuwa Bukheti ni mchafu kwani viti vyake vilivalishwa foronya chafu na pia meza yake ilikuwa imejaa magazeti kumaanisha kuwa hakuwa na mpangilio mzuri wa vitu vyake kama msimulizi anavyosema kuwa, “mito yake ya kukalia imevishwa foronya chafu”.

Vilevile, mazingira anamoishi Bwana Matar ni mazingira yanayodhihirisha upweke na umaskini. Tunasoma:

> Ukiingia unakabiliana na matalasimu yaliyojaa mabuibui yananing'inia darini. Ndani humo mnanyekenya kwa unyevunyevu wa ile nyumba kwa kukosa joto la binadamu. Harufu ya unyevunyevu ule inapalia kama vumbi kali kwa mtu asiyezoea (uk. 229)

Taswira inayopatikana chumbani mwa Bwana Matar, inatupa picha wazi kuwa, alikuwa mpweke na maskini na hakutumia muda mwingi kukaa chumbani mwake wala kukisafisha. Kuwepo kwa matalasimu chumbani mwake vilevile kunadhihirisha kuwa ni mtu aliyeamini ushirikina na kuona ni vyema kujikinga.

Tunapoangazia mazingira ya utabaka, tunaona kwamba Bwana Raza alikuwa wa tabaka la wafanyabiashara kwani anaonekana kuwa na biashara Mtendeni ambayo aliihamishia Mombasa baadaye. Tunaelezwa:

> Kama desturi ya Wahindi wengi Afrika Mashariki, Bwana Raza alikuwa mfanyabiashara mashuhuri pale Mtendeni. Alikuwa na duka kubwa la biashara ya rejareja (uk.1)

Mfano huu unadhihirisha kuwa Bwana Raza alikuwa mtu wa tabaka la juu kutokana na kumiliki biashara ya rejareja ambayo iliwasitiri watu mbalimbali waliokuwa na haja mbalimbali. Vilevile kama msimulizi anavyosema kuwa kama desturi ya Wahindi wengi Afrika Mashariki, ni wazi kuwa Wahindi walikuwa watu wa tabaka la juu wakilinganishwa na Waafrika wa eneo la Afrika Mashariki. Kwa upande wa mazingira ya kijamaa, tunapata kujua kuwa Bwana Matar hakuwa na familia.

> Yeye mwenyewe hajapata kuoa umri wake wote na ana karibu miaka sitini sasa. Siyo kuoa tu, hata yule mwanamke wa kumweka kinyumba hajapata kuwa naye (uk.230)

Kutokana na maelezo haya, tunagundua kuwa japokuwa Bwana Matar alikuwa mzee wa miaka karibu sitini, hakuwahi kuoa na aliishi maisha ya upweke. Mbali na hayo, tunagundua kuwa, hakuwa hata na mwanamke wa kumweka kinyumba. Mfano huu unatuonyesha jinsi Bwana Matar hakuwa na yeyote maishani mwake bali aliishi akijishughulisha tu kwa mambo yake ya kurandaranda mitaani.

#### 2.1.2.2 Mavazi

Wasifu wa mhusika unaweza kujulikana kupitia kwa mavazi yake. Kwa mfano: mavazi ya mahabusu yanatusaidia kujua wasifu wao.

> Wote walikuwa wamevaa kofia na magwanda meupe yenye mabaka meusi, kila mmoja kifuani ana nambari na tarehe (uk.172)

Wasifu wa mahabusu hawa unatambulikana kutokana na mavazi yao ambayo yanasemekana kuwa ya magwanda meupe yenye mabaka meusi ambayo yanaashiria kuwa wao ni mahabusu na wala sio askari wala watu wa kawaida. Mavazi ya mahabusu hawa yanatusaidia kuwafahamu zaidi. Mavazi ya Inspekta Wright yanatusaidia kubaini wasifu wake kama ifuatavyo:

> Alivaa shati jeupe la mikono mifupi, kaptura nyeupe na soksi nyeupe ndefu zilizomfika mpaka magotini. Viatu vyake vya rangi ya chakleti vilisafishwa vizuri vinameta kama kioo (uk.67)

Kutokana na mavazi ya Inspekta Wright, tunatambua kuwa ni mtu safi au anayependa usafi kwa kuwa anaonekana kuvalia shati jeupe, kaptura nyeupe na soksi nyeupe. Kikawaida, rangi nyeupe huhusishwa na watu wenye usafi wa hali ya juu. Vilevile, viatu vyake vya rangi ya chakleti vilisafishwa vizuri kiasi cha kumeta kama kioo. Kutokana na maelezo haya, tunaweza kusema kuwa, mavazi yake yanamwonyesha kama mtu aliye na cheo cha juu au mwenye mamlaka kama lilivyo jina lake “Inspekta Wright” kwani askari wa kawaida walikuwa wanavalia kanzu kama Koplo Matata.

#### 2.1.2.3 Usemi

Mhusika anaweza kusawiriwa kwa kuzingatia usemi anaoutoa au mawazo yanayompitikia akilini. Anachokisema mhusika kumhusu mhusika mwingine kinaweza kutumika kubainisha sifa zake au sifa za mhusika mwenzake. Muundo au umbo la usemi ni njia ya uhusika kwenye matini pale ambapo lugha ya mhusika huweza kutofautishwa na ya msimulizi. Rimmon-Kenan (2002) anafafanua kuwa, muundo unaweza kuonyesha asili ya mhusika, anamoishi, tabaka lake au kazi anayoifanya.

Kutokana na jinsi mhusika anavyozungumza, wasifu wake unaweza kupatikana au kujulikana. Vilevile, mhusika fulani anaweza kuwa na lafudhi inayomtambulisha. Kwa mfano: lugha anayoitumia Inspekta Wright ni ya Kiingereza kwa wakati mwingi.

> "Good Yasmin" (uk.89)

Inspekta Wright anatumia maneno haya baada ya Yasmin kukubali kwamba atamchunguza Denge na kuwaarifu yote atakayokuwa akiyafanya.

> "Nyinyi najua lipua?"
>
> "Hapana jua. Get out of my office!"
>
> "Operator! Get me the commissioner!" (uk.131)

Inspekta Wright anaonekana kuwa mtu asiyeifahamu lugha ya Kiswahili japokuwa ameishi Afrika Mashariki kwa muda na ndipo anaonekana akitumia Kiingereza wakati mwingi. Wasifu unaojitokeza wa Inspekta Wright ni kuwa, ni mtu mwenye mapuuza kwa kuwa hajali kujifunza Kiswahili na pia ni mjeuri kulingana na jinsi anavyowaongelesha askari wake.

Askari aliyeandamana na mahabusu kwenda Pwani ana sifa ya ujeuri na matusi na pia anaonekana kutojali. Kwa mfano alipokuwa anazungumza na Denge baada ya kumwona amesimama anamwambia:

> "Simama! Simama upesi! Ng'ombe wee!" (uk.237)

Askari anamtukana Denge kwa kumwita ng'ombe jambo ambalo linamfanya kuwa mtu aliyejaa matusi na mtu mjeuri kutokana na kuamrisha kwake anapomwambia Denge asimame. Anamwambia Denge kuwa "Simama! Simama upesi! Ng'ombe wee!". Maneno haya pia yanaashiria kuwa hawaheshimu wafungwa kwani anapowatukana anawavunjia heshima zao.

Vilevile, Denge anapoomba ruhusa kwenda haja ndogo, askari anamjibu kwa ukali huku uso wake ukiwa ameukunja na kipaji kimejaa misirimba.

> "Afendi naomba kwenda haja ndogo."
>
> "Hapana! Kojoa surualini!" (uk.239).

Dondoo hili linamsawiri askari huyu kama mtu asiye na utu na asiyejali maslahi ya wafungwa. Pia anaonekana kuwa mtu asiyejua kutumia maneno yenye heshima. Haya yanadhihirika anapomwambia Denge “Hapana! Kojoa surualini!”. Anapomwambia Denge akojoe surualini, ni wazi kwamba hajali wala hana wakati wa kutumia maneno yenye heshima. Kwa upande wa Denge, anaonekana kama mtu mwenye heshima kwa kutumia neno kama vile “naomba”, anaposema “naomba kwenda haja ndogo”. Vilevile Denge anaonekana kutumia maneno ya heshima anaposema haja ndogo ikilinganishwa na lugha ya askari huyo. Kupitia kwa mazumgumzo ya Koplo Matata na Yasmin, tabia zao zinadhihirika wazi na kutambulika.

> “Hivi sasa yupo wapi?”
>
> “Kasafiri.”
>
> “Kenda wapi?”
>
> “Darsalam.”
>
> “Darsalam?”
>
> “Ndiyo.”
>
> “Kufanya nini?”
>
> “Sijui”
>
> “Kenda kwa ndege au kwa meli?”
>
> “Hakuniambia angeenda kwa kitu gani” (uk.110).

Kutokana na mazungumzo haya, Koplo Matata anadhihirika kuwa ni mdadisi ambaye hachoki kuuliza maswali ili kupata habari zaidi. Maswali hayo ni pamoja na: “Hivi sasa yuko wapi?” , “kenda wapi?” “Darsalam?” , “Kufanya nini?”, “Kenda kwa ndege au kwa meli?”. Yasmin kwa upande wake anadhihirika kama mtu mwongo na msiri. Hili linatokana na kuwa, alijua alikokuwa Denge lakini kutokana na mipango yao ya kutosema ukweli, anaamua kusema kuwa hajui alienda Darsalaam kufanya nini wala hakumwambia angesafiri kwa namna gani.

Yasmin anapozungumza na mjombake Kermali, anatumia lugha yenye msamiati wa heshima. Anatumia maneno kama vile “ma” na “uncle”. Matumizi ya Kiswahili na Kiingereza,

yanamsawiri Yasmin kama msomi au mtu mwenye ujuzi wa lugha nyingi na mwenye uwezo wa kuzitumia kwa pamoja.

> "Wewe uko wapi miaka yote hii?"
>
> "Nipo uncle."
>
> "Naskia uliachana na Raza?"
>
> "Ndiyo uncle."
>
> "Yasmin mbona umebadilika? Umekonda, umepiga weusi, una nini mwanangu?"
>
> "Ni mwili wangu tu ma,"*(* uk.222).

Maneno anayoyatumia Yasmin anapozungumza na mjombake na shangazi yake, yanamsawiri kama mtu mwenye heshima na mapenzi kwao. Maneno hayo ni kama "Nipo uncle, ndiyo uncle na ni mwili wangu tu ma". Kama riwaya isemavyo, yeye humwita hivyo tokea utotoni mwake. Jambo hili ni dhihirisho wazi kuwa Yasmin aliwapenda na kuwaheshimu shangaziye na mjombake tangu utotoni.

Kando na usemi wa mhusika anapokuwa kwenye mazungumzo na wahusika wenzake, sifa zao zinaweza kubainika kupitia kwa mambo yanayowapitikia akilini mwao. Japokuwa mawazo yao hayatamkwi kwa maneno, humpa msomaji uwezo wa kujua sifa za mhusika anayewasilishwa. Tunasoma:

> "Sasa sina mwingine ila mimi na Waafrika n'do baba zangu, n'do mama zangu, n'do Shoga zangu, n'do ndugu zangu. Na wanawadharau kwa sababu gani hasa? Wao sio watu? Au kwa sababu maskini? Ikiwa wao masikini na mimi nishakuwa maskini. Nakula fadhila zao, nakula fadhila za Mwajuma na laiti ingelikuwa si yeye sijui ningeliishi vipi mpaka leo. Ah! Haidhuru na waseme wasemavyo, potelea mbali" (uk.38)

Kutokana na mawazo yanayompitikia Yasmin akilini mwake, tunaweza kutambua sifa zake. Mawazo haya yanatokea baada ya Yasmin kufukuzwa na mamake na kuambiwa kuwa asirudi kwao tena ama ataitiwa askari asemekane kuwa ni mwizi. Sifa inayodhihirika ya Yasmin ni kuwa, ni maskini hana mbele wala nyuma amesalia kutegemea watu wengine kama vile Mwajuma ili aweze kukidhi mahitaji yake kutokana na anavyosema "sina mwingine ila mimi na Waafrika". Vilevile sifa ya Yasmin ya kutojali inadhihirika anaposema kuwa, "Haidhuru na waseme wasemavyo, potelea mbali" inaonyesha kuwa ameamua kuishi

maisha ya kutojali wanachosema watu kumhusu bali anachokijali ni anachokifanya. Zaidi ya hayo, tunagundua kuwa Waafrika wanadharauliwa kwa kuwa ni maskini. Yasmin anaamua kujihusisha na Waafrika ingawa alikuwa Mhindi na haikuwa rahisi Waafrika kutangamana na Wahindi kwani walikuwa ni watu wa matabaka tofauti.

Mawazo yanayompitikia Koplo Matata akilini mwake, yanatusaidia kubaini wasifu wake anaposema:

> "Yule mtoto wa Kihindi, yeye ataweza kunipatia habari zote za mbwa yule" (uk.65)

Mawazo haya yanamjia Koplo Matata alipokuwa amesimama mbele ya chumba chake huku akifikiria atakayomweleza Inspekta Wright kuhusu aliyopata kumhusu Denge kutokana na kibarua alichopewa cha kumchunguza. Mawazo haya yanamsawiri Koplo Matata kama mtu mwenye matusi kwani anamtukana Denge kwa kumwita mbwa. Japokuwa Koplo Matata hakutamka maneno haya, sifa zake bado zinabainika kupitia kwa mawazo yake.

#### 2.1.2.4 Analojia

Analojia ni neno ambalo hutumiwa kuelezea ulinganishi wa vitu ambavyo vinahusiana kwa namna mbalimbali. Analojia huchukuliwa kama kijalizi cha uhusika wala sio mbinu ya kipekee ya kuwasawiri wahusika. Jambo hili linatokana na hali kuwa, uwezo wake wa kuwasawiri wahusika unategemea ufahamu wa kimbele kwa namna nyingine kwa misingi ya sifa ambazo uwezo huo umekitwa (Rimmon-Kenan, 2002).

Kuna njia tatu ambazo analojia hutumia kwenye ufananishaji wake ambazo ni ufananisho wa kimajazi, ufananisho wa kisitiari na ulinganishaji wa wahusika.

##### 2.1.2.4.1 Majazi

Majazi huwa ni mbinu ya kuwapa wahusika majina yanayoakisi wasifu wao. Majina ndiyo hutumika kuelekeza tabia zao (Wamitila, 2003:106-7). Majina yanaweza kuendana na wasifu wa mhusika kwa namna nne kuu ambazo ni: kimwonekano, kiakustika, kimatamshi na kimofolojia. Kuna mifano mbalimbali katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* inayodhihirisha majazi.

Bwana Matar anaitwa "Mashughuli".

> “Watu wanamwita Bwana Mashughuli kwa sababu Matar, kila wakati ni mtu aliyeshughulika. Kazi yake ni kuranda mitaani kutafuta chupa tupu, akazisafishe na kuziuza tena. Huziuza chupa hizo kwa watengenezaji marashi na arki zamda. Nyengine huzipanga dukani kwake Darajani. Si duka la kuitwa dukani. Umwonapo Matar huwa kaeleka fuko kubwa, limejaa chupa tupu. Ukimhitaji kwake lazima umvizie. Huweza kuingia akatoka hapo hapo. Hujui saa ngapi yupo na Saa ngapi hayupo. Na n’do maana wanamwita Bwana Mashughuli.” (uk. 228)

Jina analopewa na watu Bwana Matar ambalo ni Bwana Mashughuli, ni la kimajazi japokuwa la muktadha finyu na linaafikiana kabisa na tabia ya mambo mengi ambapo mara utampata amebeba fuko lililojaa chupa na pia huwezi ukajua wakati alipo nyumbani na wakati asiokuwepo. Maneno haya yanatiliwa mkazo na msimulizi anaposema kuwa “Kila wakati ni mtu aliyeshughulika. Kazi yake ni kuranda mitaani kutafuta chupa tupu, akazisafishe na kuziuza tena. Hujui saa ngapi yupo na saa ngapi hayupo”. Hili linatokana na kuwa ni mtu anayejihusisha na mambo mengi ambayo ukitaka kumpata kwake lazima utazame mienendo yake au uende mapema ili uweze kumpata.

Kwenye mazungumzo ya mfungwa na Denge, tunafahamu kwamba kuna mfungwa anayejulikana kama “Gwiji wa Gereza”.

> “Yule tunamwita Gwiji wa Gereza. Kakulia humu humu, anazeeka humu humu na nafikiri atafia humuhumu” (uk.209)

Jina hili la “Gwiji wa Gereza”, linatokana na kuwa, mfungwa huyo amezoea maisha ya gerezani kwa kuwa ametia fora sana katika wizi wa kuku. Jina hili linatiliwa mkazo kutokana na maneno ya mfungwa ambayo ni “yule tunamwita Gwiji wa Gereza. Kakulia humu humu”. Kinachomfanya kuitwa “Gwiji” ni kuwa, ameishi takribani maisha yake yote humo gerezani na hajali hata akitoka huwa anarudi tena kwa kuwa hutembea na mtama mfukoni akiwawinda kuku na ameyazoea maisha ya gerezani.

Koplo Matata ni askari ambaye bali na kufanya kazi yake anawapitisha watu kwenye matatizo na hali ngumu. Anamsumbua Yasmin kwa kumfanya alie kiasi cha macho yake kugeuka rangi yakawa mekundu na pia kumpigisha magoti alipokuwa anauliza habari za Denge. Japokuwa Yasmin anamsihi Koplo Matata asimrudishe kwa mumewe Bwana Raza, haonekani kuwa na chembe ya huruma kwani alichokitaka ni kupata habari za Denge (uk.90).

Mambo ni mfano mwingine wa jina la kimajazi kutokana na tabia zake kwani anasemekana na wahusika wenzake kuwa ana mambo kwelikweli. Pia ana jina la kimajazi ambalo huitwa na wanawake ambalo ni "Bwana Mapozi". Jina hili linatokana na tabia yake ya kuongea akiwa amejishika nyonga na kuranda huku na huko (uk 103).

Umuhimu wa mbinu hii ni kuwa, humsaidia msomaji kufahamu kwa urahisi tabia na wasifu wa mhusika na pia mwandishi huitumia kuuchimuza mtazamo na mwono wake kuwahusu wahusika fulani na hata mwelekeo wa hadithi nzima. Mbinu hii hata hivyo, ina udhaifu ambao ni kuwa, huwa msomaji hana nafasi ya kutoa uamuzi kuhusu wasifu wa mhusika bali huridhika tu na maoni yanayotolewa na mwandishi au msimulizi.

#### 2.1.2.5 Matendo

Tabia ya mhusika inaweza kutambulika kutokana na tendo analolifanya mara moja au kutokana na tendo analolifanya mara kwa mara. Tendo la mara moja huweza kuamsha kipengele cha nguvu cha mhusika na kuleta badiliko katika simulizi kwani huonyesha kuwa, sifa ambazo zinaibuliwa ni muhimu zaidi kuliko zilizozoeleka. Kwa upande wa tendo la mazoea, huweza kuibua vipengele vya mhusika visivyobadilika kama vile mhusika kufanya matendo ya zamani yaliyomfanya kuhisi hajakamilika. Japokuwa tendo la mara moja halionyeshi sifa bainifu, haimaanishi kuwa, sio sifa ya mhusika. Matendo anayoyafanya mhusika, yawe ni ya mara moja au ya mara kwa mara, yanaweza kuwekwa katika kategoria mbalimbali ambazo ni:

##### 2.1.2.5.1 Tendo la utekelezaji

Tendo hili hufanywa na mhusika. Matendo anayoyafanya mhusika ndiyo yanayotusaidia kung'amua sifa za mhusika huyo. Kwa hivyo, ni lazima mhusika afanye jambo ndiposa msomaji aweze kutambua tabia yake. Linaweza kuwa ni tendo ambalo mhusika amelifanya mara moja au liwe tendo ambalo amezoea kulitenda.

Kwa mfano, tendo la Yasmin la kusikiliza waimbaji wakighani na kutetea, ni tendo la utekelezaji kwa kuwa Yasmin alianza kucheza kila wakati ikawa ndio mtindo wake huku akinyanyua mikono yake na kuishusha, akijibeua na kujinyonganyonga mithili ya mkunga aogeleavyo kupitia mapangoni. Alikuwa anajifananisha na mchezaji Nachi stadi wa filamu za Kihindi. Wakati huo wote Yasmin aliamua kuwa, ndiposa afukuze upweke atakuwa anacheza. Jambo ambalo hakulijua ni kuwa alikuwa na kijana jirani aliyekuwa akimtazama

wakati wote akicheza kupitia dirishani. Tendo hili la Yasmin la kucheza na kusikiliza muziki kila wakati, linatujuza tabia yake kuwa ni mtu aliyependa kucheza na kusikiliza muziki (uk 11).

Mfano mwingine ni wakati ambapo Bwana Raza anarudi na kumuuliza Yasmin mbona siku hizi hamchezei Nachi. Mazungumzo yao yanatupelekea kuelewa sifa ya Bwana Raza.

> "Wewe nimekuchukua kwenu hohehahe! Huna mbele wala nyuma
>
> unanuka umaskini leo umekuwaje jeuri enh?" (uk.14).

Kabla Yasmin hajajaribu kujibu, Bwana Raza anamzaba kofi kubwa lililomsababishia vimulimuli kila rangi vikawa vinameremeta mbele ya macho yake. Kabla hajamaliza kuzungumza tena, akapigwa kofi la pili akaanguka juu ya kochi kama mzigo anatweta kama mgonjwa wa pumu. Tendo hili la kumpiga Yasmin, linatusaidia kujua kuwa Bwana Raza ni mtu katili na aliyejawa na hasira na matusi kwani kabla ya kumpiga alimtukana kuwa "Unanuka umaskini". Tabia ya Bwana Raza inajitokeza kutokana na tendo lake. Riwaya ya *Vuta N'kuvute* ina mfano mwingine wa tendo la utekelezaji. Tabia ya Koplo Matata ya kumuuliza Yasmin aliko Denge, inatusaidia kutambua tabia yake.

> "Nakuuliza umeolewa?"
>
> "Nimeachwa"
>
> "Lini?"
>
> "Siwezi kumbuka"
>
> "Hukuachwa, umemkimbia mumeo." (uk.86).

Mfano mwingine ni kama ufuatao:

> "Denge unamjua?"
>
> "Nakuuliza Denge unamjua?"
>
> "Namjua"
>
> "Unamjua vipi?"
>
> "Namjua kwa kumuona akija kwa Mwajuma"
>
> "Yeye na Mwajuma wana uhusiano gani?"

"Niliwahi kumsikia Mwajuma akisema kwao kumoja"

"Wapi?" (uk.87).

Kutokana na mazungumzo ya Koplo Matata na Yasmin, tunatambua kuwa Koplo Matata ni mdadisi kwa kuwa anataka kujua habari zaidi zinazomhusu Denge. Vilevile tunabaini kuwa ni mkali kwa kuwa hampi Yasmin wakati wa kufikiri bali anataka akiuliza swali tu ajibu bila ya kuliwazia. Hili linatokana na maswali anayomuuliza kama "Denge unamjua? Nakuuliza Denge unamjua? Unamjua vipi? Yeye na Mwajuma wana uhusiano gani?". Maswali haya yanamsawiri kama mtu asiye na subira kwani anamharakisha Yasmin kujibu maswali hayo bila hata kutathmini majibu anayopewa.

Maelezo ya msimulizi kumhusu Mwajuma, yanatufanya kufahamu kuwa alikuwa anaenda kwenye densi kila Jumamosi

> Kila jumamosi alikuwa hakosi densini na alikuwa mpenzi mkubwa wa taarabu. Katika bahari ya muziki wa aina hiyo, alikuwa na sifa kubwa katika chama chake cha "Cheusi Dawa" kwa ajili ya sauti yake nyororo kali wakati anapoimba asionyeshwe bi.harusi pahala popote pale, utamkuta Mwajuma amekwisha fika amejitia kizoro pamoja na wasichana wenzake (uk.20).

Kutokana na tendo la Mwajuma la kwenda densi kila jumamosi na sauti yake kali anapoimba, tunaweza kubaini tabia yake. Sifa zake zinazobainika ni kuwa, aliupenda muziki na kucheza na pia alipenda sherehe za harusi kwani alijua huko atafurahia. Vilevile, tunapata kujua kuwa alikuwa mpenzi mkubwa wa taarabu kiasi cha kuwa alikuwa na chama chake kilichoitwa "Cheusi Dawa."

### 2.1.2.5.2 Tendo la kunuia

Hili ni tendo la mhusika ambalo halijagunduliwa au tendo ambalo halijafanyika ilhali mhusika anatarajia kulitekeleza. Kwa mfano, tendo la Mambo na kundi lake la kumtorosha Denge gerezani ni tendo la kunuia kwa kuwa wanataka kulifanya lakini bado halijagunduliwa.

"Denge lazima tumtoroshe, tena siku hizi hizi, tusichelewe."

"Wewe mambo akili zako timamu au umeanza kuvuta bangi siku hizi?"

"Lini umeskia mtu katoroshwa jela hata Denge awe wa pili?"

"Wewe unajuaje Mwajuma, watu kila siku wanatoroka jela. Tuulize sisi

tunayoyajua." (uk. 212).

Mazungumzo ya Mambo na Mwajuma yanatusaidia kuelewa kwamba, walitaka kumtorosha Denge gerezani lakini bado hawajamtorosha. Hili linadhihirishwa na maneno ya Mambo anaposema kuwa "Denge lazima tumtoroshe, tena siku hizi hizi tusichelewe". Jambo hili linatusaidia kujua kuwa, Mambo alimthamini rafikiye Denge wala hakutaka aendelee kuteseka gerezani na yuko tayari kwa usaidizi wa kundi lake kumtorosha. Pia tunabaini kuwa sio mara ya kwanza kwa Mambo kumtorosha mtu kutoka gerezani kama anavyomwambia Mwajuma kuwa awaulize wao wanaojua. Tabia ya Mwajuma ya kutojua na woga inadhihirika kwani anaonekana kutotambua kuwa watu hutoroshwa gerezani na pia anaogopa jambo hilo litatendekaje anapomuuliza Mambo kuwa, ni lini akasikia mtu katoroshwa jela hata Denge awe wa pili.

### 2.1.2.5.3 Tendo la kukwepa

Huwa ni tendo linalostahili kufanywa na mhusika lakini anakosa kulifanya (Rimmon-Kenan, 2002). Katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*, Yasmin alitarajiwa kurudi kwa mumewe Shihab baada ya kumruhusu kwenda Unguja kuwaona wazee wake lakini anapokutana na Denge anaamua kutorudi. Jambo hili linamfanya Shihab kumsubiria Yasmin kwenye uwanja wa ndege jambo linalosababisha kifo chake kutokana na mshtuko alioupata baada ya kuona ajali ya ndege iliyotokea akifikiri kuwa amempoteza Yasmin kwenye ajali hiyo. Shihab anapoteza fahamu na kukata roho pindi tu alipofikishwa nyumbani (uk.192).

Hata hivyo,si rahisi kuwepo kwa matendo mengi ya kukwepa kwa kuwa tunatarajia kuona wahusika wakitenda wanayostahili kuyatenda.

### 2.1.2.6 Mwonekano wa nje

Mwonekano wa nje wa mhusika unaweza kutumiwa kubaini sifa zake. Kuna uhusiano wa moja kwa moja wa jinsi mhusika anavyoonekana kwenye uso na tabia zake za kipekee. Msomaji anafaa atofautishe sifa ambazo zinaonekana za mhusika ambazo hana uwezo wa kuzidhibiti kama vile kimo, rangi ya macho, urefu wa pua au sifa ambazo zinatokana na mambo ya kiteknolojia na zile ambazo zinategemea uwezo wa mhusika kama vile mtindo wa nywele na mavazi.

Kwa mfano katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*, kuna mifano ya sifa za wahusika zinazopatikana kutokana na mwonekano wao.

> Alikuwa ni mwanamke wa makamo tu, hazidi miaka ishirini na tano lakini umbile lake la wembamba lilimfanya aonekane yuko chini ya umri huo. Alikuwa na kisauti kikali azungumzapo kila jirani hujua kuwa Mwajuma yupo. Alikuwa na uso mwembamba uliochongoka sawasawa na macho remburembu yaliyowafanya wenzake wampe jina la utani "macho ya urojo" kwa kuwa yalirembuka kiasi ambacho asingeweza kutofautisha wakati amelewa na pale asipolewa. Alikuwa mrefu wa wastani na avaapo lile vazi lake alipendalo la kujifunga kiunoni na nyingine kujitupia mabegani, huku nywele zake amezisuka vizuri nne kichwa, huwezi kupita ukamtazama mara moja (uk. 4)

Kutokana na maelezo tunayopata ya Mwajuma, tunaweza kubaini kuwa alikuwa mwembamba, alikuwa na sauti kali ambayo ilimfanya kila wakati akizungumza majirani kujua kuwa yupo. Vilevile tunapata kujua kuwa Mwajuma alikuwa na macho ya remburembu kiasi cha kupewa jina la utani. Mbali na hayo, alikuwa mrefu wa wastani na kuna vazi alilolipenda sana na mtindo fulani wa kusuka nywele. Kutokana na maelezo haya, tunaona kwamba sifa zote zinapatikana kwa Mwajuma kutokana na kuwa kuna sifa ambazo anaweza kuzidhibiti kama vile mtindo wake wa nywele na mavazi aliyoyapenda sana na zile ambazo hawezi kudhibiti kama vile kimo chake na rangi yake ya macho.

Mfano mwingine ni wa Denge:

> Mrefu asiyepita futi sita. Mwembamba lakini ule wembamba uliojaa ukakamavu. Umbile hilo na ile rangi yake ya maji ya kunde lilimfanya aonekane kama mroni wa kimasai. Macho yake madogo lakini makali akutazamapo utafikiri anataka kukuumbua. Pua yake ilikuwa ya wastani na chini yake yamechipua masharubu machanga yaliyotambaa kwa utulivu toka ncha moja ya mdomo mpaka ncha nyingine. Na ndevu nazo zilikuwa ndiyo kwanza zinachipua moja hapa moja pale, na hayo yalidhihirisha waziwazi umri wake mdogo, labda ndo kwanza anapindukia miaka ya ishirini (uk.42).

Kutokana na maelezo ya Denge, wasifu wake umeweza kujitokeza. Tunapata kujua kwamba alikuwa mrefu, mwembamba na mkakamavu. Alikuwa na macho makali ambayo yalikuwa madogo lakini ya kuogofya. Tunatambua kuwa alikuwa na umri mdogo kama miaka ishirini hivi. Wasifu unaojitokeza wa Denge ni kuwa alikuwa mkali. Pia tunaona kwamba ana sifa

ambazo hawezi kudhibiti kama vile rangi yake ya maji ya kunde, kimo chake cha futi sita, pua lake la wastani na ndevu zake ambazo zilikuwa zinachipuka moja hapa na nyingine pale.

Mfano mwingine ni wa Bashiri

> Lilikuwa tumbo kubwa lililolingana sawasawa na unene wake. Ufupi wake Ulilifanya lile tumbo lionekane kubwa zaidi, na pale alikuwa amevaa shati jeupe, bwangabwanga. Saruni nzuri ya hariri ameikaza kwa ukanda kiunoni. Uso wake mdogo unachururika majasho kwa joto la pale ukumbini, amechukua upepeo anajipepea (uk. 72).

Bashiri anaonekana kuwa mtu mnene na mfupi na mwenye tumbo kubwa. Hariri aliyoivaa inamsawiri kama tajiri kwa kuwa inasemekana kuwa ya bei ghali na haipatikani katika maduka yote. Tunaona kwamba kuna sifa ambazo Bashiri hawezi kuzidhibiti kama vile ufupi alionao na uso wake mdogo. Vilevile, kuna sifa zingine anazoweza kudhibiti kama vile mavazi yake na tumbo lake kubwa.

Mfano mwingine ni wa Kibwe anayeelezwa ifuatavyo:

> Alikuwa mfupi mnene mwenye mikono ilioyojaa misuli. Kifua chake kikubwa kilivimba misuli na hujifurahisha kwa kifua hicho kwa kutofunga kifungo cha shati ili kukiweka kifua hicho bayana kuthibitisha ubabe wake (uk.45)

Maelezo ya Kibwe yanatusaidia kujua kuwa, alikuwa mfupi, mnene na mwenye misuli iliyomjaa mikononi. Tunaelewa sifa za Kibwe kama mtu mwenye majivuno kwani anasemekana kuwa huwa hafungi kifungo cha shati ndipo aweke kifua chake bayana ili aweze kuthibitisha ubabe wake. Vilevile, tunabaini kuwa kuna mambo ambayo hawezi kuyadhibiti kama vile kimo chake kwani hawezi kujirefusha lakini anaweza kudhibiti misuli yake kwani hiyo imetokana na bidii yake.

#### 2.1.2.7 Hitimisho

Katika sehemu ya kwanza ambayo ni ya uhusika na wahusika kwa kuchunguza namna wanavyosawiriwa, utafiti wetu umebaini kuwa, mbinu za usawiri wa moja kwa moja na usio wa moja kwa moja zimetumika. Katika riwaya teule ya *Vuta N'kuvute,* mbinu za usawiri usio wa moja kwa moja kama vile mazingira, mavazi, mwonekano wa nje, usemi, matendo na analojia zimetumika kwa kiasi kikubwa katika usawiri wa wahusika. Hata hivyo, katika mbinu ya analojia, matumizi ya majina ya kimajazi ndiyo imesheheni kwani ulinganuzi wa

wahusika haujathibitishwa. Sehemu hii imetuwezesha kuwafahamu wahusika zaidi kutokana na sifa na jinsi msanii alivyotaka waonekane kwani kazi ya kisanaa haiwezi kufanikishwa bila uwepo wa wahusika na hasa katika riwaya. Mwandishi amewafinyaga wahusika wake kwa njia ambazo zimemsaidia kupitisha ujumbe wake kwa wasomaji.

## 2.2 UWASILISHAJI WA USEMI NA MAWAZO YA WAHUSIKA

### 2.3 Utangulizi

Sehemu hii imechunguza lugha au usemi wa wahusika kwenye maingiliano yao na mawazo yanayowapitikia akilini. Usemi ambao hupatikana kwenye kazi ya fasihi huweza kuelezwa kwa njia mbalimbali ambapo ile kuu ni ya maelezo ya msimulizi. Njia nyingine ni pale ambapo lugha ya wahusika huwasilishwa kwa njia ya wazi wahusika wanapojibizana kwenye mazungumzo. Mbinu ambazo hutumika kuwasilisha usemi wa wahusika ni sawia na zitumikazo kuwasilisha mawazo yao. Lengo kuu katika sehemu hii lilikuwa ni kubaini kama msimulizi ataweza kufanikisha kazi yake kupitia kwa usemi na mawazo ya wahusika wake.

### 2.4 Uwasilishaji wa Usemi wa Wahusika

Uwasilishaji wa usemi huhusisha mbinu kama vile: usemi halisi, usemi halisi huru, usemi wa taarifa na usemi wa taarifa huru. Uwasilishaji wa usemi huhusisha kuwasilisha semi za wahusika ambazo ni za moja kwa moja wanapozungumza na wahusika wenzao katika kazi za fasihi. Usemi halisi huwasilisha moja kwa moja jinsi wahusika walivyosema, usemi wa taarifa huhusisha ripoti ya kilichosemwa na mtu mwingine kwa kutotilia maanani muundo asili wa kilichosemwa, usemi halisi huru huhusisha uzungumzinafsi wa wahusika mbalimbali na usemi wa taarifa huru.

#### 2.4.1 Usemi Halisi

Prince (1987) anafafanua usemi halisi kama aina ya diskosi ambayo matamshi au fikira za mhusika hutolewa au kunukuliwa jinsi alivyoziwasilisha. Usemi halisi wakati mwingine huambatanishwa na alama kama vile za kunukuu au za mtajo, kistari na nyinginezo. Kuna mifano mbalimbali ya usemi halisi katika riwaya ya *Vuta N’kuvute* kama ifuatavyo:

Yasmin anapoenda kumuaga rafikiye Mwajuma baada ya kutoka kwa mamake Zenabhai, anamwambia Mwajuma:

> “Ah! Nna haraka, siwezi kupita ndani manake sikumwambia mume wangu kama nitapitia kwako. Yeye anajua kwamba nimekwenda Kiponda kwa mama tu. Basi nikichelewa yatakuwa mengine kwani kama unavyoyajua, baba lenyewe lina wivu kama nini sijui” (uk.7).

Yasmin anazungumza na Mwajuma akimwambia kuwa ana haraka kwani mumewe hakujua kwamba angekuja kwake. Kuna matumizi ya alama za mtajo ambazo zinaonyesha kuwa maneno yaliyonukuliwa yametoka moja kwa moja kwa mzungumzaji ambaye ni Yasmin. Vilevile, kuna matumizi ya nafsi ya kwanza kama vile “nna” na “mimi” kuonyesha ukaribu uliopo kati ya wanaozungumza.

Matumizi mengine ya usemi halisi yanapatikana pale ambapo Denge na Mambo wanazungumza.

> “Unajua De, sasa iko haja ya kubadili mbinu, lakini kuna jambo moja zuri. Sasa inaonyesha wasiwasi wao ni wewe tu bado hawajawajua jamaa wengine. Sasa iko haja ya kuwatahadharisha jamaa wengine wasiweke vitu vya maana ovyo majumbani mwao” (uk.115)

Mazungumzo haya yanatokea baada ya Denge kumweleza Mambo kuwa askari walimvamia huku wakitaka pasipoti yake. Baadaye Mambo anainamia chini na kufikiria na kumwambia Denge kuwa, itawapasa wabadili mbinu na kumjuza kuwa, wanaowatafuta bado hawajui kwamba kuna vijana wengine wa kundi lao. Alama za mtajo zimetumika kuonyesha kuwa maneno yaliyotamkwa ni ya Mambo. Alama hizi zinaonyesha kuwa maneno haya yalinukuliwa moja kwa moja kutoka kwa mnenaji na wala sio mtu anayeripoti yaliyosemwa.

Usemi halisi pia umedhihirika ifuatavyo:

> “Mimi nakwenda sinema. Kuna mchezo mzuri wa Kihindi. Huyu bibi kashika anataka kuja kwako, tena namwona siku hizi hachoki kuja kwako na kila tukikaa Denge hivi, Denge vile, umemfanya nini hasa, au ushamkorogea miti shamba?” (uk.127).

Haya ni mazungumzo baina ya Mwajuma na Denge. Hapa ni baada ya Denge kuwatembelea Mwajuma na Yasmin na kumpata Yasmin akimsuka Mwajuma. Kutokana na mfano huu, alama za mtajo zimetumika kunukuu maneno ya Mwajuma. Hili linaonyesha kuwa ni maneno yaliyotoka moja kwa moja kinywani kwa Mwajuma. Pamoja na hayo, kuna matumizi ya nafsi ya kwanza inayowakilishwa na neno “mimi” inayoonyesha kuwa, msimulizi ana ukaribu na wanaozungumza.

Katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*, kuna mfano mwingine wa usemi halisi

> "Mimi nataka Denge anapokuja hapa umsikilize maneno yake vizuri, umsikilize nini anasema, nani rafiki zake anaofuatana nao, nini anataka na kila analolisema umsikilize kwa makini halafu yote atakayoyasema uje uniambie nitakapokuja tena" (uk.58)

Maneno haya ni ya askari kanzu aliyeenda nyumbani kwa Mwajuma akimtafuta Denge. Haya yanatukia baada ya askari huyo kumweleza kuwa Denge ni mkomunisti, alisoma Urusi na ni mtu hatari sana kwa kuwa ni watu wasiomwamini Mungu na wanataka kuleta fujo nchini. Huu ni usemi halisi kutokana na matumizi ya alama za mtajo kuonyesha kuwa maneno hayo ni ya askari kanzu na wala sio ya mtu mwingine. Vilevile, kuna matumizi ya kiwakilishi nafsi "mimi" kinachobaini kuwa anayezungumza ni maneno yake halisi na wala sio ya kuripotiwa.

### 2.4.2 Usemi Taarifa

Hii huwa ni ripoti ya kilichosemwa na mtu mwingine kwa kutotilia maanani mbinu au muundo asili wa kilichosemwa. Matamshi au fikira za mhusika hubadilishwa kupitia kwa mabadiliko ya nyakati na pia kubadilika kutoka kwa viambishi vya nafsi ya kwanza hadi ya tatu ambayo inaweza kuwa katika umoja au wingi. Katika usemi taarifa, alama za kunukuu huwa hazipo. Kwa mfano:

> Yasmin alitoka huku nyuma mama yake akiendelea na matusi. Aliondoka pale mnyonge akiona ule n'do mwisho wa maisha yake Uhindini. Aliona dunia imempa mgongo na maisha yake yote yametawaliwa na unyonge na bahati mbaya (uk.38)

Msimulizi anatujuza yaliyomfika Yasmin kwa kutupa ripoti ya matukio yaliyojiri. Yasmin anakutana na mamake anapoenda Zanzibar baada ya kuachana na Bwana Raza. Kiambishi "li" kinachoashiria wakati uliopita, kimetumika kuonyesha kuwa hakuna ukaribu wa kimasafa kati ya msimulizi na wahusika waliomo kwenye hadithi. Vilevile, kiambishi cha nafsi ya tatu "a" kimetumika kuonyesha kuwa ni ripoti ya mtu mwingine wala sio usemi wa moja kwa moja halisi wa mhusika.

Usemi taarifa pia huwa hauna matumizi ya alama za uakifishaji kama vile vihusishi na viulizi. Kwa mfano:

> Koplo Matata alimtazama kwa uso wa kikatili uliokosa huruma hata kidogo. Na yale macho yake ya masharubu yakathibitisha waziwazi utovu wake wa huruma uliojificha ndani ya ile sauti yake anapojidai upole. Uso ameukunja akaujaza matuta kipajini. Alikisogeza nyuma kiti alichokuwa amekalia na kuegemea kwa dharau akionyesha kwamba hajali wala habali yote aliyoyasema Yasmin (uk.87)

Haya ni matukio yanayotokana na kukamatwa Yasmin na Koplo Matata. Hata baada ya kumpigia magoti Koplo Matata anaonekana kutokuwa na huruma naye. Msimulizi anatueleza ripoti ya yaliyotokea ambapo Koplo Matata anaonekana kukosa huruma kwa Yasmin. Katika dondoo hili, hakuna matumizi ya viulizi wala vihusishi au alama za mshangao. Kuna matumizi ya kiambishi "li' kinachoonyesha kuwa ni jambo lililotendeka na pia hakuna ukaribu wa kimasafa kati ya msimulizi na wahusika wanaozungumziwa. Vilevile, kuna matumizi ya "a" inayoashiria nafsi ya tatu umoja kuonyesha kuwa sio mazungumzo ya moja kwa moja bali ni ripoti ya kilichotukia.

### 2.4.3 Usemi Taarifa Huru

Usemi taarifa huru upo baina ya usemi halisi na usemi taarifa. Sifa za kiisimu za usemi taarifa huru huweka pamoja usemi halisi na usemi wa taarifa. Kama asemavyo Rimmon-Kenan (2002), usemi taarifa huru huwa na sifa za mabadiliko ya viwakilishi ambavyo katika usemi halisi vipo katika nafsi ya kwanza na ya pili na ambavyo hubadilika na kuwa vya nafsi ya tatu katika usemi taarifa na usemi taarifa huru, huondoa vitenzi pamoja na viunganishi, haubadilishi viashiria vya mahali vya ukaribu, hudondosha vishazi ambavyo huonyesha aliyesema maneno fulani na huwa na matumizi ya vionyeshi na maswali. Kwa mfano:

> Ilikuwa karibu saa tano asubuhi na Koplo Matata anapita na baiskeli yake taratibu chini ya vivuli vya miti ya mnazi mmoja akiburudika kwa hewa inayopepea. Aliwaza aende wapi wakati ule, lakini alipigwa na mshangao mkubwa alipofika senema ya "Majestic" na kumkuta Yasmin peke yake, anatazama matangazo ya senema (uk. 69)

Koplo Matata anakabiliwa na kibarua cha kumtafuta Yasmin ili kupata habari kumhusu Denge. Hili linatokana na amri ya Inspekta Wright alipomwambia kuwa amtafute Yasmin hata ikibidi atumie pesa ndiposa ampe habari zake. Sifa za usemi taarifa huru zinadhihirika kutokana na mabadiliko ya njeo kutoka wakati uliopo hadi wakati uliopita kama vile kutoka kwa "Koplo Matata anapita" hadi "aliwaza aende wapi". Hapa, njeo zimebadilika kutoka kwa matumizi ya kiambishi "na" hadi "li" ambacho huashiria wakati uliopita. Vilevile, kuna

matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya tatu vinavyowakilishwa na matumizi ya kiambishi "a" kama inavyodhihirika kwenye maneno "akiburudika", "aliwaza", "alipigwa" na "alipofika". Matumizi ya kiambishi "a" yanaonyesha kuwa kuna mabadiliko kutoka nafsi ya kwanza na ya pili hadi nafsi ya tatu.

Wamitila (2008) katika *Kanzi ya Fasihi* (1) akimnukuu (Gavins, Textworld, 128), anasema kuwa, usemi taarifa huru hutumika kama njia mojawapo ya kuingiza sifa ya huruma kuhusiana na usimulizi na hasa kutokana na mwelekeo wake wa kumwingiza mtu kwenye hisia na usemi wa mhusika bila ya kuingiliwa au kuelekezwa na kwa njia hii kumvuta msomaji kwenye ulimwengu wa matini.

### 2.4.4 Muhtasari wa Daigesia

Muhtasari wa daigesia ni ripoti inayoonyesha kwamba tendo la usemi limetokea bila kuonyesha kilichosemwa au jinsi kilivyosemwa. Kwa mfano, Denge alipokuwa kwenye mashua na wenzake, kuna tendo la usemi lililofanyika lakini halionyeshwi wala kusemwa lilitendekaje. Msimulizi anasema kuwa:

> Mlio wa mashine ile ulichanganyika na sauti za mazungumzo mazuri ya vijana wale. Yalikuwa mazungumzo ya kufurahisha na kuchekesha (uk.99)

Kutokana na mfano huu, ni wazi kwamba, kuna tendo la usemi lililotokea kutokana na msimulizi anaposema mlio wa mashine ulichanganyika na sauti za mazungumzo mazuri ya vijana wale. Hata hivyo, hatufahamu kilichosemwa wala walikisema vipi.

### 2.4.5 Muhtasari wa Daigesia usio kamili

Rimmon-Kenan (2002), anafafanua muhtasari wa daigesia usio kamili kama muhtasari ambao kwa kiwango fulani huwakilisha, sio tu kutaja tukio la usemi bali hutaja mada za mazungumzo. Hapa, mada za mazungumzo ndizo hutiliwa maanani zaidi bali si mazungumzo kwa undani. Riwaya ya *Vuta N'kuvute* ina mifano mbalimbali ya muhtasari wa daigesia usio kamili kama ifuatavyo:

> Denge, Mambo, Huseni, Chande na Sukutua walisimama nyuma ya ukuta uliozunguka jengo la klabu hiyo wakishauriana juu ya mbinu za kuwawezesha kuingia ndani (uk.119)

Mada ya mazungumzo ya Denge, Mambo, Huseni, Chande na Sukutua inawasilishwa na msimulizi baada ya marafiki hawa kufika Karimjee Club. Baada ya kufika na kuona mandhari yalivyokuwa kama watu waliovaa nguo za fahari, kuwepo kwa magari ya kila mitindo na kuwepo na walinzi maalum waliosimama nyuma ya ukuta ndipo wakaanza kushauriana. Jambo lililoko wazi hapa ni kuwa, msimulizi hajatueleza kwa undani walichokizungumzia bali tunapata muhtasari tu wa mada waliyoizungumzia ambayo ni kushauriana juu ya mbinu za kuwawezesha kuingia ndani. Mfano mwingine wa muhtasari wa daigesia usio kamili ni pale gerezani baada ya wafungwa kurudi kutoka kazini. Msimulizi anaeleza kuwa:

> Hapo zikaanza hadithi, wengine wakieleza jinsi walivyokuwa mabingwa kwa kuiba, wengine wakijisifu kwa muda mrefu waliokaa gerezani. Zikawa hadithi za uhalifu tu (uk.173)

Kutokana na dondoo hii, tunafahamu kabla ya mada hii kuanza zilikuwa nyakati za usiku baada ya wafungwa kutoka kazini na kuja kumdadisi Denge. Baadaye wafungwa wanaanza kupakua bidhaa walizokuwa wameingia nazo zikiwemo sigareti ambazo kwao zilikuwa bidhaa muhimu kuliko dhahabu au fedha kwani aliyekuwa nazo alikuwa tajiri. Baada ya wafungwa kujipanga ndipo wanaanza kuvuta sigara na wakaanza hadithi mbalimbali. Msimulizi anatuelezea kuwa walielezana jinsi walivyokuwa mabingwa wa kuiba, wengine wakijisifu kwa muda mrefu waliokaa gerezani. Tunachofahamu hapa ni mada ya kile walichokizungumzia bali hatujaelezwa kwa undani mazungumzo yao.

Muhtasari wa daigesia usio kamili una umuhimu ambao ni kupunguza wakati matini kwani mazungumzo yamefupishwa na vilevile una udhaifu wake ambao ni kuwa, haumpi msomaji ruhusa ya kujua mazungumzo ya wahusika na humuacha akiwa na hamu na maswali ya kutaka kujua walichokizungumzia kwa undani.

## 2.5 UWASILISHAJI WA MAWAZO YA WAHUSIKA

Sehemu hii itashughulikia uwasilishaji wa mawazo ya wahusika ambao hutokana na mambo yanayotokea akilini mwao wala si mazungumzo ya moja kwa moja na wahusika wenzao. Mwandishi anapowasilisha mawazo ya wahusika, huwa ni rahisi kwa msomaji kuelewa tabia, matamanio na hisia za mhusika. Katika uwasilishaji wa mawazo, alama za mtajo huwa hazitumiki kwa wingi japokuwa kwenye kipengele cha mawazo huru. Uwasilishaji wa

mawazo ya wahusika unafuata mkondo sawa na ule wa uwasilishaji usemi. Mbinu zitakazoshughulikiwa ni pamoja na mawazo halisi, mawazo halisi huru, mawazo taarifa na mawazo taarifa huru.

### 2.5.1 Mawazo Halisi

Mawazo halisi huwa ni mawazo yaliyoko akilini mwa mhusika ambayo hupatikana kwenye simulizi. Mawazo halisi hubainika kwa njia ya uzungumzinafsi, jambo ambalo humfanya msomaji kubaini yanayojiri akilini mwa mhusika. Kwa mfano:

> "Ah, haidhuru nitaishi hivyohivyo. Yache maji yafuate mkondo na upepo uvume utakapo kwani wangapi duniani wenye dhiki. Mwisho wa dhiki si dhiki ni faraja tu." (uk.38)

Haya ni mawazo yanayojiri akilini mwa Yasmin baada ya kufika kwa mamake Kiponda. Anapofika, anakutana na mamake ambaye anamtukana kwa kumwita mwanaharamu na kumwambia aondoke kwa kuwa hataki kumwona na akirudi tena atamwitia askari. Yasmin anaamua kuondoka huku mamake akimfuatilizia matusi na kwa unyonge mwingi akiona kuwa ule ndio mwisho wa maisha yake Uhindini. Yasmin anaona kuwa dunia imempa mgongo na kutawaliwa na bahati mbaya. Haya yanatokana na kuozwa kwa mume mzee na asiyemtaka, kufukuzwa na mjomba wake anaporudi kwao na kinachomvunja moyo zaidi, ni kule kufukuzwa na mamake jambo linalompelekea kuwa na mawazo haya.

Mawazo halisi yanadhihirika kutokana na matumizi ya alama za mtajo na matumizi ya viwakilishi vya wakati uliopo. Yasmin anaonekana akijizungumzia. Msimulizi anatueleza yanayotokea akilini mwa Yasmin ili tupate kumjua zaidi na kufahamu jambo linalomsumbua ambapo tunapata kujua kuwa Yasmin amekata shauri na kusema liwe liwalo.

Katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* kuna mfano mwingine wa mawazo halisi tunapopata kujua kinachompitikia Koplo Matata akilini mwake.

> "Lakini ah, Unguja ndogo. Siku mbili tu nitapata habari zake zote" (uk.69)

Mawazo haya yanatokea akilini mwa Koplo Matata baada ya kuambiwa na Inspekta Wright afanye juu chini kupata habari za Denge. Anaamrishwa kumshawishi Yasmin kupitia njia zote hata akitaka atumie mbinu ya pesa zaidi ili kupata habari hizo. Mawazo haya yanamjia

alipokuwa akiendesha baiskeli yake taratibu bila ya kuwa na haraka kwani hakuwa na mahali maalum alipotaka kwenda.

Mawazo halisi yanadhihirika kutokana na matumizi ya alama za kunukuu na pia kupitia kwa matumizi ya viwakilishi vya wakati uliopo vinavyowakilishwa na “ni” kwenye neno “nitapata”. Kupitia kwa mawazo haya, tunabaini kuwa Koplo Matata ana matumaini makubwa kuwa atamnasa Denge kwani anaona Unguja ikiwa kama kijiji kidogo anachokifahamu vizuri. Msimulizi ametuwezesha kubaini kuwa Koplo Matata ana majukumu yanayomsubiri japokuwa anajipa moyo kuwa atamnasa Denge kwa vyovyote vile. Tunamfahamu Koplo Matata zaidi kutokana na jinsi msimulizi amemwasilisha kwetu.

Mfano mwingine wa mawazo halisi unapatikana kwenye mazungumzo ya Denge na nafsi yake.

> “Saa hizi kila mtu kashughulika. Nitampitia Yasmin.” (uk.156)

Mawazo haya yanatokea akilini mwa Denge baada ya kufika kutoka Nairobi ambako alikuwa ametowekea bila kumjuza yeyote alikokuwa. Denge alikuwa amebadilika sana kwani hakutaka ajulikane kwamba ni yeye kutokana na kuwa alijua kwamba bado askari wanamtafuta wamkamate. Uso wake ulikuwa umezungukwa na sharafa ya ndevu zilizoungana na nywele kubwa zilizochanwa vizuri zikapasuliwa njia upande wa kushoto. Baada ya kufika nyumbani kwake na kupumzika, anaamka na kwenda kwa kinyozi na hapo ndipo alianza kuwa na mawazo ya atakakokwenda na kuwa na mawazo mseto kwani hakujua aende kwa Yasmin, au akamtafute Sukutua na pia akaanza kujiuliza ikiwa polisi wanamtafuta. Anaamua kuwa angetaka kuwatafuta marafiki zake awahadithie aliyoyaona nao wamhadithie yao na mwishowe, anasema ataenda kwa Yasmin kwani watu wengi wakati ule walikuwa wameshughulika.

Mawazo halisi yanadhihirika kupitia kwa matumizi ya alama za mtajo na matumizi ya kiwakilishi cha wakati uliopo ambacho ni “ni” kwenye neno “nitampitia”. Msimulizi anatuwezesha kumfahamu Denge zaidi kwa kujua kuwa alikuwa amechanganyikiwa kwani hakujua aanze wapi na amalizie wapi kutokana na kutoweka kwake kwa muda.

Vilevile, kuna matumizi ya mawazo halisi yanayowasilishwa na mhusika Denge kwenye riwaya husika ya *Vuta N’kuvute* kama ifuatavyo:

> “Si kosa lake, wala si kosa langu, ni kosa la jamii yenyewe kwa jumla. Jamii Iliyomweka kila mtu katika hali duni kiasi ambacho mtu hana uhakika wa maisha yake peke yake wacha kuwa na mke.” (uk.164)

Mawazo haya yanampitikia Denge baada ya kupata barua iliyotoka kwa Yasmin alipokuwa anamweleza kuwa hata kama yuko mbali naye moyo wake uko pamoja naye na kumwambia pia asimkasirikie kwani wataonana Mungu akipenda. Baada ya Denge kusoma barua ile anahuzunika na kuiweka mfukoni na akaanza kusoma gazeti la siku ile na baada ya muda kidogo akajifunika na gazeti hilo na akaanza kumuwaza Yasmin. Maneno haya yanatokana na mawazo yanayomjia baada ya kusoma barua ile.

Mawazo halisi yanadhihirika kutokana na matumizi ya alama za mtajo zilizotumika kuonyesha uzungumzinafsi wa Denge na vilevile kupitia kwa matumizi ya kiwakilishi nafsi cha wakati uliopo “ni” anaposema kuwa, “ni kosa la jamii”. Msimulizi anatusaidia kumfahamu Denge zaidi kwani tunapata kujua kuwa anailaumu jamii kwa kuwaweka watu katika hali duni ambapo hawana uhuru wa kufanya maamuzi kuhusu maisha yao na inawafanya kufuata mambo yaliyopangwa na watu bila kuuliza chochote. Vilevile tunafahamu kuwa Denge anasononeka baada ya kumkosa Yasmin. Mbali na hayo, kuna mabadiliko kutoka usimulizi ambao ulikuwa wa nafsi ya tatu hadi wa nafsi ya kwanza kwani hapa tunapata kujua yanatukia akilini mwa Denge kwa njia ya moja kwa moja kama ni yeye anayesimulia.

Mfano mwingine wa mawazo halisi unapatikana tunapomwona Denge akiwaza alipokuwa na Yasmin baada ya kumwambia kuwa alikuwa mjamzito.

> “Haidhuru, matatizo ndiyo maisha yenyewe, bila ya matatizo hakuna maisha. Matatizo mengi nimekwishapambana nayo, mengine bado naendelea kupambana nayo na haya ya sasa wacha yawe pamoja na yale ninayopambana nayo.” (uk.129)

Mawazo haya yanatokea kwa Denge anapoanza kufikiri kuhusu maneno aliyoambiwa na Yasmin kwamba ana ujauzito. Anajiuliza kama ana ujauzito au ni utani tu lakini anasema kuwa hawezi kulea mimba ile kwani yeye ni hohe hahe. Leo anacho kesho hana, kesho kutwa hana, mtondogoo anacho. Baada ya haya ndipo anaanza kufikiri kuwa matatizo ndiyo hali ya maisha na atapambana nayo kwani bila matatizo maishani huwezi kupata nguvu za kupambana.

Mawazo halisi yanadhihirika kutokana na matumizi ya alama za mtajo pamoja na matumizi ya kiwakilishi cha wakati uliopo "ni" kwenye neno "ninayopambana". Msimulizi anatusaidia kumwelewa Denge zaidi kwani tunafahamu kuwa ni mtu mwenye matatizo mengi lakini yuko tayari kupambana nayo kwani anajiambia bila matatizo hakuna maisha.

### 2.5.2 Mawazo Taarifa

Mawazo taarifa huwa ni uwasilishaji wa mawazo ya wahusika kupitia kwa usemi taarifa. Nafsi ya tatu ndiyo hutumika kwa uwasilishaji huu na viwakilishi vinavyotumika huwa ni vya wakati uliopita. Riwaya ya *Vuta N'kuvute* ina mifano kadhaa ya mawazo taarifa. Kwa mfano:

Baada ya Yasmin kutoka Mombasa na kwenda kwa mjombake na kufukuzwa, anaamua kwenda kwa Mwajuma na ndipo mawazo haya yanamjia.

> Hapo tena fikira zilianza kutembea kichwani mwake na kuanza kujiuliza vipi ataweza kuyakabili maisha ilhali yu pekeyake na yeye bado yu ngali mtoto hata ubwabwa wa shingo bado haukumtoka. Alijiuliza vipi ataweza kujiendesha? Mpaka lini ataishi kwa Mwajuma, mtu aliyemjua kwa mazungumzo tu? Nini jamaa zake watasema wakiskia anaishi Uswahilini na Waafrika? (uk.18)

Yasmin anawaza jinsi atakavyoishi kwani anaona maisha yatamlemea na hajui ataanzia wapi. Haya yanatokana na kutoka kwake kwa Bwana Raza Mombasa na kwenda kwa mjombake na anapofika anafukuzwa na kuamua mwokozi wake atakuwa tu ni Mwajuma. Anawaza kwani yu ngali mtoto atawezaje kuishi kwa mtu ambaye hakumjua kwa undani mbali kwa mazungumzo tu lakini hana budi kwani hakuwa na pengine pa kwenda. Mawazo taarifa yanadhihirika kutokana na matumizi ya nafsi ya tatu kama vile kwenye maneno, "ataweza" na "ataishi" inayowakilishwa na matumizi ya kiambishi cha nafsi ya tatu "a". Vilevile, viwakilishi vilivyotumika ni vya wakati uliopita vinavyowakilishwa na "li" kama vilivyotumika kwenye maneno "zilianza", "alijiuliza" na "aliyemjua".

Mfano mwingine wa mawazo taarifa unatokana na mawazo ya Mwajuma baada ya kupigana na shogake Yasmin.

> Naye Mwajuma alikuwa na mtihani wake. Amekaa jikoni kimya akifumua nywele. Amezongwa na majuto anajiuliza. Kilimsibu nini hata ikajiri kupigana na shogaye mpenzi, hali ile aliyo mjamzito (uk.153)

Mawazo haya yanamjia Mwajuma baada ya kupigana na Yasmin. Anajiuliza nini kilimsukuma hadi apigane naye akiwa mjamzito na Yasmin ni rafikiye. Lakini baadaye wanazungumza na kusameheana na kuendelea na urafiki wao. Mawazo taarifa yanawasilishwa na matumizi ya viwakilishi vya wakati uliopita kupitia kwa matumizi ya kiambishi "li" kama ilivyo kwenye neno "alikuwa". Mbali na hayo, mawazo taarifa yanadhihirishwa na matumizi ya nafsi ya tatu kama inavyopatikana kwenye neno "amekaa" ambayo huashiriwa na matumizi ya kiambishi "a".

Mawazo taarifa yanadhihirika katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* baada ya Denge kutoka kwa Mwajuma akiwa ameandamana na Yasmin. Anapokuwa njiani anamfikiria Yasmin tu

> Njia nzima alimuwaza mtoto yule mzuri aliyeumbwa akaumbika. Alifikiri vipi ataweza kumwingia mtoto yule amwambie maneno aambilike (uk.44)

Mawazo haya ni ya Denge anapomfikiria Yasmin alivyo mzuri na anajiuliza anawezaje kumpata kwa kumwambia maneno aambilike. Kupitia kwa mawazo haya, tunafahamu kwamba Denge alikuwa na hamu sana ya kumpata Yasmin. Kinachodhihirisha mawazo taarifa ni matumizi ya viwakilishi vya wakati uliopita "li" kama vinavyopatikana kwenye maneno "alimuwaza na aliyeumbwa". Matumizi ya viwakilishi vya wakati uliopita vinaashiria kuwa ni jambo linaloripotiwa wala si usemi wa moja kwa moja.

### 2.5.3 Mawazo Taarifa Huru

Haya huwa ni mawazo ya mhusika yanayowasilishwa na msimulizi ambayo husaidia kuelewa tabia pamwe na hisia za mhusika kuhusu mambo fulani. Katika mawazo taarifa huru, huwa kuna mabadiliko ya nyakati ya wakati uliopita hadi uliopo na huwa na mabadiliko yanayowasilishwa kutoka kwa nafsi ya tatu hadi nafsi ya kwanza. Vilevile, huwa kuna matumizi ya vihusishi na viulizi na hakuna matumizi ya alama za mtajo kwa kuwa ni mawazo taarifa na yako huru kabisa. Riwaya ya *Vuta N'kuvute* inadhihirisha mawazo taarifa huru baada ya Gulam kupata barua iliyotoka kwa Bwana Raza.

> Yasmin, Yasmin, Yasmin gani naye? Lakini alifikiri na kuhisi kwamba Raza anampenda na apendacho mtu dawa. Alihisi kwamba Raza anaumwa na dawa yake ni Yasmin. Kwa nini asimsaidie? Lakini atamsaidiaje kiumbe huyu? Yeye mwenyewe hajui Yasmin alipo, na hata kama angejua alipo angemlazimishaje arudi Mombasa? (uk.74)

Mawazo haya yanamjia Gulam ambaye ni mjomba wa Yasmin baada ya kusoma barua iliyotoka kwa Bwana Raza. Barua ya Raza ilikuwa inaeleza masikitiko aliyokuwa nayo baada ya kumpoteza Yasmin na kumwomba Gulam amshauri Yasmin arudi kwani Raza alisema kuwa yupo tayari kumpokea wakati wowote na katika hali yoyote. Mawazo ya Gulam yanaonyesha kuwa, kwa upande mmoja angetaka au angemshauri Raza amsahau Yasmin kabisa na kuendelea na maisha yake na pia kwa upande mwingine, anamwonea huruma kwamba aliachwa pweke na anasononeka na mapenzi.

Mawazo taarifa huru yanadhihirika kutokana na uwasilishaji wa hisia za Gulam ambazo tunaona kwamba alikuwa na hisia za huruma kwa Raza na anaona itakuwa heri amsaidie kumpata Yasmin. Vilevile kuna mabadiliko ya nyakati kutoka wakati uliopita unaowakilishwa na matumizi ya viambishi "li" hadi wakati uliopo unaowakilishwa na viambishi "ni" kama inavyodhihirika kwenye maneno kama vile, "alifikiri", "alihisi" na "anampenda" na "anaumwa". Kutokana na mfano huu, ni wazi kwamba, kuna mabadiliko ya nyakati kutoka wakati uliopita hadi wakati uliopo.

Bukheti alipokuwa peke yake alikuwa na mawazo mbalimbali kuhusu jinsi arusi yake na Yasmin itakavyokuwa.

> Na hilo sanduku nalo, kwani litakuwa sanduku la aina gani? Litakuwa sanduku la kusambuliwa kitu kimoja kimoja kama arusi ya mwari? Hata hilo sanduku nalo si lazima. Kwanza mambo ya sanduku Wahindi yanawahusu nini? (uk.227)

Mawazo haya yanampitikia Bukheti anapotoka kwa Bashiri ambapo alimpa mawaidha kuhusu mke na kumwambia kuwa lazima awe makini sana anapomtafuta mke na anapoamua nani wa kuishi naye asije akajuta na kuomba ardhi ipasuke. Haya ni mawazo taarifa huru kwa kuwa tunajua hisia za Bukheti kuhusu sanduku analotaka kumzawadia Yasmin na tunagundua kwamba anaona hata halina maana kwani anasema kuwa Wahindi hawahusiani na masanduku. Vilevile kuna matumizi ya viulizi, Bukheti anapojiuliza maswali kama: "kwani litakuwa sanduku la aina gani? Kwanza mambo ya sanduku Wahindi yanawahusu nini?". Vilevile kuna mabadiliko ya nyakati kutoka wakati uliopita kama kwenye neno "litakuwa" na wakati uliopo unaonyeshwa kwa matumizi ya kiambishi "na" kwenye neno "yanawahusu".

## 2.6 Hitimisho

Sehemu ya pili ya utafiti wetu imeshughulikia uwasilishaji wa usemi na mawazo ya wahusika. Sehemu hii imebainisha aina mbalimbali za uwasilishaji usemi na mawazo ya wahusika huku zikionekana kama mbinu muhimu za uandishi kwa kuwa husukuma kasi ya msimulizi mbele. Utafiti huu umethibitisha kuwa uwasilishaji wa usemi na mawazo ya wahusika hutumia nafsi ya kwanza na ya tatu na pia uzungumzinafsi ni kipengele muhimu katika uwasilishaji wa usemi na mawazo ya wahusika. Utafiti huu vilevile umebaini kuwa mbinu ambayo imejitokeza sana ni ya usemi halisi kwani msimulizi amewahusisha wahusika wake katika mazungumzo mengi ndiposa aweze kupunguza umbali wa masafa baina yake na wao na mbinu ya usemi halisi huru haipo kwenye *Vuta N'kuvute*. Vilevile, kuna mbinu nyingine za uwasilishaji usemi kama vile muhtasari wa daigesia na muhtasari wa daigesia usio kamili. Hata hivyo, mbinu za uwasilishaji wa mawazo ni chache zikilinganishwa na za uwasilishaji wa usemi wa wahusika na kutokana na jambo hilo, utafiti wetu umebaini kuwa, hakuna matumizi ya mawazo halisi huru katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* kwani mbinu hii sio rahisi kuwepo katika matini nyingi. Sura yote kwa jumla imezungumzia usawiri wa wahusika ambao ni wa moja kwa moja na usio wa moja kwa moja na uwasilishaji wa usemi na mawazo ya wahusika. Masuala haya mawili yanahusiana moja kwa moja kwani ndipo uweze kuwaelewa wahusika zaidi, utazielewa tabia zao zinazowakilisha matendo, semi na mawazo yao.

# SURA YA TATU

# WAKATI NA MUUNDO WA SIMULIZI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii imechunguza wakati kama unavyojitokeza katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* kama kipengele kimojawapo cha simulizi. Wakati katika simulizi za kibunilizi unaweza kufafanuliwa kama uhusiano kati ya hadithi na matini. Rimmon-Kenan (2002) ameainisha wakati kwa namna mbili ambazo ni wakati hadithi na wakati matini. Wakati hadithi ni ule wakati ambao hadithi nzima huchukua kutoka mwanzo hadi mwisho na unaweza kuwa wa siku moja, siku kumi, mwaka mmoja au miaka mingi. Kwa upande mwingine, wakati matini, unafafanuliwa kama wakati unaomchukua msomaji kusoma matini fulani. Wakati matini hutofautiana kutoka kwa msomaji mmoja hadi mwingine kwani kasi za usomaji ni tofauti. Wakati matini hupimwa kwa kuzingatia idadi ya maneno, mistari au kurasa zinazopatikana kwenye matini husika.

Kimsingi, sura hii ilichunguza vigezo vitatu vilivyoko chini ya wakati ambavyo ni mpangilio wa matukio, muda wa utokeaji wa matukio na idadi ya utokeaji wa matukio hayo. Kauli zinazohusiana na mpangilio wa matukio, zilijibu swali la lini?  Kumaanisha la kwanza, la pili, la awali, la mwisho na la baadaye. Kauli za muda wa utokeaji wa matukio nazo zilijibu swali la kwa muda gani? Kama vile, saa moja, mwaka, muda mrefu na mwingineo. Kwa upande wa idadi ya utokeaji wa matukio hujibu swali la mara ngapi? Vigezo hivi ndivyo hutumika kuonyesha uhusiano uliopo kati ya wakati hadithi na wakati matini. Vigezo hivi vimechunguzwa kwa kutolewa mifano vinapopatikana kwenye riwaya ya *Vuta N'kuvute.*

## 3.1 Mpangilio wa matukio

Mpangilio wa matukio huhusisha jinsi matukio yamefuatana kwenye hadithi kiwakati au kwa kutozingatia wakati. Mpangilio sawa au mmoja wa msuko na hadithi huibuka matukio yanaposimuliwa kiwakati (Wamitila, 2002). Jambo la muhimu katika sehemu hii huwa ni kubainisha ni kipi cha kwanza, cha pili na cha tatu. Iwapo matukio yatasimuliwa pasipo na mfuatano wa kiwakati, analepsia na prolepsia huibuka ambazo husababishwa na mfuatano

wa ki-anakroni. Sehemu inayofuata ya utafiti itaangazia analepsia na prolepsia kama zilivyotumika kwenye riwaya husika ya *Vuta N'kuvute.*

### 3.1.2 Analepsia

Analepsia hutumiwa na mwandishi kama mbinu ya kuyaeleza matukio yaliyotokea wakati wa nyuma ya wakati wa hadithi. Analepsia hutoa habari zaidi za awali kuhusu mhusika, tukio au hadithi inayotajwa wakati huo kwenye matini au kuhusu mhusika mwingine anayesimuliwa. Kwa mfano, katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*, askari Keya anamweleza Denge walivyokuwa wakati wao. Anasema kuwa:

> Zama zetu tulivyokuwa mpakani, tukitwanga mwendo wa maili hamsini, sitini bila ya kujali, siyo nyinyi vijana wa siku hizi (uk.239)

Katika dondoo hili, tunafahamu maisha ya askari Keya yalivyokuwa zamani anapoeleza walivyokuwa wanatembea mwendo wa maili hamsini na tisini bila kujali. Jambo hili lilitokea awali wala sio wakati wa sasa wa hadithi. Maneno haya yanatufahamisha kuwa kuna tofauti iliyopo baina ya askari Keya na vijana wa sasa kwani anawachukulia kama watu wazembe. Mfano mwingine wa analepsia inayoeleza kuhusu maisha ya mhusika ni pale ambapo mfungwa anamweleza Denge kuhusu familia yake.

> Mimi nishakaa miaka mingi humu na dalili za mtu kutolewa nazijua. Sasa rafiki yangu ukitoka tafadhali kawape salamu watoto wangu, nimewaacha wadogo, sasa nafikiri washakuwa wakubwa. Waambiye mimi mzima wasitie wasiwasi. Waambiye wasiwache kuniombea dua Mungu anisaidiye (uk.179)

Kutokana na mfano huu, tunafahamu kwamba msimulizi ambaye ni mfungwa, alikuwa na familia ambayo alitengana nayo kwa miaka mingi tangu kukamatwa kwake. Kukamatwa na kutengana na familia yake ni jambo ambalo lilitokea zamani lakini analisimulia wakati wa sasa wa hadithi anapomtuma Denge akawasalimu na kuwaambia wazidi kumwombea.

Analepsia inaweza kuwa ya wasifu pale ambapo tunaelezwa kuhusu matukio yaliyopita kuhusu mhusika mwingine, matukio mengine au hadithi tofauti ambayo haiendani na kipindi cha hadithi iliyopo. Kwa mfano, Kermali anapomweleza mkewe kuhusu Gulam kuwa na mke Mswahili baada ya Yasmin kwenda kwa Kermali na kumwomba akazungumze na mjombake kuhusu mchumba wake anayetaka kumposa. Anasema:

> Sasa Yasmin anafuata nyayo. Yeye Gulam mwenyewe ana mke wa Kiswahili na Yasmin naye anataka kuolewa na Mswahili. Anaye mke Mswahili! Tena naye siku nyingi, amezaa naye watoto wawili wa kiume tena wakubwa sasa. Amemwoa kwa siri. Ni siri hajui mtu yeyote. Yuko Vikokotoni (uk.224)

Mfano huu ni analepsia wasifu kutokana na kuwa, Kermali alikuwa anazungumza na Yasmin kuhusu jinsi atakavyokwenda kwa mjombake Gulam kumwambia kwamba akamuombee radhi kwa wazazi wake na awaambie kwamba ataletewa posa. Baada ya Yasmin kuondoka, Kermali na mkewe wanaanza mazungumzo kumhusu Yasmin na kuyageuza na kuwa ya Gulam pale ambapo tunafahamu kuwa ana mke Mswahili ambaye amezaa naye watoto wawili. Msomaji anafahamu kuwa, jambo la Gulam kuwa na mke mwingine lilitokea zamani lakini linasimuliwa sasa kutokana na mkondo wa hadithi.

Kuna aina nyingine ya analepsia ambayo ni analepsia ya nje. Aina hii husimulia matukio ambayo huwa yalitokea kabla ya hadithi kuanza. Katika riwaya ya *Vuta N'kuvute,* kuna mfano wa aina hii pale ambapo Denge anamwelezea Sukutua alivyokuwa anaandamwa na askari baada ya kutoka Urusi, kiasi cha askari mmoja kumuuliza mambo yako vipi Urusi. Denge anamwambia Sukutua kuwa alimjibu kama ifuatavyo:

> "Nilimwambia Urusi kuna majumba marefu kama mnara wa Wailesi lakini watu wote wa nchi hiyo wafupi kama Athumani Kifupi" (uk. 46)

Kisa cha Denge na askari, kinatokea baada ya Sukutua kumwambia Denge kuwa angependa kumsaidia lakini anaogopa kwani akionekana akimpa pesa ripoti hiyo itawafikia polisi. Baada ya hili, Denge anamwambia Sukutua kuwa hata angetaka kufanya kazi hawezi kuipata kwani Waigereza hawawezi kumpa kazi mtu kama yeye kwani tangu atoke Urusi walipoona pasipoti yake kwenye uwaja wa ndege huwa wanamwandama na kumuuliza maswali, jambo linalompelekea kumwambia rafikiye jinsi askari mmoja alivyomuuliza na jibu alilompa. Matukio haya yalitokea kabla ya hadithi kuanza hata ingawa yanasimuliwa kwa sasa. Kutokana na mifano ya analepsia tuliyoiorodhesha, analepsia tawasifu, wasifu na analepsia ya nje ndizo zinajitokeza bila uwepo wa analepsia ya ndani.

### 3.1.3 Prolepsia

Prolepsia ni aina ya usimulizi ambapo, tukio au matukio ambayo yatatokea baadaye katika matini husimuliwa kabla hayajatokea. Prolepsia huwa chache kuliko analepsia katika kazi nyingi zinapolinganishwa. Prolepsia zinapotokea huwa zinajazilia taharuki ambazo hutokana na swali ambalo ni nini kitatokea baadaye? Na kuligeuza kuwa litatendeka vipi? Prolepsia inafaa kutofautishwa na utayarishaji au utoaji fununu kuhusu kitakachotokea baadaye. Prolepsia inaweza kujitokeza kama zinavyojitokeza analepsia na kutoa habari zaidi kuhusu mhusika, tukio au hadithi ambayo inakuja kutokea baadaye. Kwa mfano, Mambo, Yasmin, Mwajuma na Bukheti wanapozungumzia kitendo cha kumtorosha Denge gerezani, ni prolepsia kwani kitendo hicho kinakuja kutokea baadaye wanapofaulu kumtorosha.

> Wewe ni mmoja wetu, usiogope wala usihuzunike. Denge atatoka, tena tutamtoa sisi wenyewe. Mimi, wewe na wengine (uk.203)

Dondoo hili linatuonyesha jinsi Mambo anamfariji Yasmin kwa kumwambia asiogope kwani watamtoa Denge gerezani yeye na wengine ambao baadaye wanapanga mikakati kwa kushirikiana na askari na marafiki zao wanamtorosha Denge. Hii ni prolepsia kwani jambo la kumtorosha Denge linasimuliwa kabla ya kutokea japokuwa linatokea mwishoni. Hata hivyo, tukio linaposimuliwa kabla halijatokea, wakati mwingine sio lazima litendeke baadaye.

Kama zilivyo analepsia, prolepsia inaweza kuwa ya ndani, ya nje, prolepsia wasifu na prolepsia tawasifu. Mfano uliotolewa unadhihirisha kuwa, prolepsia ya ndani ndiyo inajitokeza kwenye riwaya husika bila uwepo wa prolepsia ya nje, wasifu na tawasifu.

## 3.2 Muda wa Matukio

Kipengele hiki huonyesha mfungamano uliopo katika hadithi husika kiwakati. Katika kipengele hiki, kipindi ambacho tukio huchukua ndicho huangaziwa. Kimsingi, muda unahusu mahusiano yaliyopo kati ya wakati hadithi na wakati matini. Wakati hadithi ni wakati ambao hadithi nzima inachukua na unaweza kupimwa kupitia kwa dakika, saa, siku, wiki, miezi na hata miaka kama asemavyo Rimmon-Kenan (2002:52). Wataalamu wengi huwa hawasemi wakati huo ni upi lakini unaweza kukisiwa. Kwa upande mwingine, wakati matini huwa ni wakati anaouchukua mtu kusoma hadithi fulani na hupimwa katika mistari na kurasa. Wakati matini hutofautiana kutoka kwa msomaji mmoja hadi mwingine kwani

wasomaji wana kasi tofauti tofauti. Hii ina maana kwamba, kuna msomaji anayeweza kuchukua siku moja kusoma matini fulani, mwingine akachukua wiki moja na mwingine akatumia muda wa mwezi mmoja kusoma matini ile ile moja.

Kasi ya usimulizi katika matini inaweza kuchukua miundo miwili ambayo ni kuharakishwa au kupunguzwa, jambo ambalo hutegemea msimulizi. Athari ambazo hutokana na uharakishwaji, huhusishwa na sehemu ndogo ya matini kupewa muda mwingi kwenye hadithi kama vile, maisha ya mhusika kuelezwa kwenye kurasa tano. Vilivile, kwenye upunguzwaji, sehemu kubwa ya matini inaweza kusimuliwa au kupewa kipindi kifupi sana kwenye matini kama vile, safari ya mhusika ambayo ilimchukua siku nne kuelezwa kwa mistari mitano katika hadithi. Rimmon-Kenan (2002), amebaini vipengele vinne vinavyohusiana na muda ambavyo ni, udondoshi, mtuo, muhtasari na onyesho.

### 3.2.1 Udondoshi

Udondoshi huhusisha kutosimulia tukio fulani au kutolieleza kwenye hadithi. Wakati matini huwa ni kama haupo lakini hadithi ina muda fulani kumaanisha kuwa, huwa kuna tofauti kati ya wakati hadithi na wakati matini. Msimulizi huonyesha kwamba jambo fulani si muhimu au kwa wakati ule sio muhimu kulisimulia. Msimulizi huweza kumpa msomaji nafasi ya kujaza mapengo yanayopatikana ya kiwakati jinsi atakavyo. Udondoshi unaweza kubainika moja kwa moja au usibainike waziwazi na huitaji umakinikaji kuutambua. Mifano mbalimbali ya udondoshi inadhihirika katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* kwenye sehemu mbalimbali kama vile, msimulizi anapotueleza kuhusu Bukheti aliposikia sauti kali ya mwimbaji wa Kihindi na kudhani kwamba Yasmin amerejea.

> Baada ya mwezi mzima, Bukheti kama aliyekuwa akiota akasikia sauti kali ya mwimbaji wa Kihindi, sauti ile ikapenya mpaka ndani ya moyo wake, ukachanua kwa furaha pale alipokuwa amekaa. Akadhani Yasmin amerudi na ile nyimbo ni ishara ya kumwita (uk.35)

Msimulizi anatuelezea kuhusu Bukheti kuwa chumbani mwake baada ya mwezi mmoja kupita bila kumwona Yasmin. Udondoshi unadhihirika pale ambapo, hatujaelezwa alikokwenda Bukheti wakati Yasmin akiondoka kwa Bwana Raza kwani aliishi kumtazama kwenye kidirisha bila kumwona. Udondoshi mwingine unapatikana pale ambapo msimulizi anatueleza jinsi Yasmin alivyobadilika na kuyazoea maisha ya Uswahilini na Waswahili wenyewe.

> Miezi kadha ilipita. Yasmin alikuwa amezama katika maisha ya Uswahilini ambayo kidogo kidogo alianza kuyazoea. Si kama aliyazoea maisha tu, bali na Waswahili wenyewe vilevile (uk.37)

Kutokana na maelezo ya msimulizi, inabainika wazi kwamba, kuna maelezo ya Yasmin ambayo yamedondoshwa kwani hatujaelezewa miezi ambayo ilipita baada ya kuja Uswahilini aliishije na alikuwa anafanya nini kwani tunaelezewa kumhusu baada ya miezi kadhaa ambapo tunampata akiwa amewazoea Waswahili na maisha ya huko. Mfano wa udondoshi vilevile unapatikana pale ambapo hatuelezwi alikokwenda Denge kwani alitoweka tu bila kumwambia mtu yeyote.

> Miezi mitano ilipita Denge hakuonekana wala hapana yeyote aliyejua habari zake (uk.149)

Udondoshi bayana unadhihirika katika dondoo hili kwani tunapata kujua kwamba, miezi mitano ilipita bila ya Denge kuonekana wala kujulikana alikokuwa. Msimulizi ameyadondosha mambo mengine yaliyotukia kwani labda aliona si muhimu kuyasimulia au kuyasimulia kwa wakati huo na kuamua kutujuza kuhusu wasiwasi aliokuwa nao Yasmin na marafiki wa Denge wakiwemo Mambo, Sukutua na Salum baada ya miezi hiyo mitano bila ya kutujuza walikuwa wanapitia nini kwenye miezi hiyo iliyopita. Msimulizi anatueleza mambo ya Yasmin kumtumia Denge barua baada ya kufika kwake Tanga.

> Siku kumi baada ya Yasmin kuondoka, Denge alipata barua kutoka kwake ikimweleza kufika kwake Tanga salama (uk.163)

Ni wazi kwamba kuna mambo ambayo msimulizi ameamua kutomjuza msomaji kuhusu maisha ya Yasmin. Jambo hili linatokana na msimulizi kutueleza kuhusu Yasmin kumuandikia Denge barua baada ya siku kumi bila kutujuza hizo siku zilizotangulia alikuwa wapi na alikuwa anafanya nini. Kwa hivyo, kuna sehemu ambayo msimulizi aliona kwamba sio muhimu kumjuza msomaji kwa wakati ule.

Wakati mwingine, msimulizi huwa hasemi muda unaodhihirika kwa msomaji bali husema kwa jumla tu na kumwacha msomaji aweze kukadiria muda usioelezwa unaweza kuwa upi. Kwa mfano, msimulizi anapotueleza kuhusu kuadimika kwa Denge.

> Siku nyingi zilipita bila ya Denge kupita kwa Mwajuma mpaka Mwajuma akasahau kama Denge aliwacha amana yake ndani ya nyumba ile (uk.52)

Muda ambao umerejelewa kwenye dondoo hili si bayana kwani hatuwezi kukadiria siku nyingi zilizopita zilikuwa siku ngapi labda wiki au miezi. Kutokana na matumizi ya maneno kama "siku nyingi", msomaji anapewa nafasi na msimulizi kujaza mapengo ya siku hizo atakavyo. Mfano mwingine unapatikana msimulizi anapotueleza kuhusu Yasmin na alivyoishi kwa Mwajuma.

> Kila siku zilipozidi kupita, Yasmin alizidi kujuana na kila aina ya watu katika mazingira aliyokuwa akiishi (uk.39)

Dondoo hili linatufahamisha kwamba siku zilivyozidi kupita, ndivyo Yasmin aliendelea kuwajua watu na kufahamiana zaidi na watu hao. Udondoshi unadhihirika ambao si bayana msimulizi anapotumia maneno "kila siku zilipozidi kupita", kumaanisha kuwa hatujui ni siku ngapi zilipita ndiposa tujue kuwa Yasmin alikuwa amezoeana na watu na mazingira alimokuwa akiishi.

Udondoshi unaweza kuwepo ambao hautaji chochote kuhusu muda uliopita. Hapa, msomaji hutakiwa kubaini kuwa kuna muda ambao umepita anapopata kujua kwamba kuna mwanya ambao ni wa kiwakati yaani, hakuna mfululizo kwenye hadithi. Kwa mfano, pale ambapo msimulizi anatuelezea kuhusu Denge na kundi lake walipokuwa kwenye ufukwe.

> Usiku ule ulikuwa mwema uliobarikiwa nyota nyingi na mwezi kamili na vyote hivyo vilikuwa vikicheka nao vikawakarimu nuru iliyong'arisha ufukwe wote pale walipokuwa wakihangaika kuishua mashua baharini (uk.196)

Kutokana na dondoo hili, tunafahamu kwamba kuna wakati ambao umepita lakini sio dhahiri. Hapa, tunapata mwanya wa mfululizo kwenye hadithi kwani tunajuzwa mambo yaliyokuwa yanatendeka usiku ule bila kujuzwa yaliyotendeka mchana. Udondoshi wa aina hii unasababisha mapengo ya kisimulizi. Mapengo haya huweza kumshughulisha msomaji pale tu anahisi kuwa pana taarifa au maelezo muhimu ambayo labda yangeboresha simulizi yameachwa.

Udondoshi umedhihirika katika sehemu nyingi za riwaya ya *Vuta N'kuvute* kutokana na mifano kama vile, maisha ya nyuma ya Bwana Raza hayaelezwi kwani tunapata kumjua akiwa na miaka hamsini na mbili, hatujaelezwa alikokwenda Bukheti baada ya kuagana na Yasmin kuwa wangeenda sinema, maisha ya Denge alipokuwa anaishi Nairobi yalikuwaje na

maisha ya rafikiye Denge waliyekamatwa pamoja yalikuwaje. Udondoshi unapotumika huweza kusaidia kuharakisha kasi ya hadithi kwani kuna mambo ambayo huwa yamebanwa na pia kwa kiasi kikubwa huleta taharuki kwa msomaji huku akiwa na hamu ya kutaka kujua zaidi.

### 3.2.2 Muhtasari

Katika kipengele cha muhtasari, hadithi huharakishwa kwa kubana muda fulani au kwa kutumia kauli zisizo ndefu. Kadri viwango vya ubanaji vinavyoweza kubadilika, husababisha mabadiliko ya muhtasari mmoja hadi mwingine, hivyo basi kuibua uharakishwaji wa aina mbalimbali. Katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*, kuna mfano wa muhtasari pale msimulizi anapotueleza kuhusu maisha ya Denge.

> Denge alimaliza darasa la nane skuli ya Gulioni na alifuzu vizuri mtihani wake. Aliingia darasa la tisa Government Secondary School. Alimaliza darasa la 12 na alishinda mtihani wa Cambridge daraja la kwanza. Mwaka huohuo aliajiriwa kazi ya ukarani katika baraza la mji wa Zanzibar. Mwaka mmoja baadaye mwanasiasa mmoja alimshauri kwenda Urusi kusoma. Aliomba ruhusa kazini kwenda likizo Nairobi, kwa hivyo haikuwa shida kwake kupata pasipoti ya kusafiria. Baada ya miaka mitano alimaliza masomo yake katika chuo kikuu cha Lomonosov na alipata shahada ya ubingwa katika mambo ya uchumi (uk.63)

Msimulizi anatueleza kuhusu maisha ya Denge kwa kifupi sana kwa kutusimulia alipomaliza darasa la nane, kumaliza darasa la kumi na 12 na kuwa bora, alivyopata kazi mwaka huohuo na alipoenda Lomonosov na kupata shahada ya uchumi baada ya miaka tano. Kuna mambo mengi ambayo msimulizi ameyabana kumhusu Denge kwani kuna udondoshi wa alivyokuwa anaishi akiwa na umri mdogo na alivyokuwa akifanya kazi na akisoma chuo kikuu. Kauli kama vile "baada ya miaka mitano" inaonyesha kuwa, kuna kipindi ambacho kimepita lakini msimulizi hakuona haja ya kusimulia mambo hayo bali aliona ayafupishe ili aweze kuharakisha hadithi na pia kufupisha muda wa usimulizi. Mfano mwingine wa muhtasari, ni pale ambapo msimulizi anatuelezea kuhusu Koplo Matata.

> Koplo Matata alijiunga na jeshi la polisi miaka kumi na mitano iliyopita na tokea kuanza kwake kazi alikuwa askari kanzu akishughulikia upelelezi wa mambo mbalimbali ya uhalifu. Kupanda kwake cheo kulikuwa ni kwa bahati nasibu tu, labda kwa elimu yake ndogo, lakini jinsi alivyokuwa na hamu ya ukubwa aliifanya kazi yake kwa bidii na hakuwa na msamaha kwa yeyote yule aliyewahi kumtia mkononi. Alivuma nchi nzima kwa ukali wake uliochanganyikana na utovu

wa huruma. Cheo cha ukoplo alikipata miaka miwili tu iliyopita baada ya kufanikiwa katika kesi moja ya upelelezi wa uvunjaji wa duka moja la sonara na kuibiwa vyombo kadhaa vya dhahabu. Sasa anafanya kazi katika kikosi maalum cha Special Branch ambacho kinashughulikia zaidi usalama wa serikali (uk.65)

Katika dondoo hili, tunaona kwamba maisha ya Koplo Matata yameelezwa kwa kifupi tukielezwa kuwa alijiunga na kikosi cha polisi miaka kumi na mitano iliyopita bila kuelezewa kabla ajiunge na kikosi hicho alikuwa wapi au akifanya kazi gani. Msimulizi anaeleza kwamba alianza kazi akiwa askari kanzu na hakuwa na elimu kubwa ndiposa alikuwa anapanda cheo polepole na baadaye ndipo alipata cheo cha ukoplo na sasa anafanya kazi katika kikosi cha Special Branch. Maisha ya Koplo Matata ambayo yangeelezwa kwa kurasa kadhaa yameelezwa kwa aya moja na kudhihirisha kwamba kuna mambo mengi ambayo yamebanwa.

Muhtasari umejitokeza katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* kupitia kwa mifano ya maisha ya Denge na Koplo Matata na kudhihirisha kuwa ni kipengele muhimu cha muda. Wakati hadithi umeharakishwa na wakati matini unafupishwa na kumfanya msomaji atumie muda mchache zaidi anaposoma matini husika.

### 3.2.3 Onyesho/ Maonyesho

Katika kipengele cha onyesho, hadithi na usomaji wake huenda pamoja. Mazungumzo huchukuliwa kuwa mbinu inayofaa zaidi kubainisha onyesho. Huelewaji zaidi wa wahusika hutokana na sifa ya uigizaji inayofungamanishwa na mazungumzo yao mbele ya msomaji. Jambo hili, husaidia kuwaelewa zaidi na hata wakati mwingine kudhihirika kwa hisia zao na pia mitazamo yao hutambuliwa na msomaji kutokana na mazingira anamopatikana mhusika. Hata ingawa mazungumzo ndiyo huwa muundo wa onyesho, usimulizi wa tukio kwa mapana unafaa pia kuchukuliwa kama onyesho. Riwaya ya *Vuta N'kuvute*, ina mifano ya mazungumzo ya wahusika mbalimbali kama vile mazungumzo kati ya Bwana Raza na Yasmin.

"Vipi?"

"Si hivyo ulivyo!"

"Niko vipi?"

> "Naona siku hizi …."
>
> "Siku hizi unaona nini?"
>
> "Naona siku hizi huchangamki, hata nachi huchezi tena."
>
> "Kwani umenioa niwe nikikuchezea nachi? Kama unataka kuchezewa nachi si wende senema! Una nini mtu mzima wewe?" (uk.13)

Mazungumzo ya Bwana Raza na Yasmin yanatokea baada ya Yasmin kugundua kuwa hamu yake haikuwa chakacha bali yule kijana aliyekuwa akimtazama kila mara akicheza chumbani mwake na baada ya Bwana Raza kuona Yasmin amebadilika na kuacha kumchezea nachi, ndipo anaanzisha mazungumzo haya. Kutokana na mazungumzo haya, sifa ya uigizaji inajitokeza wazi kwani wahusika wanaonekana wakizungumza mbele ya msomaji. Mazungumzo haya yanadhihirisha wazi kuwa kuna mgogoro kwenye ndoa ya Bwana Raza na Yasmin kuhusu masuala fulani. Sifa ya Yasmin ya kukosa heshima inajitokeza kutokana na jinsi anavyomjibiza Bwana Raza kwani hangestahili kumjibu mumewe hivyo. Vilevile, sifa ya Bwana Raza ambayo ni ya mtu makini inadhihirika anapobaini kuwa mkewe amebadilika na kuacha kumchezea nachi kama awali. Bali na hayo, msomaji anafahamu uhusiano uliopo kati ya Bwana Raza na Yasmin.

Onyesho limedhihirika tena kwenye mazungumzo ya Yasmin na Mwajuma baada ya Yasmin kufika kwa Mwajuma baada ya kufukuzwa na mjombake na kuanza kumweleza yaliyomfika kwa Bwana Raza kiasi cha kushindwa kuishi naye. Mwajuma anamkaribisha Yasmin kwa furaha na kuanzisha mazungumzo:

> "Enhe! Khabari za Mombasa?"
>
> "Khabari shoga yangu mbaya. Maisha na bwana mkubwa yule yamenishinda. Sina raha sina starehe, mwisho nimeona bora nirejee kwetu kwa wazee wangu. Nimekwenda kwa mjomba nimetimuliwa kama mbuzi na kwa mama naogopa kwenda manake maneno yake nayajua." "Sasa hata sijui la kulifanya usiku huu"
>
> "Maskini shoga yangu. Sasa una shauri gani?"
>
> "Sina shauri lolote, nimekuja kwako kukusikiliza utaniambia nini. Tafadhali nisitiri, nisitiri aibu yangu!"
>
> "Basi karibu shoga, tutajibana hapa hivyohivyo, ijapokuwa kitanda chenyewe kimoja." (uk.17)

Mazungumzo haya yanamwezesha msomaji kumfahamu Yasmin zaidi kwani tunafahamu kuwa amefukuzwa na mjombake na hana mbele wala nyuma. Vilevile, mazungumzo haya yanaibua maudhui mbalimbali kama vile maudhui ya ndoa, umaskini na urafiki kwani chumba cha Mwajuma kinadhihirisha umaskini kutokana na kuwepo kwa kitanda kimoja, wema wa Mwajuma kumsitiri Yasmin unadhihirisha urafiki na Yasmin kumtoroka Bwana Raza, kunaonyesha kwamba kulikuwepo na ndoa. Mazungumzo huwa mafupi kuliko simulizi yenyewe kwani huwa ni kijisehemu tu cha simulizi nzima. Mtazamo wa maisha alio nao Yasmin unadhihirika kutokana na kuwa anasema hata hajui la kufanya kwani anaona kama maisha yake yamefikia ukingoni.

Mazungumzo kati ya Denge na mfungwa aliyekuwa anamnyoa na aliyekuwa amemtuma akaiangalie familia yake, ni mfano mzuri wa onyesho kwani msomaji anapata kufahamu zaidi kuhusu wahusika na mitazamo yao kuhusu maisha. Mazungumzo haya yanaanzishwa na mfungwa anapomwona Denge tena kama ifuatavyo:

> "Umerudi rafiki yangu?"
>
> "Nimerudi na wewe bado umo humu?"
>
> "Mimi sitoki huku, labda itakayotoka ni maiti yangu."
>
> "Njoo nkunyowe rafiki yangu."
>
> "Inaonyesha wewe umo humu kuninyoa mimi tu."
>
> "Nafikiri ingelikuwa kila ninayemnyoa namtoza pesa, basi ningelikuwa milionea sasa."
>
> "Ungelikuwa mtu wa kwanza duniani kuwa milionea kwa kazi ya kunyoa."
>
> "Hebu rafiki yangu tuache utani, ulikwenda kuwaona watoto wangu?"
>
> "Nilikwenda."
>
> "Hawajambo?"
>
> "Hawajambo, washakuwa wakubwa ukiwaona huwezi kuwajua."
>
> "Lo! sijui nitawaona lini, bado wapo palepale?"
>
> "Wapo palepale lakini wana nia ya kuhamia Shamba."
>
> "Bora wende Shamba, unajua rafiki yangu maisha ya mjini yana shida siku hizi?"

> "Najua." (uk.218)

Mazungumzo ya Denge na mfungwa yamewasilishwa kwa msomaji kama uigizaji. Masuala mbalimbali yanajitokeza yakiwemo suala la familia ya mfungwa na kazi aliyoifanya huko gerezani ya kuwanyoa wafungwa wenzake. Mitazamo ya wahusika hawa kuhusu maisha inabainika. Mfungwa anaonekana kutokuwa na matumaini yoyote ya kutoka gerezani kwani anasema labda maiti yake ndiyo itakayotoka. Vilevile, wote wana mtazamo sawia kuhusu maisha ya mjini kwani wanayaona yakiwa magumu kulingana na nyakati. Kutokana na urefu wa mazungumzo haya, kunatokea matini ndefu kwani yamechukua nafasi kubwa katika matini husika. Pamoja na hayo, msomaji anamwamini msimulizi kwani kutokana na jinsi anavyowawasilisha wahusika wake kwenye mazungumzo, anaonekana kuwafahamu na kwa hivyo, anaweza kutegemeka.

Onyesho ni kipengele muhimu cha muda, kwani humsaidia msomaji kuwafahamu zaidi wahusika waliomo katika matini fulani, humsaidia pia kubaini migogoro inayowakumba wahusika mbalimbali, pia huibua maudhui mbalimbali na kufahamu mitazamo waliyonayo wahusika kulingana na mazingira wanamopatikana. Sifa muhimu katika onyesho ni idadi ya ujumbe na uwezo wa msimulizi wa kuwasilisha ujumbe huo.

### 3.2.4 Mtuo

Mtuo kama asemavyo Rimmon-Kenan (2002), hujihusisha na vijisehemu au kijisehemu cha matini na wakati hadithi kutokuwepo. Katika mtuo, huwa kuna mwanya ambao hupunguzwa na kuwa muhtasari na onyesho. Kwenye mtuo, msomaji huhisi kama hadithi imesitishwa na msogeo au mwendo wa hadithi haupo. Mtuo unaweza kuwasilishwa na mambo kama vile, wakati msimulizi anaposimulia yanayotukia akilini mwa mhusika au anapoeleza kuhusu jamii fulani.

Ndoto inaweza kutumiwa kama mfano wa mtuo kwani hadithi yenyewe huwa imesitishwa na kuonyesha kwamba haiendelei. Kwa mfano ndoto ya Denge alipokuwa gerezani akiota kumhusu Yasmin imeelezewa kama ifuatavyo:

> Usiku wa manane, usingizi mzito ulipokuwa umemchukua aliota amemkumbatia Yasmin wanajibizana maneno ya mapenzi na katikati ya ndoto yake tamu alishituliwa na mtu aliyemsukuma huku akitukana, "mjinga we! Unanikumbatia unafikiri mimi mkeo!" (uk.210)

Ndoto ya Denge akiwa amemkumbatia mpenziwe Yasmin huku wakiambizana maneno ya mapenzi inayompelekea kutukanwa na mfungwa aliyemkumbatia, inaonyesha kuwa hadithi imesitishwa kwa muda kwani mhusika hatendi lolote bali amelala. Jambo kama hili husababisha ufupishaji wa wakati hadithi kuliko wakati matini.

Vilevile, mtuo unaweza kujitokeza pale ambapo msimulizi anaeleza kuhusu tabia ya mhusika fulani jambo ambalo husitisha hadithi. Kwa mfano, msimulizi anapoeleza tabia ya Bwana Raza anamwezesha msomaji kumjua zaidi.

> Anapokuwa katika kazi hiyo ya kufanya hesabu, Bwana Raza huvuta biri moja baada ya moja na moshi wa biri hizo huhanikiza harufu yake mbaya nyumba nzima (uk.2)

Hadithi ambayo ilikuwa inahusu mazungumzo ya Bwana Raza na Yasmin kuhusu vitumbua vilivyoletwa na msimulizi imesitishwa na badala yake anaanza kueleza kuhusu tabia ya Bwana Raza. Kutokana na jambo hili, inafahamika kuwa, ilikuwa ni tabia ya Bwana Raza ya kuvuta biri kila alipokuwa anafanya hesabu. Msimulizi anapotoa maelezo kuhusu mandhari fulani, huwa amesitisha hadithi. Kwa mfano, msimulizi anapotoa taswira ya mandhari ya Pigale Hotel anaeleza kuwa:

> Mandhari yalikuwa matulivu kwenye ukumbi wa kulia ambao ulimulikwa na mwanga mwekundu uliofifia. Meza zilikuwa zimepangwa vizuri moja hapa nyengine pale na zilikuwa zimetandikwa vitambaa safi vyeupe. Juu ya kila meza uliwekwa mtungi wa maua yaliyochanua vizuri. Visu na vijiko vikawa vimepangwa kwa ustadi juu ya meza zile mbele ya kila kiti katika viti vilivyozizunguka meza hizo (uk.159)

Kutokana na maelezo ya mandhari ya Pigale Hotel, ni wazi kwamba msimulizi amesitisha hadithi ili aweze kutoa maelezo kuhusu mandhari ya mahali pale. Mandhari haya yanapoelezwa, yanampa msomaji taswira ya mahali pale hata ingawa hapajui. Maelezo kama haya yanapotokea, utendaji huwa haupo kwani maelezo ya msimulizi ndiyo hutawala kwa wakati huo. Kipengele cha mtuo ni muhimu kwani humpa msomaji uelewa wa mambo mengine ambayo hangeyafahamu katika matini husika. Baada ya kuchanganua kipengele cha muda, kipengele kilichofuatia ni cha idadi marudio kwa kuonyesha jinsi kilivyojitokeza katika riwaya husika.

### 3.3 Idadi Marudio

Idadi marudio ni dhana ambayo hutumiwa kuonyesha uhusiano uliopo baina ya utokeaji wa tukio, yaani ni mara ngapi tukio fulani limetokea na mara ambazo tukio hilo linasimuliwa. Idadi marudio pia huhusisha urudiaji ambao huchukuliwa kama dhana iliyoko akilini inayofanikishwa kutokana na kuondolewa kwa sifa mahsusi za kila tukio na uhifadhi wa zile ambazo zinahusisha matukio sawia pekee. Kwa kawaida, hamna tukio ambalo linaweza kurudiwa lilivyo au sehemu ya matini kurudiwa kama ilivyo kwani, hupatikana kwenye miktadha tofauti jambo ambalo husababisha mabadiliko kimaana. Idadi marudio inaweza kuchukua miundo tofauti ambayo ni; usimulizi mosi, usimulizi rudufu na usimulizi banifu.

#### 3.3.1 Usimulizi Mosi

Usimulizi mosi ni aina ya usimulizi ambao, tukio hutokea mara moja na kusimuliwa kwenye sehemu moja au kwa wakati mmoja tu. Aina hii ya usimulizi ndiyo hupatikana kwa kiasi kikubwa katika simulizi. Riwaya ya *Vuta N'kuvute* ina mifano maridhawa ya usimulizi mosi. Kwa mfano, Yasmin anapomkosea mumewe Bwana Raza heshima kutokana na kuulizwa mbona siku hizi hachezi nachi, anamjibu kwa dharau kwa kumwambia kwamba hakumuoa awe akimchezea na kama anataka kuchezewa nachi aende senema. Kutokana na majibizano yao, Bwana Raza anapandwa na hasira na kuishia kumpiga Yasmin.

> Kabla hakumaliza aliyotaka kusema Yasmin alitandikwa kofi kubwa; vimulimuli kila rangi vikawa vinameremeta mbele ya macho yake. Nuru iliyojaa ukumbini ikapotea mbele ya macho yake pakawa kiza kitupu. Hajawahi kumaliza akachapwa kofi la pili (uk.14)

Katika dondoo hili, tunaona jinsi Yasmin alitandikwa kofi moja na kabla hajamaliza kuzungumza akatandikwa la pili jambo linalompelekea kuchomoka kwa ghafla na kukimbilia mlangoni na kukimbia akatoweka. Kitendo hiki kimetendeka mara moja tu na kimesimuliwa mara moja tu wala hakipatikani mahali pengine katika riwaya nzima. Kisa cha vita vya Yasmin na Mwajuma, ni mfano mwingine wa usimulizi mosi tunapowaona Yasmin na Mwajuma wakipigana na baadaye kujawa na majuto.

> Aliponyanyuka pale, Mwajuma akamchupia Yasmin wakaburushana mpaka nje ya chumba, akamudu kumwangusha Yasmin chini akaanguka kifudifudi akamkalia kiunoni. Akazikamata nywele zake akazivuta kama wenye kuvuta hatamu farasi. Vita vile viliendelea kila mmoja akivunjwa na matusi, midomo haina breki. Wanatukana watakavyo (uk.152)

Vita vya Yasmin na Mwajuma ambavyo vilitokana na Mwajuma baada ya kuitwa kahaba na Yasmin, ni mfano mzuri wa usimulizi mosi kwani vilitokea mara moja na kusimuliwa mara moja tu. Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kwamba, tukio lina uwezo wa kutokea mara moja na kusimuliwa kwenye sehemu moja tu bila kurudiwa tena katika kazi nzima.

### 3.3.2 Usimulizi Rudufu

Hii ni aina ya usimulizi ambayo huhusisha tukio kutokea mara moja na kusimuliwa mara nyingi kumaanisha kuwa, huwa kuna urudiaji wa kisimulizi. Usimulizi huu unapojitokeza, kuna uwezekano wa kuwepo au kutokuwepo kwa mabadiliko ya msimulizi, muda, muundo au kinachozungumziwa. Kunapokuwa na urudiaji huu, sio lazima maneno yaleyale yatumiwe kwani huwa yanategemea muktadha yanamopatikana. Riwaya ya *Vuta N'kuvute* ina mifano inayojitokeza ya usimulizi rudufu kama vile kuachana kwa Yasmin na Bwana Raza. Jambo hili lilitokea mara moja tu walipokuwa Mombasa baada ya Yasmin kupigwa na Bwana Raza lakini limesimuliwa zaidi ya mara tano. Kwa mfano, Yasmin anapokwenda kumtembelea mjombake baada ya kutoka Mombasa, tukio la kuachana na Bwana Raza linajitokeza wanapozungumza.

> "Nakuuliza mume wako yuko wapi?"
>
> "Yuko Mombasa, mimi nimerudi. Nimeshindwa kuishi naye." (uk.16)

Kuachana na Bwana Raza kulitokea mjini Mombasa lakini Yasmin anapokosa pa kuenda akijiuliza aende kwa mamaye huku akihofia kutukanwa, anaamua kuenda kwa mjombake. Wanapozungumza, Yasmin anasema kuwa ameshindwa kuishi na Bwana Raza kumaanisha kuwa waliachana au alimwacha Bwana Raza jambo ambalo linamfanya Yasmin kufukuzwa na mjombake na kuambiwa atafute pa kwenda.

Tukio hili pia limesimuliwa tena Yasmin wanapokutana na rafikiye Mwajuma baada ya Yasmin kuhangaika akijiuliza atakwenda wapi kwengine kwani amefukuzwa kwa mjombake. Mazungumzo baina ya Yasmin na Mwajuma, ndiyo yanatuwezesha kubaini kuwa Yasmin anasimulia tukio hilo kwa mara nyingine.

> "Enhe! Khabari za Mombasa?"
>
> "Khabari shoga yangu mbaya. Maisha na bwana mkubwa yule yamenishinda. Sina raha Sina starehe, mwisho nimeona bora nirejee kwetu kwa wazee wangu. Nimekwenda kwa mjomba

> nimetimuliwa kama mbuzi na kwa mama naogopa kwenda manake maneno yake nayajua." (uk.17)

Hii ni mara ya tatu tukio la Yasmin na Bwana Raza kusimuliwa kwani baada ya Yasmin kumsimulia mjombake, anaenda kwa rafikiye Mwajuma na kumwambia kuwa, maisha yamemshinda na hakuwa na budi kuondoka kwa bwana yule kwani hakuwa na raha wala starehe. Tukio hili linaporudiwa kusimuliwa, kuna mabadiliko ya miundo ya maneno kwani Yasmin anapomsimulia mjombake anasema kuwa "amechoka kuishi naye" na anapokwenda kwa Mwajuma anatumia jina "Bwana mkubwa" ilhali anamrejelea mtu mmoja ambaye ni Bwana Raza.

Tukio la kuachwa kwa Bwana Raza na Yasmin linapatikana tena kwenye riwaya ya *Vuta N'kuvute,* kwenye barua ya Bwana Raza aliyomwandikia Gulam mjombake Yasmin. Msimulizi anaeleza hali aliyokuwa nayo Bwana Raza kiasi cha kufikia kuandika barua ili Yasmin ashauriwe kumrudia.

> Mjomba wa Yasmin aliipata barua kutoka Mombasa. Bwana Raza akieleza masikitiko yake ya kukimbiwa na mkewe mpenzi (uk.74)

Barua ya Bwana Raza kwa Gulam, inasimulia tena tukio la kuachana au kukimbiwa Bwana Raza na Yasmin. Kupitia kwa barua hii, tunagundua kwamba Bwana Raza alikuwa na masikitiko mengi na anamuomba Gulam azungumze na mpwaye amlaani shetani awaze mbele na nyuma na arudi kwake. Tukio hili linaposimuliwa tena, kuna mabadiliko ya msimulizi kwani matukio tuliyoorodhesha mwanzoni yalikuwa yanasimuliwa na Yasmin lakini tukio hili limesimuliwa na msimulizi wa hadithi kupitia kwa barua.

Baada ya Yasmin kukamatwa na Koplo Matata, tukio lake la kuachana na Bwana Raza linajitokeza tena kwenye masimulizi yao kwani Koplo Matata alitaka kutumia jambo hilo kama kisingizio cha kupata habari zaidi kumhusu Denge.

> "Nakuuliza umeolewa?"
>
> "Nimeachwa."
>
> "Lini?"
>
> "Siwezi kukumbuka."

> "Hukuachwa, umemkimbia mumeo."
>
> "Jamani nakwambieni nimeachwa!"
>
> "Mimi nakwambia hukuachwa ila ulimkimbia mumeo."

Mazungumzo ya Yasmin na Koplo Matata yanaibua tukio la kuachana kwa Yasmin na Bwana Raza. Yasmin anamweleza kwamba ameachwa ilhali Koplo Matata anasisitiza kuwa, hakuachwa mbali alimkimbia mumewe. Tukio la Bwana Raza na Yasmin kuachana linaposimuliwa hapa, tunapata kwamba kuna mabadiliko ya wakati kwani tukio hili liliposimuliwa kabla lilisimuliwa kwa muda tofauti na linaposimuliwa hapa.

Usimulizi rudufu unatokea tena kwenye tukio la Yasmin kufukuzwa kwa mjombake alipokwenda kumtembelea baada ya kuachana na Bwana Raza akiwa na matumaini ya kusitiriwa naye. Tunampata Yasmin akimsimulia Mwajuma kuwa alifukuzwa kwa mjombake.

> "Nimeenda kwa mjomba nimetimuliwa kama mbuzi." (uk.17)

Tukio hili lilitokea kwa mara ya kwanza Yasmin alipoenda kwa mjombake lakini Yasmin analisimulia kwa Mwajuma kwani alikuwa hana pa kwenda mbali kwa Mwajuma ambaye alikuwa rafikiye. Anamwelezea haya ili aweze kumsaidia kwani aliona hana mbele wala nyuma na hata akafikiri akienda kwa mamake atatukanwa kwani alimfahamu vyema.

Jambo hili la kufukuzwa kwa Yasmin na mjombake, linasimuliwa tena na msimulizi anapoeleza jinsi Yasmin aliyazamia maisha ya Uswahilini baadaye na kuanza kuyazoea. Anasema kwamba hakuyazoea maisha hayo tu bali na Waswahili wenyewe.

> Juu ya kuyazoea maisha hayo, haikuwa rahisi kwake kuwasahau wazee wake ijapokuwa kwa mjomba wake amekwisha fukuzwa kwa kashfa na taadhira (uk.37)

Kisa cha Yasmin kinasimuliwa tena na wakati huu kuna mabadiliko ya msimulizi na muda. Wakati wa kwanza wa kisa hiki kusimuliwa, kilisimuliwa na Yasmin alipokwenda kwa Mwajuma kwani hakuwa na pengine pa kwenda na mara ya pili, msimulizi wa hadithi ndiye anayesimulia kisa hiki. Vilevile muda umebadilika kwani kisa hiki kinaposimuliwa mara ya pili ni baada ya Yasmin kuwa ameyazoea maisha ya Uswahilini sio kama mwanzoni alipokuwa ndio amefika Uswahilini tu. Urudiaji wa sehemu hii unadhihirisha kuwa,

japokuwa Wahindi walichukuliwa kuwa watu wa kifahari, Yasmin anaonyesha kuwa, hamna mtu asiyeweza kuhitaji msaada kwa mwenzake hata kama ni watu wa makabila tofauti na viwango tofauti maishani.

Kitendo cha Denge ambacho ni kuvamiwa na askari chumbani mwake, kilitokea mara moja lakini kimesimuliwa mara kadha. Kwa mfano, Mambo anaporejea nyumbani kutoka kazini, anamkuta Denge amesimama mbele ya chumba chake na ndipo mazungumzo yao yanaanza jambo linalopelekea Denge kumweleza Mambo kuwa walivamiwa na askari.

> "Nikwambie nini rafiki yangu."
>
> "Nini tena?"
>
> "Askari wametuingilia leo."
>
> "Humu ndani?"
>
> "Humu ndani." (uk.114)

Denge anaposimulia tukio la kuingiliwa na askari kwake, ni dhihirisho wazi kuwa ni jambo ambalo lilitendeka na linasimuliwa kwa mara nyingine. Jambo hili linamfanya Mambo kumwambia Denge wawe waangalifu kwani inaonekana kuwa polisi hawakujua kwamba kuna jamaa wengine mbali na Denge peke yake na ingefaa jamaa wengine wajuzwe wasiweke vitu vya maana ovyo majumbani mwao.

Tukio la Denge la kuvamiwa na askari linasimuliwa tena na Mambo walipokuwa wakistarehe kwa kunywa pombe katika baa ya Minara Miwili. Mambo anakatisha soga la wenzake na kutaka wamsikilize.

> "Jamani leo askari wametufanyia mambo makubwa, wametuingilia nyumbani bila ya hata kufanya heshima, utadhani labda wameingia ndani ya nyumba ya wezi. Wamevunja mlango wa nyumba na walipoingia ndani walivuruga kila kitu." (uk.118)

Japokuwa tukio hili lilitokea mara moja, linasimuliwa mara mbili zaidi na wasimulizi tofauti. Msimulizi wa kwanza alikuwa Denge kwa Mambo na msimulizi wa pili ni Mambo kwa rafikize kina Chande, Sukutua na Huseni. Vilevile, muda wa usimulizi unabadilika kwani mara ya kwanza tukio hili linasimuliwa punde tu Mambo anapowasili nyumbani kutoka kazini ilhali wakati wa pili tukio hili linasimuliwa kwenye baa ya Minara Miwili. Vilevile,

maneno na miundo ya sentensi imebadilika kwani matukio haya yanapatikana kwenye miktadha tofauti.

### 3.3.3 Usimulizi Banifu

Usimulizi banifu ni aina ya usimulizi ambao, tukio ambalo limetokea mara nyingi huwa linasimuliwa mara moja tu. Riwaya ya *Vuta N'kuvute* ina mifano maridhawa ya matukio yaliyotokea mara nyingi lakini yakasimuliwa mara moja kama vile kitendo cha Mwajuma kwenda densi kila jumamosi.

> Kila Jumamosi alikuwa hakosi densini na alikuwa mpenzi mkubwa wa taarabu (uk.20)

Ni dhihirisho wazi kwamba Mwajuma alikuwa mpenzi wa taarabu na alikuwa anapenda densi sana. Matumizi ya maneno "kila Jumamosi" yanadhihirisha kwamba ni jambo ambalo Mwajuma alikuwa analifanya ifikapo Jumamosi kwa hivyo, ina maana kuwa ni jambo alilokuwa akilifanya mara nyingi lakini linasimuliwa mara moja tu. Tabia ya Yasmin ya kumtembelea Mwajuma ni mfano mwingine wa usimulizi banifu kutokana na maelezo ya msimulizi.

> Kila alipopata nafasi, Yasmin hupenya na kumtembelea Mwajuma nyumbani kwake naye alikuwa ni mtu wa pekee ambaye Yasmin alimhadithia dhiki anayoiona kuishi na mume zee kama lile (uk.4)

Kutokana na maelezo ya msimulizi, ni wazi kwamba Yasmin alikuwa na mazoea ya kwenda kwa Mwajuma na kumhadithia maisha ya dhiki ya kuishi na mume mzee. Matumizi ya maneno "kila alipopata nafasi" yana maana kuwa hakikuwa kitendo cha siku moja mbali mara nyingi tu ambayo Yasmin alienda kumtembelea Mwajuma kila wakati alipopata nafasi.

Maelezo ya msimulizi kumhusu Bashiri vilevile, yanaonyesha mfano mzuri wa usimulizi banifu kwani anaieleza tabia aliyokuwa nayo Bashiri kila wakati aliposhiba. Anasema kuwa, alikuwa na tabia ya kulipigapiga tumbo lake aliposhiba.

> Hiyo ilikuwa ni tabia yake kila anaposhiba, kulipigapiga tumbo lake (uk.72)

Tendo la Bashiri la kushikashika tumbo lake kila anaposhiba, linaonekana kuwa ni jambo alilolizoea na kulifanya mara kadha wa kadha kwani kuna matumizi ya maneno "hiyo ilikuwa ni tabia yake". Maneno haya yanaweka wazi kuwa, halikuwa jambo alilolifanya siku

moja mbali alilifanya siku nyingi hadi likawa jambo la mazoea. Vilevile, Bashiri ana tabia ya kunywa kahawa kila anapotoka msikitini kama inavyodhihirishwa na maneno ya msimulizi kama ifuatavyo:

> Chupa nzima ya kahawa ikaletwa na vikombe vya kahawa vinne. Hiyo ni desturi yake. Akisharudi msikitini tu, hukaa hapo na chupa yake ya kahawa na kila apitaye na kumjulia hali, basi atamkaribisha, anywe angalau kikombe kimoja (uk.225)

Matumizi ya maneno kuwa "hiyo ni desturi yake" yanadhihirisha wazi kwamba, Bashiri alikuwa anakunywa kahawa kila siku mara tu alipotoka msikitini na alikuwa akimkaribisha yeyote aliyekuwa anamwamkua.

Kitendo cha Bwana Raza cha kuvuta biri akifanya hesabu ni kitendo alichokizoea kila siku. Msimulizi anaeleza kuwa, anapokuwa katika kazi hiyo ya kufanya hesabu, Bwana Raza huvuta biri moja baada ya moja na moshi wa biri hizo huhanikiza harufu yake mbaya nyumba nzima (uk.2). Matumizi ya mofu "hu" kwenye kitenzi "huvuta" kunaonyesha kuwa ni hali ya mazoea kwa Bwana Raza kuvuta biri kila afanyapo hesabu. Hili linaonyesha kuwa kitendo hiki hufanyika mara nyingi lakini kinasimuliwa mara moja tu.

Tabia ya Yasmin kulala pindi inapofika usiku ni mfano wa usimulizi banifu kwani ni jambo ambalo hulifanya kila siku kama msimulizi anavyoeleza. "Inapofika usiku yeye huwa amejichokea na hulala mara tu baada ya kukiweka kichwa chake juu ya mto". Matumizi ya mofu "hu" katika kitenzi "hulala", ni dhihirisho wazi kuwa ni tabia ya mazoea ya Yasmin kulala pindi anapojiwekelea tu kwenye mto.

Ni wazi kwamba katika sehemu hii ya usimulizi banifu, tukio linatokea mara nyingi lakini linasimuliwa mara moja jambo ambalo hufupisha wakati hadithi na wakati matini. Msimulizi hutumia maneno mbalimbali kusimulia matukio yaliyotokea mara nyingi na kuyafanya yaonekana kama yalitokea mara moja tu.

### 3.4 Hitimisho

Sura hii imechunguza kipengele cha wakati kwa kuonyesha jinsi wakati unavyodhihirika katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*. Utafiti wetu ulibaini kuwa matukio yamepangiliwa kwa ki-anakroni yaani kwa matumizi ya analepsia na prolepsia japokuwa prolepsia haijajitokeza kwa wingi kama ilivyo analepsia. Kwa kuzingatia muda wa utokeaji wa matukio, udondoshi

umejitokeza zaidi pamoja na maonyesho ikilinganishwa na muhtasari na mtuo. Katika idadi ya utokeaji wa matukio, imebainika kuwa, kuna matukio ambayo yametokea mara moja na kusimuliwa mara moja, matukio mengine yametokea mara nyingi na kusimuliwa mara moja na tukio kutokea mara moja na kusimuliwa mara nyingi. Hata hivyo, maneno na miundo ya sentensi inayotumika kwenye urudiaji wa matukio sio sawa kwani hayapatikani kwenye miktadha sawia.

# SURA YA NNE

# USIMULIZI NA MTAZAMO KATIKA *VUTA N'KUVUTE*

## 4.0 Utangulizi

Usimulizi ni kipengele muhimu sana katika simulizi kwani huhusisha mchakato wa anayesimulia hadi anayesimuliwa pamoja na mbinu za uwasilishaji wa ujumbe. Rimmon-Kenan (2002), anasema kwamba, uboreshaji wa mawasiliano huhusisha wahusika wanne wakuu ambao ni mwandishi ambaye ni binadamu, msomaji, msimulizi na msimuliwa. Hata hivyo, kilichoko muhimu zaidi ni msimulizi na msimuliwa. Kwenye sura hii, tutaangazia riwaya ya *Vuta N'kuvute*, kwa kuchunguza aina za usimulizi, utambuzi wa msimulizi na mtazamo pamoja na aina zake na sawia zitumiwazo kwenye uchunguzi wake.

## 4.1 Aina za Usimulizi

Usimulizi unaweza kuainishwa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vikiwemo kigezo cha wakati, nafsi na vinginevyo. Utafiti wetu utajihusisha na kigezo cha wakati na cha nafsi. Tunapoangazia kigezo cha wakati, tunapata usimulizi wa baadaye, usimulizi wa kitabiri na usimulizi sawia.

### 4.1.1 Usimulizi baadaye

Rimmon-Kenan (2002:90) anasema kuwa, usimulizi wa matukio hutokea baada ya kutokea kwake. Masafa baina ya msimulizi na matukio hubadilika kutoka matini moja hadi nyingine. Hii ndiyo aina ya usimulizi ambayo hutumika sana. Kiambishi 'li' cha wakati uliopita ndicho hutumika kuonyesha usimulizi baadaye kwani matukio huwa tayari yashatokea. Kimsingi, hii ndiyo aina ya usimulizi ambayo inatawala hadithi hii. Kwa mfano, msimulizi anaposimulia jinsi Bwana Raza alimpiga Yasmin,

> Kabla hakumaliza aliyotaka kuyasema Yasmin alitandikwa kofi kubwa vimulimuli kila rangi vikawa vinameremeta mbele ya macho yake. Hajawahi kumaliza akachapwa kofi la pili. Yasmin alianguka juu ya kochi kama mzigo anatweta kama mgonjwa wa pumu (uk.14)

Kutokana na mfano huu, ni wazi kwamba matukio haya yalitokea kabla ya usimulizi wake. Matumizi ya kiambishi 'li' kwenye maneno "aliyotaka", "alitandikwa" na "alianguka"

kinadhihirisha kuwa ni matukio ya wakati uliopita. Msimulizi anapotueleza jinsi Denge alivyokuwa akila, ni mfano mwingine wa usimulizi wa baadaye.

> Alipowekewa chakula mbele yake, alifakamia kama anayefukuzwa. Alikatakata slesi ya mkate, akakikata kiwanda pande mbili na kuizonga ile slesi kwa upande wa kiwanda akafinyangafinyanga na kubugia. Alinyanyua kikombe cha chai akanywa mafunda matatu mfululizo. Angeimaliza yote kwa mkufuo mmoja lakini ilikuwa i moto. Alipoweka kikombe juu ya kisahani chake alichukua sambusa na kuibugia nzima nzima ikawa kama iliyotumbukizwa ndani ya kinywa cha chewa. Kinywa kilikuwa kimemjaa, mashavu yamemvimba, akichakua na kupumua (uk.199)

Tukio hili linatendeka baada ya Denge kukutana na Zanga na Zanga alipoona uso wa Denge ulivyosawajika, midomo imekauka, macho yake yote anamwangalia mwandazi alivyokuwa akipanga vikombe vya chai na sahani za vyakula juu ya meza, ndipo anamwuliza ana njaa ya siku ngapi naye Denge anasema tokea chai ya jana asubuhi hajauma kitu. Denge anapoletewa chakula ndipo anabugia hivyo. Kuna matumizi ya kiambishi 'li' kwenye maneno "alipowekewa", "alifakamia", "alikata", "alinyanyua" na "kilikuwa" kuonyesha kwamba matukio haya hayajatokea wakati huu japokuwa yanasimuliwa sasa. Mifano hii inadhihirisha kwamba kuna masafa baina ya msimulizi na matukio ya hadithi ambayo yanategemea matini au aina ya usimulizi.

### 4.1.2 Usimulizi wa kitabiri

Usimulizi wa kitabiri au usimulizi wa kabla, ni aina ya usimulizi ambao huwa unatokea kabla ya tukio linalosimuliwa kutendeka. Utabiri wa aina hii huwa haupatikani kwenye kazi nyingi. Biblia ndiyo huwa na mifano mingi ya usimulizi wa aina hii na wakati mwingi hubainika kupitia kwa matumizi ya wakati ujao au uliopo. Usimulizi wa kabla hutokea kwenye simulizi zilizo ndani ya simulizi zingine katika miundo ya kinabii, laana au ndoto za wahusika wa kubuni. Prolepsia zote ni mifano ya usimulizi wa kitabiri.

Mfano wa usimulizi wa kitabiri ni pale ambapo Mambo na Bukheti wanazungumza kuhusu jinsi watakavyomtorosha Denge gerezani. Bukheti anamwambia Mambo kuwa:

> Denge atakwenda, atapelekwa mpaka Kismayu na huko atatunzwa vizuri (uk.215)

Mambo anapomsihi Bukheti awasaidie kumtorosha Denge kwa kumtafutia jahazi linalokwenda Kismayu, Bukheti anamwambia kuwa hakuna lisilowezekana kwani majahazi

yale hubeba vitu kwelikweli wala sio boriti, maembe na machungwa tu. Kwenye mazungumzo yao ndipo Bukheti anasema kuwa Denge atakwenda na atatunzwa vizuri. Kuna matumizi ya kiambishi ‘ta’ kwenye maneno “atakwenda”, “atapelekwa” na “atatunzwa” kudhihirisha kwamba ni jambo ambalo bado halijatokea kama tunavyoona kwenye simulizi, japokuwa tunaona baadaye Mambo na Bukheti wanafanikiwa kumtorosha Denge.

### 4.1.3 Usimulizi sawia

Rimmon-Kenan (2002:91) anaufafanua usimulizi sawia kama aina ya usimulizi ambao matukio husimuliwa kadri yanavyotokea. Sanaa za utendaji zikiwemo drama na filamu ndizo huhusisha mitindo ya aina hii kwa kiwango kikubwa. Usimulizi huu huhusishwa na tukio kama vile kitendo cha kuripoti matukio ya kila siku. Riwaya ya *Vuta N’kuvute* ina mifano ya usimulizi sawia kama vile msimulizi anapoeleza jinsi mashua waliyokuwa wameabiri Denge na Mambo ilivyokuwa. Msimulizi anaeleza kuwa:

> Mashua inakata maji, mawimbi yananguruma, maji mpaka ndani. Komamanga inainama na kuinuka ikiyafuata mawimbi vile yanavyopanda na kushuka, yakinjikunja na kunjikunjua, yakijimwaga na kujitandaza juu ya uso wa bahari. Nayo hivyo hivyo, mara iko juu, juu ya mgongo wa wimbi, mara iko chini, kwenye maporomoko ya wimbi. Inawasubiri. Mashua inakaribia, Sukutua ameikamata sukani anaiongoza anaielekeza sawasawa na pale lilipo Komamanga. Denge amekaa upande mmoja wa mashua na Mambo upande wa pili. Denge yuko vilevile na magwanda ya gerezani (uk.243)

Mfano huu unaonyesha jinsi mashua ilikuwa inakwenda ikiyafuata mawimbi wakati mwingine inakuwa juu na wakati mwingine chini kutokana na mawimbi na vilevile jinsi Sukutua alivyokuwa anaiongoza akiielekeza kwenye Komamanga. Usimulizi huu ni sawia kwani tukio hili linasimuliwa wakati linapotokea jambo ambalo linampa msomaji picha halisi ya kinachotendeka. Mbali na hayo, kuna matumizi ya kiambishi ‘na’ cha wakati uliopo kwenye maneno “inakata”, “yananguruma”, “inainama”, “yanavyopanda”, “inawasubiri” na “anaiongoza” na kiambishi “me” kinachoashiria hali timilifu kwenye maneno “ameikamata” na “amekaa” kuonyesha kwamba matukio haya yalisimuliwa wakati yalipokuwa yanatukia.

Vita vya Mwajuma na Yasmin ni mfano wa usimulizi sawia kwani vita vyao vinasimuliwa vinapoendelea. Vita vyao vinatokana na mazungumzo yao baada ya Mwajuma kumwambia Yasmin akubali posa ya Shihab na amsahau Denge. Kwenye harakati ya mazungumzo yao,

Yasmin anamtukana Mwajuma kwa kumwambia kuwa ni kahaba. Msimulizi anasimulia tukio hili kwa msomaji wakati lilipokuwa linatendeka (uk.153)

### 4.2 Aina za usimulizi kwa kuzingatia kigezo cha Nafsi

Tunapoangazia aina za usimulizi kwa kuzingatia kigezo cha nafsi, tunapata kwamba, kuna usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya pili na usimulizi wa nafsi ya tatu. Suala hili linapochunguzwa, huwa ni muhimu kubaini usimulizi unaotokea katika kazi fulani unafanywa na nani. Usimulizi unaopatikana kwenye riwaya ya *Vuta N'kuvute* ni wa nafsi ya tatu.

#### 4.2.1 Usimulizi wa Nafsi ya Tatu

Mofu "a" inapotumika kumtambulisha msimulizi, hubaini moja kwa moja kuwa huo ni usimulizi wa nafsi ya tatu. Kwa kiwango kikubwa, usimulizi wa aina hii ndio hutumika zaidi. Kinachodhihirika wazi hapa ni kuwa, msimulizi huyazungumzia masuala yanayowahusu watu wengine wala siye. Kwa mfano, riwaya ya *Vuta N'kuvute* inapoanza tunasoma kwamba:

> Mara tu baada ya kuvunja ungo, Yasmin aliozwa mume. Alikuwa mume wa jamii yake ya Ithnashiria ambaye alikuwa akiishi jirani naye hapo Mtendeni (uk.1)

Kutokana na mfano huu, ni wazi kwamba huu ni usimulizi wa nafsi ya tatu kwa kuwa kuna matumizi ya mofu "a" inayoambatanishwa na vitenzi kama vile "aliozwa" na "alikuwa", msimulizi anapomzungumzia Yasmin. Maelezo haya yanaonyesha kuwa usimulizi huu unafanywa na mtu asiye mhusika hadithini.

Usimulizi wa aina hii unapotumika, huonyesha kuwa msimulizi ana ufahamu wa siri na mambo yote kwani hata huwa na uelewa wa kila kitu kinachowahusu wahusika, mandhari, hadithi, mwelekeo, saikolojia ya viumbe wa hadithini na mambo mengine. Uelewa mwingi wa matukio kwa msomaji hutokana na ufichuzi wa msimulizi unaotokana na uelewa wake wa mambo anapoingia akilini mwa mhusika na kusimulia yanayompitikia pamwe na mijadala yake. Kwa mfano, msimulizi anapotueleza kumhusu Yasmin alipofika kwa Mwajuma baada ya mazungumzo yake na Koplo Matata. Anaeleza kwamba:

> Yasmin aliingia chumbani na kujinyosha kitandani na hapo hapo usingizi mzito ulimchukua. Alilala mpaka mchana na alipoamka Mwajuma hakuwepo. Alibakia palepale kitandani na hapo

> mawazo ya mkasa uliomtokea jana yalianza kuzagaa kichwani mwake. Maneno ya Koplo Matata yalivuma kwa nguvu masikioni mwake na alimsikia waziwazi akimwambia kwamba atarejeshwa kwa mumewe, azidishe uhusiano wake na Denge, ampelekee habari zote za Denge, Denge koministi, kafiri hivi na vile. Kichwa kilimdhuru akajiona amezama ndani ya bahari ya matatizo. Yote aliyoambiwa juu ya Denge aliyasikia tu lakini hayaelewi hata kidogo. Hakujua aanzie wapi katika kazi aliyopewa na Koplo Matata, kazi ambayo ni kinga ya pekee itakayomnusuru kurudishwa kwa Bwana Raza (uk.91)

Kutokana na mfano huu, ni wazi kwamba, usimulizi uliotumika hapa ni wa nafsi ya tatu kutokana na uelewa wa mambo yote yanayomhusu Yasmin kutokana na kueleza yanayompitikia akilini anaposema, "hapo mawazo ya mkasa uliomtokea jana yalianza kuzagaa kichwani mwake". Hili ni dhihirisho kwamba msimulizi ana uwezo wa kuingia akilini mwa mhusika na kumfichulia msomaji mawazo ya mhusika huyo. Mijadala inayotokea akilini mwa Yasmin ni kuhusu vile atarejeshwa kwa mumewe, jinsi atazidisha uhusiano na Denge, Denge kuwa komunisti na kafiri. Mambo haya kama wasomaji tumeyafahamu kutokana na uwezo wa msimulizi wa kutueleza zaidi kuhusu Yasmin.

Usimulizi wa nafsi ya tatu unapotumika, huwa haumfungi msimulizi mahali pamoja kwani anaweza kuwa sokoni na baada ya muda mfupi akawa kwenye msitu. Kwa mfano, msimulizi anapomaliza kueleza kumhusu Yasmin, dondoo lifuatalo linatueleza kuhusu Bukheti.

> Bukheti alijiona kama aliyebeba mzigo uliompotea. Umemuemea, mzito hakuna mtu wa kumtua. Amefika nyumbani mnyonge moto wa mapenzi unarindima ndani ya moyo wake, hakuna wa kuupoza, hakuna wa kuuzima. Hapo kwao jana kucha Bwana Bashiri hakulala, alipita akihangaika vibarazani kumtafuta yeye ambaye naye amekesha kuyatafuta mapenzi. Mapenzi yenyewe yamepeperuka, hayoo, yamepotea, yamle, hana tamaa nayo tena. Bora arudi Mombasa (uk.91)

Ni kweli kwamba, usimulizi wa nafsi ya tatu unapotumika msimulizi huwa hafungiki mahali maalum. Huu ni mfano mzuri kwani dondoo la kwanza msimulizi anatuelezea kumhusu Yasmin na mawazo yaliyokuwa yanampitikia akilini mwake na kisha dondoo linalofuata tunampata msimulizi nyumbani mwa Bwana Bashiri. Anapopatikana nyumbani kwa Bwana Bashiri, anasimulia jinsi Bukheti alivyokuwa anahangaika kwa ajili ya mapenzi yake kwa Yasmin kiasi cha kutolala nyumbani usiku uliopita na kumfanya Bashiri kumtafuta. Anaonelea afadhali arudi Mombasa aache kuhangaika.

### 4.3 Utambuzi wa msimulizi

Msimulizi kama asemavyo Rimmon-Kenan (2002:90), ni ajenti ambaye husimulia au hushiriki kwenye shughuli zinazohusisha usimulizi. Viwango vya utambulisho wa msimulizi vinaweza kutofautiana kutokana na msimulizi anayepatikana kwenye matini husika. Msimulizi anaweza kutambulishwa kwa uwazi au asitambulishwe. Baadhi ya sehemu za matini zinaweza kumtambulisha mhusika waziwazi na zingine zinaweza kukosa kumtambulisha waziwazi. Ishara zitumiwazo kwenye utambuzi wa msimulizi ni ufafanuzi wa mandhari, utambulisho wa wahusika, muhtasari wa muda na kuwaeleza wahusika.

#### 4.3.1 Ufafanuzi wa mandhari

Kwenye riwaya za kibunilizi, mandhari huwa yanaelezwa kwa lugha ya msimulizi na huelezwa kwa kina yakilinganishwa na filamu au tamthilia ambazo hujihusisha zaidi na matendo ya wahusika. Riwaya ya *Vuta N'kuvute* ina mifano ya ufafanuzi wa mandhari unaoashiria uwepo wa msimulizi kama tunapopata ufafanuzi wa chumba cha Bwana Raza.

> Chumba cha Bwana Raza kilikuwa kimejaa makorokocho. Mifuko ya unga, mikungu ya ndizi, maboksi ya majani ya chai na makopo ya maziwa. Kuta za chumba hicho zilikuwa zimepambwa na picha mbili tu, moja ni picha ya maandishi yaliyokuwa na nakshi ya Kiarabu majina ya Fatma, Ali, Hassan na Hussein. Picha ya pili ilikuwa ni ya farasi aliyebeba mkono ulioonyesha vidole vyote vitano. Mlikuwa na kiti kizuri cha msaji kilichongongwa kwa nakshi pembeni na miguuni. Bwana Raza alinunua kiti hicho Darajani kwenye mnada. Kwenye pembe nyingine ya chumba hicho mlikuwa na kiti cha marimba na juu yake palikuwa na rafu iliyogongomelewa kwa misumari ukutani. Kwenye rafu hiyo, palitundikwa maguo machafu na kwenye kijiti cha mwisho cha rafu hiyo ilining'inia tasbihi ndogo (uk.2)

Kutokana na maelezo ya chumba cha Bwana Raza, tunapata kufahamu kuwa kuna mtu anayesimulia na anachukuliwa kama mtazamaji ambaye ni msimulizi. Hili linatokana na kuwa, anaonyesha ufahamu wa chumba cha Bwana Raza kwa kuonyesha jinsi kilivyojaa makorocho, mifuko na picha zilizotundikwa ukutani. Vilevile tunapata kufahamu kwamba kuna kiti kizuri alichokinunua Darajani mnadani. Mandhari yanaelezwa kwa kutumia lugha na ufafanuzi ambao unaonyesha kuwa sio wa mhusika bali ni wa msimulizi-mtazamaji. Mfano mwingine wa ufafanuzi wa mazingira ni pale ambapo tunaelezwa kuhusu mandhari ya Darajani.

> Kwa wana mji wa Zanzibar, Darajani ni pahala maarufu sana. Siku zote Darajani huambatanishwa na wingi wa maduka, biashara za kila aina na wingi wa magari. Darajani pia huambatanishwa na shughuli za kidini kama vile "Jahusein" siku za Muharram na maandamano ya dhikiri yanayopitia hapo kila siku ya Ijumaa baada ya wachamungu kumaliza kusali El-jumaa. Pia Darajani ni midani ya wanasiasa wanapotaka kuhutubia mikutano ya hadhara. Hali kadhalika, Darajani ni maarufu kwa misururu ya mafukara wanaoranda sehemu hiyo na makopo yao mikononi wakipita madukani na kuomba, "Yalla masikini Yalla masikini". Lakini Darajani vilevile huambatanishwa na wahuni, wavuta bangi, wezi na walevi wa spiriti (uk.122)

Tunapopata ufafanuzi wa Darajani, tunafahamu kwamba ni mahali ambapo pana umaarufu sana na kuna maduka mengi, biashara mbalimbali na magari mengi. Vilevile tunafahamu kwamba huwa ni mahali pa wanasiasa ambapo huenda kuhutubia, kuna masikini wengi ambao huombaomba na wavuta bangi, wezi na walevi wa spiriti. Kutokana na maelezo haya, tunafahamu kwamba kuna msimulizi anayedhihirika kama mtazamaji. Mfano mwingine wa ufafanuzi wa mandhari ni pale ambapo tunaelezwa au kufafanuliwa chumba cha Shihab.

> Mandhari ya chumba kile yalikuwa ya anasa tupu. Makochi ya vitambaa vya mahmel, sakafu imetandikwa zulia nene la Kiajemi, makabati makubwa ya vioo yaliyojaa sahani, mabakuli na vikombe vya asili, mapambo ya kila aina na radio kubwa iliyofunguliwa kwa sauti hafifu kuleta muziki mwororo. Taa ya buluu iliyokuwemo chumbani mle ilitoa mwanga dhaifu (uk.176)

Mandhari ya chumba cha Shihab yameelezwa vizuri pale ambapo tunafahamu kuwa kulikuwa na vitambaa vya mahmel, zulia la Kiajemi, makabati makubwa makubwa ya vioo yaliyojaa sahani, mabakuli na mapambo ya kila aina. Kutokana na maelezo haya, kuna udhihirisho kwamba kuna mtu anayesimulia au kueleza mandhari haya ambaye ni msimulizi.

### 4.3.2 Muhtasari wa muda

Muhtasari wa muda huleta hamu ya kueleza muda ulivyopita kihadithi, ili kujibu maswali aliyo nayo msimuliwa kuhusu kilichotendeka kwa muda fulani. Msimulizi anaweza kuamua kueleza kilichojiri kwa muda fulani kwa kifupi. Muhtasari wa muda huwa ni dhihirisho la uwepo wa msimulizi ambaye huamua ni sehemu gani ya simulizi inahitaji wakati mwingi kusimuliwa na inayohitaji muda mchache. Kwa mfano, maisha ya Denge yanapoelezwa kwa kifupi ni mfano wa muhtasari wa muda kwenye riwaya ya *Vuta N'kuvute* kama ifuatavyo:

> Denge alimaliza darasa la nane skuli ya Gulioni na alifuzu vizuri mtihani wake. Aliingia darasa la tisa Government Secondary School. Alimaliza darasa la 12 na alishinda mtihani wa Cambridge

> daraja la kwanza. Mwaka huo huo aliajiriwa kazi ya ukarani katika Baraza la mji wa Zanzibar. Mwaka mmoja baadaye, mwanasiasa mmoja alimshauri kwenda Urusi kusoma (uk.64)

Kutokana na mfano huu, ni dhihirisho kwamba kuna msimulizi ambaye ameamua kuyaeleza maisha ya Denge kwa kifupi. Maisha ya Denge yanaelezwa tunapofahamu kuwa alisomea skuli ya Gulioni na kufuzu vizuri kwenye mtihani wake, akasomea Government Secondary School na kushinda mtihani wa Cambridge hadi kuajiriwa kwake na baadaye kwenda Urusi kusoma. Msimulizi ameamua sehemu hii ndiyo muhimu kuieleza kumhusu Denge na hajaipa muda mwingi kuieleza. Uwepo wa msimulizi unatambulika kutokana na kuwa anaonekana kumfahamu vyema Denge tokea shule ya msingi hadi kuajiriwa kwake na kwenda Urusi. Mfano mwingine wa muhtasari wa muda ni pale ambapo tunampata Mwajuma na kupata maelezo yake.

> Ilikuwa siku ya jumapili iliyopambazuka vizuri, kiasi cha saa tano za asubuhi na Mwajuma ameamka na nishai za pombe ya jana usiku, yuko uani anafua. Akifua huku akiimba (uk.75)

Muhtasari wa muda unaodhihirishwa na maelezo ya siku ya Jumapili na saa tano asubuhi, ni dhihirisho tosha kwamba kuna msimulizi kwa kuwa anamfahamu Mwajuma na siku yenyewe na saa alipokuwa akifua huku akiimba. Msimulizi ameona jambo lililo muhimu ni kusimulia kuwa Mwajuma alikuwa anaosha akiwa na nishai za pombe huku akiimba.

### 4.3.3 Uelezaji wa wahusika

Ufafanuzi wa wahusika huonyesha ujumla au muhtasari kwa upande wa msimulizi pamoja na hamu ya kuwasilisha wasifu wake kwa sauti yenye nguvu zaidi ambayo ni ya msimulizi. Kwa kuwa msimulizi wa hadithi huwa nje ya hadithi anayoisimulia, ujumbe anaoutoa huaminika na msimuliwa bila kuuchunguza upya. Kwa mfano, tunapopata taswira ya Mwajuma, tunafahamu kwamba kuna msimulizi anayewatazama wahusika wake.

> Alikuwa ni mwanamke wa makamo tu, hazidi miaka ishirini na tano lakini umbile lake la wembamba lilimfanya aonekane yuko chini ya umri huo. Alikuwa na kisauti kikali azungumzapo kila jirani hujua kwamba Mwajuma yupo (uk.4)

Ujumbe unaopatikana kumhusu Mwajuma, unaonekana wa kuaminika kwa kuwa umetoka kwa msimulizi ambaye anaonekana kuwa na ufahamu wa mhusika huyu. Vilevile, sauti ya msimulizi huchukuliwa kuwa ya kuaminika kwani huwa hana mapendeleo. Riwaya ya *Vuta*

*N'kuvute* ina mfano mwingine wa uelezaji wa mhusika tunapopata maelezo kumhusu Sukutua.

> Alikuwa na kiduka kidogo akiuza urembo hapo Mchangani na kwa biashara yake hiyo pesa mbili tatu za kutumia hazikumpa shida. Kila wakati anazo. Biashara hiyo pia ilimpa umaarufu mkubwa kwa wanawake na ndiyo maana alikuwa hatoki densini kwani huko ndiko hukutana na wengi wa wale wateja wake (uk.45)

Msimulizi ndiye anamfahamisha msomaji kwamba Sukutua alikuwa na kiduka kidogo na hakuwa na shida ya pesa, alikuwa maarufu kwa wanawake kutokana na biashara yake na alikuwa hakosi kwenda kwenye densi ili apate wateja huko. Sauti inayozungumza ndiyo ya msimulizi. Sehemu inayofuatia tutaeleza kuhusu mtazamo, aina zake kuu na sawia zinazotumika kwenye uchunguzi wake.

## 4.4 Mtazamo

Mtazamo hueleza jinsi msimulizi hutazama na mahali ambapo huwa kwenye hadithi. Msimulizi wa hadithi anapokuwa sehemu ya anachokisimulia, hubainisha mtazamo wa ndani na anapokuwa nje ya hadithi hiyo mtazamo wake huwa wa nje.

### 4.4.1 Aina kuu za mtazamo

Ili kubainisha aina za mtazamo, vigezo viwili huzingatiwa ambavyo ni nafasi ambayo inachukuliwa ya kutazamia matukio na mikabala ya mwandishi. Vilevile, umbali wa mhusika unaweza kutumika kama kigezo cha kubainisha aina za mtazamo. Kwa kuangazia aina za msimulizi, tunaweza kupata usimulizi wenye mtazamo wa nafsi ya kwanza, usimulizi wenye mtazamo wa nafsi ya pili na usimulizi wenye mtazamo wa nafsi ya tatu. Uainishaji wa aina hii unapotokea huwa unaangazia anayesimulia pamoja na uhusiano wake na hadithi. Aina mbili kuu za mtazamo ni mtazamo wa ndani na mtazamo wa nje.

Mtazamo wa ndani ni aina ya mtazamo ambayo huhusishwa na hadithi ambazo husimuliwa kwa kutumia nafsi ya kwanza. Aina hii hujihusisha sana na mhusika ambaye ni msimulizi wa hadithi anayoisimulia. Viwakilishi "mimi" na "ni" ndivyo hutumika na husaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza masafa baina ya mhusika na msomaji kwa kuwa, huweza kujitambulisha na mtazamo uliochukuliwa na mhusika.

Mtazamo wa nje kwa upande wake ni aina ya mtazamo ambao huhusishwa sana na matumizi ya nafsi ya tatu. Mtazamo huu huwa hauko hadithini pekee mbali huweza kuwa nje yake. Msimulizi anayepatikana hapa huwa si mmoja wa wahusika wa hadithi bali huwa haonekani na huripoti pamoja na kutoa maoni huku akiona matukio ya hadithi akiwa nje. Mtazamo wa nafsi ya tatu unapotumika, msimulizi huwa ana ufahamu wa kila jambo na huwa anapatikana popote. Msimulizi wa aina hii anao uwezo wa kuingia kwenye akili ya mhusika na kumjuza msomaji mawazo na hisia za mhusika fulani. Mtazamo wa nje unapotumika, mwandishi huwa na uwezo wa kuchunguza masuala ambayo hayangewezekana kwa mtazamo wa ndani. Kwa mfano anapoeleza kuhusu Yasmin anasema:

> Yasmin hakupenda hata kidogo kuolewa na mume kama yule kwani yeye mwenyewe angelipenda sana kupata mume kijana kama yeye mwenyewe. Alipenda ampate mume ambaye yeyote angelimwona angelisema, "kweli Yasmin kapata mume". Alikuwa anatamani kupenda lakini hakumpata wa kumpenda. Yeye alitaka kijana wa makamu yake ambaye angelimwonyesha pendo na yeye angelimiminia pendo lote moyoni mwake (uk.1)

Usimulizi hapa unamhusu Yasmin kwani siye anayesimulia hadithi. Msimulizi ambaye haonekani na ambaye si mhusika hadithini ndiye anayesimulia na anaonekana kumfahamu Yasmin kabisa kwani anasema "Yasmin hakupenda kuolewa na mume kama yule". Msimulizi anamtazama Yasmin akiwa nje ya hadithi.

### 4.5 Sawia za uchunguzi wa mtazamo

Sawia za uchunguzi wa mtazamo huhusisha viwango mbalimbali ambavyo hutumiwa kwenye uchunguzi wa mtazamo. Kilichoko muhimu hapa ni jicho analotumia msimulizi kuyatazamia matukio na sehemu ambayo huwa anatazamia. Sawia za mtazamo tunazoainisha ni sawia ya mwanda-wakati, sawia ya kisaikolojia na sawia ya kitathmini.

#### 4.5.1 Sawia ya mwanda-wakati

Utambuzi unaohusishwa na nafasi na wakati kwa kuzingatia mkabala kwenye riwaya, ndio hushughulikiwa hapa. Maana ya ujumbe huathiriwa na nafasi iliyopo baina ya msimulizi na msimuliwa. Anayesimuliwa na vinavyosimuliwa vinaweza kuwa vimekaribiana au vikawa na umbali. Alikosimama msimulizi na wakati anaposimulia ndivyo huwa muhimu zaidi. Vielekezi vya lugha ndivyo vya kimsingi vya mwanda-wakati na huwasilishwa kwa matumizi ya vielezi vya mahali. Kwa mfano tunasoma:

> Mara tu baada ya kuvunja ungo, Yasmin aliozwa mume. Alikuwa mume wa jamii yake ya Ithnashiria ambaye alikuwa akiishi jirani naye hapo Mtendeni (uk.1)

Katika dondo hili, neno "hapo", limetumika kama kielekezi cha umbali kuonyesha umbali uliopo kati ya anayesimulia na kile ambacho kinasimuliwa. Hili linaonyesha kwamba, msimulizi yuko mbali kidogo na eneo la Mtendeni. Mfano mwingine ni pale ambapo Denge anamtafuta Mambo. Tunaelezwa kwamba:

> Watu walitapakaa nje ya Banda la Mbata, wamesimama vichunguvichungu na kila kichungu kilikuwa na lake kwani eneo lile lilikuwa na vimbiti vya kila aina. Hilo lilikuwa eneo la wale waliovunjika moyo na maisha na wao waliishi ndani ya vibanda vidogovidogo vilivyolizunguka Banda la Mbata. Vibanda hivyo ndivyo vilivyokuwa maskani yao na humo kutwa kucha walijilevya vileo vya kila aina kujipumbaza na maisha (uk.47)

Vielekezi vya umbali vimetumika kwenye mfano huu ambavyo ni "lile", "hilo" na "hivyo". Vielekezi hivi vinaonyesha kwamba msimulizi hayuko karibu sana na anachokisimulia. Mfano mwingine ni pale ambapo tunampata Bukheti na Bwana Bashiri wakiwa sokoni na shughuli zao za kila siku pale. Tunasoma:

> Hiyo huwa ni kazi yake ya kutwa, kila siku. Shughuli hizo hufayika katikati ya vurugu na kelele zilizojaa sokoni hapo. Sehemu ya mbele ya soko hilo kuna baraza ....... Kule pembeni kuna mikahawa ya wauza supu na maharagwe. Imejaa walaji. Huyu kaagiza supu ya mafupa, huyu ya miguu ya mbuzi, huyu supu ya utumbo, kelele mtindo mmoja (uk.82)

Mfano huu unadhihirisha kuwa vielekezi vya umbali na ukaribu vinaweza kutumiwa pamoja kama vile matumizi ya " hiyo", "hizo", "hilo" na "huyu". Neno "huyu" vilevile limerudiwa kuonyesha kuwa, linamshawishi msomaji kuona shughuli ambazo hutokea pale sokoni. Kila mtu pale sokoni ameshughulika pamoja na mikahawa ya supu. Umbali uliokuwepo baina ya msimulizi na soko umefupishwa kwa matumizi ya neno "huyu".

Tunapoangazia wakati au mahusiano ya wakati kwenye riwaya, tunaweza kuangalia kama matukio yamesimuliwa kwa wakati uliopita, uliopo au wakati ujao na kila njeo huibua mtazamo tofauti. Viashiria vya wakati vinapotumiwa huonyesha umbali au ukaribu uliopo baina ya matukio yanayosimuliwa na wakati ambao yanasimuliwa. Kwa mfano, tunapokutana na Kamishna wa polisi tunagundua kwamba,

> Siku ile ilikuwa ni siku ngumu kwa Kamishna wa polisi, siku ambayo ilipambazuka kwa matukio ya ajabu, yasiyo ya kawaida. Kwake yeye ajabu ile ilikuwa kama kwamba jua limechomozea upande wa magharibi, kwani tokea kuanza kwake kazi Zanzibar, si kama kwamba hazikupata kutokea harakati za kisiasa, lakini ya leo yameleta fora (uk.169)

Kutokana na mfano huu, ni wazi kwamba msimulizi yupo karibu na matukio anayoyasimulia. Hili linathibitishwa na matumizi ya viashiria vya wakati ambavyo ni "siku ile" na "leo". Msimulizi anasimulia jinsi Kamishna alivyokuwa na wasiwasi siku ile kutokana na makaratasi yaliyokuwa yametapakaa kote yakisomwa na wananchi mjini Zanzibar.

### 4.5.2 Sawia ya kisaikolojia

Sawia ya kisaikolojia hujihusisha na akili na hisia za msimulizi kwa msimuliwa au kisimuliwa kama asemavyo Rimmon-Kenan (2002:80). Utambuzi wa kazi alionao mhusika pia huwa kwenye sawia hii. Wamitila (2002:51) anasema kuwa, sifa za lugha ndizo hutumika kuyatambua mawazo ya mhusika. Ili kuelewa sawia ya kisaikolojia, utambulisho wa maneno yajulikanayo kama "maneno ya hisia" huangaziwa. Kwa mfano, tunapompata Yasmin akiwa chumbani na Bwana Raza tunabaini kuwa:

> Alikuwa mbali katika mawazo akifikiri vipi ataweza kumwepuka mzee yule, lakini kila alipofikiri hakuweza kupata kisingizio chochote cha kumkataa mumewe (uk.4)

Mfano huu unaonyesha mawazo yanayompitikia Yasmin akilini na mtazamo alionao kuhusu Bwana Raza kwani anaonekana kutafuta kisingizio chochote cha kumkataa bila mafanikio. Neno "alipofikiri" ni neno la hisia linaloonyesha mtazamo wa kisaikolojia wa Yasmin. Neno kama hili linapotumika husaidia msomaji kufahamu hisia za mhusika fulani kana kwamba mhusika huyo alikuwa anasimulia matukio yake moja kwa moja.

Mfano mwingine ni wa Koplo Matata anapowaza baada ya kupewa kazi ya kumtafuta Denge kwa lolote lile. Tunasoma:

> Aliwaza aende wapi wakati ule, lakini alipigwa na mshangao mkubwa alipofika senema ya "majestic" na kumkuta Yasmin peke yake, anatazama matangazo ya senema (uk. 69)

Neno "aliwaza" limetumika kuonyesha mtazamo wa kisaikolojia wa Koplo Matata unaosababishwa na hamu yake ya kumkamata Denge. Matumaini yake yanaonekana kuzaa

matunda anapomwona Yasmin kwenye senema kwani alijua kuwa atapata habari za Denge. Mfano mwingine ni wa Yasmin alivyokuwa akihisi baada ya kufika Mombasa.

> Lakini leo wiki ya pili, Yasmin anajihisi amepwaya ndani ya nyumba amezongwa na upweke kila pembe, hana wa kuzungumza naye. Kutwa kuchungulia madirishani. Lakini Yasmin hakutoshelezwa na kukaa akisikiliza waimbaji wakighani na kutetea, bali mara mojamoja husimama katikati ya ukumbi akacheza (uk. 10)

Kutokana na mfano huu, tunapata kufahamu hisia za Yasmin kwamba alikuwa anajihisi yuko mpweke pale chumbani kwani hakuwa anaenda sokoni kumsaidia mumewe mbali alisalia nyumbani tu. Msimulizi anawasilisha mawazo ya Yasmin na kuonyesha jinsi yanavyomuathiri kihisia na kiakili. Jambo hili linawezekana kutokana na uwezo wa msimulizi wa kuwa na ufahamu wa kila kitu kinachompitikia Yasmin.

### 4.5.3 Sawia ya kitathmini

Sawia hii hujihusisha na mfumo wa kuutazama ulimwengu kwa kuangazia jinsi matukio na wahusika wa hadithi wanavyoangaziwa na wanavyoangazia matukio yanayosimuliwa. Msimulizi anapotathmini matukio, huwa anaonyesha mwelekeo anaouchukua au anachokiegemea ki-itikadi. Mtazamo wa msimulizi huchukuliwa kwa uzito. Tathmini ya ki-itikadi vilevile inaweza kufanywa kupitia kwa mhusika mkuu akiwa amewasilishwa kwa tathmini yake au tathmini ya msimulizi ikatumika kumwasilisha. Kwa ujumla, sawia hii hujihusisha na Maadili na kanuni zilizoko simulizini. Kutokana na hayo, tutachunguza kanuni za kiimani, maadili, mitazamo na maoni ya ulimwengu yaliyoko kwenye riwaya ya *Vuta N'kuvute* kuhusu masuala fulani. Kwa mfano, tunafahamu kuwa Yasmin hakupenda kuolewa na Bwana Raza lakini wazee wake walimuoza kwa kuwa alikuwa wa jamii yake ya Ithnashiria. Tunaelezwa:

> Kukubali kwake kuolewa ilikuwa ni kwa sababu ya kuwaridhi wazee wake tu. Yeye hakuona fahari ya kuolewa na mzee anayeweza kumzaa. Hakupenda kufuatana na mumewe pahala popote pale na hata ile siku iliyotokea wakaenda senema, basi yeye huwa hapendi kukaa karibu naye. Yasmin hakupenda hata kidogo kuolewa na mume kama yule kwani yeye mwenyewe angelipenda sana kupata mume kijana kama yeye mwenyewe (uk.1)

Mfano huu unaashiria wazi kwamba, Yasmin hakupenda kuolewa na Bwana Raza kwani ni mzee kwake na angeweza kumzaa. Jambo linalomfanya kuolewa naye ni kuwaridhisha

wazee wake tu mbali yeye hakutaka vile. Hapa, msimulizi anatathmini matukio na kuonyesha kuwa Yasmin hakupenda kuolewa na Bwana Raza kutokana na matumizi ya maneno kama "yeye hakuona fahari", "hakupenda" na "angelipenda". Huu ni mtazamo wa msimulizi kuhusu Yasmin na ndoa yake na Bwana Raza. Mfano huu unaonyesha wazi kwamba Yasmin hakuwa na uwezo wa kujichagulia mume mbali angechaguliwa tu na wazee wake na mume wa jamii yake. Baadaye, Yasmin wanakosana na mumewe na kuamua kuondoka na anaenda kwa mjombake ambapo tunaona mtazamo wake wa kitathmini anaposema:

> Mjomba, kusema ukweli thawabu, mimi nimeshindwa kuishi na Bwana Raza. Kwa hakika, mimi sikumpenda wala sikumtaka. Nilikubali kuolewa naye kwa kukuridhini nyinyi wazee wangu tu (uk.16)

Yasmin ni mhusika mkuu na ametumiwa kufanya tathmini ya ki-itikadi. Yasmin ametumika kama mlengwa kuwakilisha wanawake wanaolazimishwa kuolewa na watu wasiowapenda ili wawaridhishe wazee wao. Yasmin anasema kuwa ameshindwa kuishi na Raza kwa kuwa hakumpenda wala kumtaka. Baada ya hapo, tunapata tathmini ya ki-itikadi inayowasilishwa na mjombake Yasmin anapomwambia:

> Hapa palikuwa kwenu kabla hujaolewa. Sisi tulikupa mume ili tupungukiwe na mzigo. Sasa madhali umemkimbia mumeo, tafuta pa kwenda (uk16)

Haya ni maneno ya mjombake Yasmin anapomwambia aondoke kwani hapo si kwao na aende akaolewe na anayempenda. Mtazamo wa ki-itikadi wa mjombake Yasmin unaonyesha kuwa, mwanamke anapoolewa huwa nyumbani kwao si kwao tena. Vilevile, mtazamo wake unaashiria kuwa, mwanamke huozwa ili kupunguza mzigo. Mwanamke anachukuliwa kama kifaa ambacho kinaleta mzigo kwenye familia na akiolewa hana uhuru wa kurudi kwao hata kama ndoa yake ina matatizo anafaa kuvumilia. Mfano mwingine ni pale ambapo tunaelezwa kuhusu Kamishna. Tunasoma:

> Kamishna akaendelea kuropoka mpaka akachoka kusema, akanyamaza, akamtazama Inspekta Wright ambaye naye alikuwa ametulia tuli, akamwambia "*Take him back to prison*" (uk.182)

Mfano huu unaonyesha jinsi msimulizi anavyotathmini kitendo cha Kamishna. Neno "kuropoka" linaashiria kuwa huu ni mtazamo wa kitathmini wa msimulizi. Vilevile, tunabaini kuwa, msimulizi hajajitambulisha na kile ambacho Kamishna anasema.

### 4.5.4 Sawia ya kilugha au kiisimu

Sifa za lugha pamwe na za kiisimu ndizo hushughulikiwa kwenye sawia hii. Mtazamo wa msimulizi unaweza kubainika kupitia kwa maneno atakayotumia, majina yanayopatikana kwenye kazi yake na sifa za lugha anayotumia.

Matumizi ya majina ni sifa moja inayopatikana kwenye sawia hii. Matumizi ya majina ni kipengele muhimu kwani hubeba maana ambazo huelekeza jinsi msomaji atakavyoichukulia kazi fulani kupitia kwa utambuzi wa wahusika na msuko. Majina ambayo hutumiwa katika riwaya ni majina ambayo hupatikana katika jamii, yanaweza kuwa majina ya lakabu au majina yanayohusiana na tabia au wasifu wa kitu fulani lakini yanapotumiwa kisanaa huwasilisha au kupitisha mitazamo mbalimbali. Riwaya ya *Vuta N'kuvute*, imetumia majina kwa njia mbalimbali kuonyesha sifa fulani kuhusiana nayo. Kwa mfano, Mambo anapokuwa kwenye mazungumzo na Denge, tunaona jinsi anavyomwita. Anasema:

> Unajua De, sasa iko haja ya kubadili mbinu, lakini kuna jambo moja nzuri, mpaka sasa inaonyesha wasiwasi wao ni wewe tu bado hawajawajua jamaa wengine (uk.115)

Sifa inayobainika hapa ni ya ufupishaji wa jina ambapo Mambo anamwita Denge "De". Sifa hii inapojitokeza huashiria kwamba wahusika hawa wana ukaribu sana wa kihisia. Hapa, tunabaini kuwa hisia zilizopo ni za kutaka kufanya mabadiliko ya mbinu walizokuwa wanazitumia kwenye mapambano. Mfano mwingine wa aina hii ni pale ambapo Denge anakutana na Sukutua. Tunaelezwa:

> Sikiliza Suku, hata nikitaka, Waingereza hawakubali kumpa kazi mtu kama mimi (uk.46)

Denge ametumia jina "Suku" kuonyesha ukaribu alionao wa kihisia na rafikiye ambaye anamhurumia kwa kuwa hana kazi. Sukutua anamhurumia Denge ambaye hana kazi na anaogopa kumpa hela kwani anaogopa akionekana atakamatwa. Baada ya Sukutua kusema hayo, ndipo Denge anamwita "Suku" na kumweleza kuwa hata atafute kazi Waingereza hawawezi kumpa. Hisia za ukaribu zinadhihirika kwa kuwa hawa ni marafiki walio na nia moja ya kupigania uhuru wa nchi yao. Tunapopatana na Denge na Mambo, tunaona kwamba kuna ukaribu uliopo baina yao kutokana na majina wanayoitana na pia ukaribu ule unapotea.

> "Nikwambie nini brother, Yasmin kasema atakuja leo" (uk.102)

Maneno haya ni ya Denge anapomwakikishia Mambo kuwa wikendi itakuwa nzuri kwa kuwa Yasmin alisema kuwa atakuja kuwatembelea pamoja na Mwajuma. Denge anatumia jina "brother" kumwita Mambo kuonyesha ukaribu walionao wa kindugu kwani walikuwa marafiki wa karibu sana. Hili linaonyesha kuwa kuna ukaribu wa kihisia baina yao. Hata hivyo, mfano unaofuatia unaonyesha umbali wa kihisia baina ya Mambo na Denge. Tunasoma:

> "Sasa wewe Mambo unataka kujifanya hodari sana au vipi? Kila mwanamke mzuri unamtaka wewe, juzi uli..." (uk.103)

Kutokana na mfano huu, Denge anatumia jina "Mambo" ambalo linatumiwa na msimulizi wa hadithi kuonyesha kuwa ule ukaribu wao wa kihisia umepotea. Hili linatokana na Mambo kusema kuwa Yasmin atakuwa wake ilhali alijua kuwa Denge ni mpenziwe. Hisia za ukaribu zinapotea kwani Denge ameudhika na maneno ya Mambo na tabia yake ya kupenda kila mwanamke mzuri.

Vilevile, jina la utani au majina ya kimajazi yanaweza kutumiwa kuonyesha mtazamo alionao msimulizi au mhusika fulani kuhusu mhusika mwenzake. Majina ya kimajazi wakati mwingine huonyesha uhalisia wa mhusika fulani. Kwa mfano, Matar amepewa jina la "Bwana Mashughuli" ambalo linaafikiana na tabia yake ya kufanya mambo mengi. Tunaelezwa:

> Watu wanamwita Bwana Mashughuli kwa sababu Matar, kila wakati ni mtu aliyeshughulika. Kazi yake ni kuranda mitaani kutafuta chupa tupu, akazisafishe na kuziuza tena. Huziuza chupa hizo kwa watengenezaji marashi na arki zamda. Nyengine huzipanga dukani kwake Darajani... Kila unapomwona, Matar huwa kaeleka fuko kubwa, limejaa chupa tupu. Ukimhitaji kwake, lazima umvizie. Hujui saa ngapi yupo saa ngapi hayupo. Na nd'o maana wanamwita Bwana Mashughuli (uk.228)

Msimulizi kwenye mfano huu anaonyesha jinsi watu walivyobadili jina la Matar na kumbadika jina la Bwana Mashughuli. Hili linatokana na tabia yake ya kushughulika kila wakati na kuwa vigumu kumpata kwake kwani huwezi kujua wakati yupo na wakati ambao hayupo. Jambo hili linaonyesha kuwa mtazamo walio nao watu kumhusu Matar ni wa mtu anayejishughulisha kila wakati na mambo mengi hasa ya biashara. Watu wanapomwita kwa jina la "Bwana Mashughuli", wanaonyesha ukaribu uliopo kati yao.

Lugha ambayo inatumika inaweza kudokeza sauti ya msimulizi au mwandishi. Tukio linaweza kuelezwa kwa namna tofauti kutegemea anayetazama ambaye anaweza kuwa msimulizi, mhusika au mtazamaji ambaye anayaangalia matukio tu bila kuhusika. Askari kanzu anapokwenda kwa Mwajuma akimtafuta Denge, ana mtazamo wa kuwa Denge ni koministi. Tunasoma:

> Denge ni koministi, kasoma Urusi na watu wa namna hiyo ni hatari sana. Watu namna hiyo hawaamini Mungu, tena wanataka kuleta fujo nchini (uk.57)

Huu ni mtazamo alionao askari kanzu kumhusu Denge kwa kuwa anaona kuwa ni tishio kwa serikali ya watawala. Anamwona Denge kama mtu hatari sana kutokana na kuwa alisomea Urusi na anasema kuwa ni mtu asiyemwogopa Mungu.

Lugha ya askari kanzu inafanywa sehemu ya lugha ya msimulizi kama ifuatavyo:

> Waliotiliwa shaka ni wale waliowahi kufika kwa namna yoyote ile katika hizo nchi za kikoministi, watu ambao walikuwa wengi, wengine wakiranda bila ya kazi kama Denge, wengine wanasiasa, wengine viongozi wa vyama vya wafanyakazi. Kwa vile serikali ya Bwana Sayyid chini ya himaya ya Muingereza ilikuwa haitambui elimu ya nchi za kikomunisti, wataalam wote waliosoma nchini hizo walibakia bila kazi. Wataalam hao kwao walikuwa hatari kwa usalama wa raia wema (uk.64)

Katika mfano wa kwanza, lugha iliyotumiwa ni ya mhusika ambayo inabadilishwa katika mfano wa pili na kuwa lugha ya msimulizi. Ufanano uliopo katika matumizi ya lugha hapa, ni kuwa, mhusika ambaye ni askari kanzu anasema kuwa Denge ni komunisti, alisomea Urusi na ni hatari sana kwa usalama wa nchi na maneno hayo pia yanapatikana kwenye lugha ya msimulizi. Hii ina maana kwamba, askari kanzu na msimulizi wana mtazamo sawia kuwahusu watu waliosomea Urusi kuwa ni watu hatari kwa usalama wa nchi.

Mfano mwingine unaoashiria lugha ya mhusika kuwa lugha ya msimulizi ni pale ambapo Bashiri wanazungumza na Bukheti. Bashiri anasema:

> Kama unataka mke kweli tutakuoza somoye. Wacha mambo ya kwenda kutafuta Maponjoro (uk. 226)

Haya ni maneno ya Bwana Bashiri anayomwambia Bukheti baada ya Bukheti kumwambia kuwa amepata mke. Mjombake anapinga jambo hilo na kumwambia kuwa akitaka mke

aozwe somoye wala si kutafuta maponjoro. Wahindi ndio wanaitwa maponjoro. Maneno ya Bashiri yanageuka na kuwa lugha ya msimulizi anaposema:

> Bukheti akaona mambo yanamzonga. Yeye alikuwa na wasiwasi kwamba kwa kina Yasmin atakataliwa kwa kuwa yeye ni golo. Huku kwao leo Yasmin anakataliwa na kuitwa ponjoro. Hajui uponjoro gani huo aliokuwa nao Yasmin (uk.226)

Mfano wa kwanza unaonyesha lugha ya mhusika ambaye anatumia neno "ponjoro" kumaanisha Wahindi na mfano wa pili unaonyesha lugha ya mhusika ikitumiwa na msimulizi kueleza jinsi Bukheti alivyokuwa anafikiria. Neno "ponjoro" limetumiwa na msimulizi kuonyesha kuwa hiyo ni lugha yake.

## 4.6 Hitimisho

Sura hii imechunguza kipengele cha usimulizi kwa jumla huku ukijikita kwenye aina za usimulizi kwa kutaka kubaini kama hadithi inasimuliwa baadaye, kabla, wakati tukio linapotendeka au kiutabiri ambapo tukio hilo linaweza kutokea au lisitokee. Utafiti umebaini kuwa, usimulizi wa baadaye, kabla na sawia ndio unapatikana kwenye riwaya husika ya *Vuta N'kuvute* ilhali usimulizi changamano haupo. Pamoja na hayo, usimulizi wa nafsi ya tatu unapatikana kwenye matini husika, na ndio umetawala kazi nzima. Vilevile, utafiti wetu ulichunguza utambuzi wa msimulizi na kubaini kuwa, kuna ishara mbalimbali ambazo hutumika kwenye utambuzi wa msimulizi ambazo ni, ufafanuzi wa mandhari, muhtasari wa muda na uelezaji wa wahusika. Pamoja na hayo, mtazamo ulichunguzwa kwa kuangazia aina kuu za mtazamo na sawia mbalimbali zinazotumika kwenye uchunguzi wake. Sawia zilizodhihirika kwenye utafiti ni sawia ya mwanda-wakati, sawia ya kisaikolojia, sawia ya kitathmini na sawia ya kilugha au kiisimu.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.0 Utangulizi

Tasnifu hii imeshughulikia muundo wa simulizi wa riwaya ya Kiswahili kwa kujikita kwenye riwaya ya *Vuta N'kuvute*, kwa kuongozwa na nadharia ya Naratolojia hasa mkabala wa Rimmon-Kenan (2002). Malengo ya utafiti huu yalikuwa matatu ambayo ni kuchunguza muundo wa simulizi katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*, kuonyesha jinsi vipengele vya hadithi, matini na usimulizi vinavyodhihirika katika riwaya hii na kubainisha uamilifu wa vipengele vya simulizi katika kujenga ukamilifu wa riwaya ya *Vuta N'kuvute*. Kwenye uchunguzi wa muundo wa simulizi, vipengele vikuu ambavyo ni hadithi, matini na usimulizi vilichunguzwa. Masuala yaliyoangaziwa ni uhusika pamoja na uwasilishaji usemi na mawazo ya wahusika, wakati pamoja na usimulizi na mtazamo unavyodhihirika katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*. Kinachoangaziwa kwenye sura hii, ni muhtasari na matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo ya tafiti za baadaye.

## 5.1 Muhtasari wa utafiti

Utafiti wetu una sura tano kuu ambazo zimeshughulikia vipengele mbalimbali lakini vinavyohusiana. Sura ya kwanza imejikita kwenye usuli wa mada huku ikionyesha tatizo la utafiti lililopelekea kuwepo na mwanya uliohitajika kuzibwa, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu zilizopelekea uchaguzi wa mada hii, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada husika, msingi wa kinadharia na mbinu za utafiti zilizojumuisha aina ya utafiti na ukusanyaji wa data pamoja na uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

Sura ya pili ilichunguza uhusika na uwasilishaji wa usemi na mawazo ya wahusika. Sehemu hii ilinuia kuonyesha majukumu ya wahusika katika kuendeleza kazi za kifasihi. Kipengele cha usawiri wa wahusika cha njia ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja na jinsi wanavyotumia lugha kwenye usemi na mawazo yao vilijadiliwa.

Kipengele kilichochunguzwa kwenye sura ya tatu ni cha wakati kwa madhumuni ya kudhihirisha unavyojitokeza kwenye riwaya ya *Vuta N'kuvute*. Wakati ulichunguzwa kwa

kuuainisha kwa kuzingatia mpangilio wa matukio, ambapo utafiti ulitaka kudhihirisha kama matukio yanafuatana kiwakati au la, muda wa matukio ambao unahusisha uharakishwaji au upunguzwaji wa kasi ya hadithi na idadi marudio ambayo ilinuia kuonyesha matukio yanatokea mara ngapi na kusimuliwa mara ngapi.

Sura ya nne kwa upande wake ilishughulikia kipengele cha usimulizi na mtazamo kwa kuonyesha aina mbalimbali za usimulizi zikiwemo usimulizi baadaye, wa kiutabiri, usimulizi sawia na usimulizi wa nafsi ya tatu. Vilevile sura hii ilichunguza ishara mbalimbali zinazotumika kwenye utambuzi wa msimulizi. Kwa upande wa mtazamo, ulichunguzwa kwa kuangazia aina kuu pamoja na sawia zitumikazo kwenye uchunguzi wake.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti wetu umebaini kuwa malengo ya utafiti yametimia kutokana na kuwa, vipengele vya hadithi, matini na usimulizi vimejitokeza kwa uwazi pamoja na uamilifu wake katika kujenga ukamilifu wa riwaya ya *Vuta N'kuvute*. Muundo wa simulizi umebainika wazi kutokana na mifano mbalimbali iliyotolewa kutoka katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*, inayoipelekea kueleweka zaidi kutokana na jinsi vipengele vinavyohusiana, kutegemeana na kukamilishana.

Imedhihirika kuwa, usawiri wa wahusika wa moja kwa moja na usio wa moja kwa moja unapatikana kwenye riwaya ya *Vuta N'kuvute* pale ambapo sifa za mhusika zimetajwa moja kwa moja kwa kutumia vivumishi, nomino dhahania na aina nyingine za maneno. Mbinu mbalimbali pia zimepatikana zinazoashiria usawiri usio wa moja kwa moja. Pamoja na hayo, uwasilishaji wa usemi na mawazo ya wahusika yamedhihirika.

Ni bayana kuwa, analepsia na prolepsia zimejitokeza kwenye utafiti, udondoshi, mtuo, muhtasari na onyesho vilevile kama vipengele vya muda wa matukio vikidhihirika. Vilevile, usimulizi banifu, radifu na mosi umepatikana kwenye riwaya husika. Pia imedhihirika kwamba, aina mbalimbali za usimulizi zimejitokeza zikiwemo usimulizi baadaye, usimulizi kabla na usimulizi sawia, ishara mbalimbali za utambuzi wa msimulizi na mtazamo pamoja na sawia zake mbalimbali zipo kwenye riwaya husika.

## 5.3 Mapendekezo kuhusu utafiti wa baadaye

Utafiti wetu ulichunguza muundo wa simulizi wa riwaya ya Kiswahili kwa kujikita kwenye riwaya ya *Vuta N'kuvute*. Utafiti wetu ulichunguza uhusika na uwasilishaji wa usemi na mawazo ya wahusika, wakati, usimulizi na mtazamo kwa kuangazia aina za usimulizi pamoja na msimulizi na utambuzi wake, mtazamo na aina zake kuu na sawia zinazotumika kwenye uchunguzi wake.

Tungependekeza tafiti za baadaye za kazi zingine za Adam Shafi kuhusu muundo wa simulizi kama vile kwenye riwaya ya *Mbali na Nyumbani*, *Kuli* na *Mtoto wa Mama* kwa kutumia nadharia ya Naratolojia kwa kujikita kwenye mikabala mbalimbali.

Vilevile, tunapendekeza kwamba utafiti wa baadaye ufanywe wa kiulinganishi ambapo mtafiti anaweza kulinganisha muundo wa simulizi wa utanzu wa riwaya na hadithi fupi huku ukitumia mikabala mbalimbali ya Naratolojia.

## 5.4 Kiishio

Sura hii imeangazia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo ya tafiti za baadaye za muundo wa simulizi.

# MAREJELEO


Arege, T. (2012) "Narration in Swahili Narrative Poetry: An Analysis of *Utenzi Wa Rasi'l Ghuli*." Tasnifu ya uzamifu. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Bal, M. (2009) *Narratology*: *Introduction to the Theory of Narrative*(3rd Edition). Toronto: University of Toronto Press.

Barthes, R. (1970) *An introduction to the structural Analysis of Narration Discourse*. Blackwell: Oxford University Press.

Burundi na wenzake (2017) "Usimulizi katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali"*. Journals. Udsm.ac.tz. 991-3103-2-PB.

Genette, G. (1980) *Narrative Discourse*: *An Essay in Method*.Ithaca:Cornell University Press.

Khamis, B. (2015) "Uhakiki wa Usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba Cha Moyo Na Mstahiki Meya.*" Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

Kimani, P. (2012) "Arki za simulizi bunilizi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*". Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Kwaka, A. (2018) "Uhakiki wa wakati na uwasilishaji usemi kama vipengele vya Usimulizi katika *Utenzi wa Nabii Isa*". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

Ong'ondi, E. (2005) "Usimulizi katika riwaya ya *Walenisi* ya Katana Mkangi" Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Prince, G. (1987) *A Dictionary of Narratology*. Aldershot: Scolar Press.

Rimmon-Kenan, S. (2002) *Narrative Fiction*: *Contemporary Poetics.(*2nd Edition). London: Routledge.

Shafi, A. Shafi. (1999) *Vuta N'kuvute*. Dar es Salaam, Tanzania: Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

Shitemi, M. (2011) "Usimulizi katika *Utenzi wa Siri Li Asirali".*Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

Wambui, J. (2018) "Usimulizi katika riwaya ya *Dharau ya Ini*." Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi*: Misingi na Vipengele Vyake. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

(2003) *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.

(2008) *Kanzi ya Fasihi I: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers Ltd.